Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI

## Kikao cha Nane – Tarehe 7 Februari, 2013

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu tuendelee na shughuli za leo.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):**

Taarifa ya Mwaka ya Hesabu zilizokaguliwa na Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011 *(The Annual Report and Audited Accounts the Local Authorities Pensions Fund for the Financial Year 2010/2011).*

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na Kanuni yetu iwapo Waziri Mkuu hayupo kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu siku ya Alhamisi na chenyewe kinakuwa hakipo. Kwa hiyo, Waziri Mkuu ana udhuru mwingine.

Kwa hiyo, mnaweza kumkuta Mheshimiwa Shamai Vuai Nahodha, ndiye anayekaimu kiti chake.

Kwa hiyo kipindi cha Maswali ya Waziri Mkuu leo hatuna. Kwa hiyo, tunaendelea na Maswali ya Kawaida, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, ataanza kuuliza swali.

Na. 98

### Mgogoro Kati ya Wafugaji na Wakulima – Kibaha Vijijini

**MHE. ABUU H. JUMAA** aliuliza:-

Pamoja na jitihada za Serikali za kulenga maeneo ya wafugaji na wakulima, bado kumekuwa na migogoro baina ya wafugaji na wakulima ambao umekuwa ukisababisha wakulima kuumizwa na wafugaji ambao hutumia silaha mbalimbali kuwashambulia wakulima pale hali ya kutoelewana inapotokea kama ilivyotokea kwenye kijiji cha Miziguni tarehe 4 Oktoba, 2011 ambapo wafugaji walipowavamia wakulima wakasababisha majeraha makubwa sana:-

Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuwa na sheria itakayosimamia makundi haya na maeneo yanayowa husu ili kuondoa kabisa matatizo haya kwenye jamii yetu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imeweka utaratibu wa kuwa na Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi katika vijiji ambao unakusudia kuwa na utaratibu unaoleweka wa matumizi ya ardhi kwa ajili ya makundi mbalimbali wakiwemo wakulima, wafugaji, wawekezaji, makazi na huduma za jamii.

Kiini cha migogoro ya wakulima na wafugaji ni kuwepo kwa idadi kubwa ya mifugo ikilinganishwa na uwezo wa maeneo ya malisho pamoja na baadhi ya wakulima na wafugaji kutoheshimu utaratibu uliowekwa na Serikali wa matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, zipo sheria mbalimbali zilizowekwa na Serikali ili kulinda na kusimamia maslahi ya wakulima na wafugaji. Sheria hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Sheria ya Ardhi Sura 113 kifungu cha 175 kinachozuia mtu kuchunga mifugo kwenye eneo lisiloruhusiwa kwa mujibu wa sheria. Sheria ya Ardhi ya Vijiji Sura 114 kifungu cha 7(1)(e) (ii) kinatambua kuwepo kwa ardhi katika kijiji inayotumika kwa ajili ya malisho ya mifugo

ya wanakijiji au mifugo ya watu binafsi kwa makubaliano na wanakijiji au kimila;

(ii) Sheria Ndogo zinazotungwa na Halmashauri kwa lengo la kudhibiti na kusimamia ufugaji na kilimo katika maeneo yake;

(iii) Sheria ya Makosa inayozuia mtu kuharibu mali ya mtu mwingine au kuingia kijinai kwenye eneo la mtu mwingine kwa lengo la kutenda kosa; na

Mheshimiwa Spika, sheria nilizozitaja pamoja na sheria nyingine zinazoruhusu kilimo na ufugaji zinatosheleza kusimamia makundi ya wakulima na wafugaji. Changamoto kubwa tuliyonayo ni usimamizi mdogo wa sheria hizi pamoja na kukosekana kwa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi za Vijiji kwa baadhi ya maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Halmashauri zote nchini zikiwemo Serikali za Vijiji, kuhakikisha zinaandaa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi na kusimamia ipasavyo utekelezaji wa sheria zinazosimamia masuala ya kilimo na ufugaji. Aidha, wakati wa kuandaa mipango hii ushirikishwaji wa makundi mbalimbali wakiwemo wakulima na wafugaji ni muhimu ili kuleta maelewano. *(Makofi)*

**MHE. ABUU HAMOUD JUMAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa na maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa tatizo hili la wafugaji na wakulima ni tatizo la muda mrefu na tatizo

hili limekuwa kero kubwa katika maeneo yetu. Kwa sasa hivi ushahidi tunao tosha katika maeneo mengine inapelekea kupunguza amani katika nchi yetu.

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura au mikakati gani mizito ya kuhakikisha kwamba tatizo hili tunalimaliza kwa muda mfupi?

Jambo la pili, nilikuwa naomba kutoa ushauri tu kwa sababu suala hili linahusiana kwa karibuni na Wizara nne, Wizara ya Ardhi kwa maana ya Ardhi na pia Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na TAMISEMI. Sasa ningependeza Waheshimiwa Mawaziri hawa wakutane pamoja ili waweze kuweka mikakati ya kuona kwamba jambo hili tunaweza tukalimaliza. Kwa mfano leo hii hawa wafugaji wakati mwingine tumewatengea maeneo.

**SPIKA:** Mheshimiwa unataka kutoa hotuba au vipi?

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Swali?

**SPIKA:** Ehee!!!! Basi uliza swali lenyewe, Wizara hizi zitakubaliana kukutana, maana yake ndiyo hivyo. Endelea Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa.

**MHE. ABUU H. JUMAA**: Nafikiri swali langu limeeleweka Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Haya. Je, Wizara hizo ziko tayari kukutana mkamaliza hilo tatizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa

Spika, kwanza hili la pili analosema tunalifanya na wenzangu huku wapo wanasikia. Huwa tunakutana ni wazo zuri hilo na wala Mbunge hana haja ya kutumia nguvu kubwa. Ndio utaratibu wetu na kwa sababu usiporatibu haya mambo unaweza kukuta hawa wanazungumza hili, wale wanazungumza lile.

Masuala ya ardhi yote mambo ya *policy issues* mambo ya sera, *quality control* na kadhalika yanafanywa na Wizara ya Ardhi. Sisi ni mambo ya *Management* na *Administration* ndio tunafanya. Kwa hiyo, tunaiona mantiki na *logic* kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tunazingatia ushauri huu ambao unatolewa hapa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anaulizia suala hili la mpango gani wa dharura tulionao hapa. Hapa zunguka, panda, teremka, fanya lolote unalotaka kufanya hapa *the bottom line is* kama huna matumizi bora ya ardhi ambapo utasema hapa ni kwa ajili ya kilimo, hapa ni kwa ajili ya mifugo na hapa ni kwa ajili ya biashara ndogondogo, hapa ni kwa ajili ya makanisa na misikiti, hapa ni kwa ajili ya watoto kubembea *it will never work.* Haitafanya kazi hata siku moja.

Lazima tufike mahali tuheshimiane, kila mmoja ajue kwamba sisi tunamhitaji na yeye anatuhitaji. Ukifika mahali Halmashauri ikafika mahali kila mtu anajifanyia anavyotaka huyu anakwenda kwa mkulima, huyu anakwenda kwa mfugaji anakwenda kufanya kazi ile pale itakuwa ni vurugu. Historia imeonyesha kwamba katika mahali popote ambapo hapakuwa na utaratibu huo pamekuwa na *conflict.*

Mheshimiwa Spika, na anaposema hapa ni kweli kwamba nchi nzima tunajua kwamba kumekuwepo na mgogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Kwa hiyo, tunachosema hapa au tunachoaagiza kama Serikali Halmashauri zetu zote lazima zifike mahali kupitia vijiji na mitaa ziseme kwamba tumeweka mpango wa matumizi bora ya ardhi. Mpango wa dharura, mpango wa muda mrefu wote lazima ulenge hapo kwamba tukubaliane baada ya hapo tuna-*demarcate* mnaweka na *beacons. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba ipo changamoto kubwa tuliyonayo hapa. Halmashauri nyingi hazina uwezo wa kwenda kupima ardhi. Lakini tumesema tufike mahali tuwe hata na viashiria Maafisa wetu wa Mipango Miji wapite wawaambie wananchi hapa msijenge kwa sababu tunategemea barabara itapita hapa.

Hapa zitapita nguzo za umeme, hapa patapita mtaro wa maji. Unawaeleza hapa jamani sisi kama kijiji tumeamua eneo hili litumike kwa ajili ya mifugo, hapa patumike kwa ajili ya shughuli za mifugo, hapa patumike kwa ajili ya shughuli za kilimo.

Mkifika hapa mkishaelewana Serikali ziko pale hamtasikia matatizo hayo na tukifika mahali sisi sote tushirikiane. Siyo suala la mtu mmoja, siyo suala la Wizara moja ni sisi wote tushirikiane kwa sababu wote hawa ni watu wetu na tunawahitaji. (*Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa sababu kila mmoja anajua

kwamba ukiwa na mahindi mengi unatafuta ghala, tafuta soko. Ukiwa na ng'ombe wengi unatafuta malisho. Kwa kuwa Serikali ndiyo imehodhi mapori ambayo ndio chakula cha ng'ombe, imehodhi ranchi ambazo hazina ng'ombe. Kwa nini Serikali isiwe na ubunifu wa kuweza hata kuwatoza hawa wafugaji, lakini wapate malisho ya ng'ombe ambao tunawahitaji? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hapa natakiwa niwe mwangalifu kabisa. Hili jambo linalosemwa hapa ni jambo linaloingia kwenye mjadala mpana unaoangalia maslahi ya Taifa zima. Mimi nikikurupuka nikasema sawa, kesho watu wakaingia katika maeneo ya Hifadhi wakaanza kuchunga ng'ombe kule mimi hapa nitakuwa *head responsible* kwamba wewe ulituambia hivyo.

Ninachosema naiona *concern* ya Mbunge, naona kwamba kweli kuna tatizo hapa. Hili jambo si jambo la kusema hapa haraka *okay* kutoka leo Serikali inasema tunaruhusu wafugaji ingizeni mifugo maeneo ya hifadhi. Wizara inayoongoza kwa mapato ya Serikali ni Wizara ya Maliasili na Utalii. Inawezaje ikafanya mambo hayo ikafanya hayo yote kama sisi tutasema maeneo ya hifadhi haya tuache tu yaparamiwe.

Nasema hivi tunakaribisha mawazo ya Mheshimiwa John Cheyo. Serikali iko hapa inasikia ni sikivu, Serikali ya Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, inasikiliza. Tupo tayari kukaa na wakulima na wafugaji tukae nao tuzungumze tuelewane vizuri tupate majibu ya pamoja kwamba tumeafikiana

kwamba tufanye hivyo. Hayo ndiyo majibu ya Serikali. (*Makofi/Kicheko)*

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, imejengeka dhana kwamba wafugaji ndio wakorofi na ndio wanaosababisha athari yanapotokea mapigano. Lakini ukweli ni kwamba mara nyingi wafugaji ndio wanawakimbia wakulima. Mimi nimetoka Mkoa wa Shinyanga maeneo mengi yaliyokuwa ya mifugo hivi sasa ni ya kilimo na wafugaji sasa wametoka Shinyanga wako Tabora, wako Kigoma na kule wanakwenda kugombana na wakulima.

Nilitaka kuomba kusikia upande wa Serikali hii dhana ya kusema kwamba wafugaji na hasa ilivyojengeka hata kwenye swali hapa kwamba wafugaji ndio wanaowasumbua wakulima. Wakati wakulima ndio wanaopanua mashamba yao hivi itaendelea hadi lini ili wafugaji kweli nao waonekane kwamba ndio wanaochokozwa na kilimo kinachoongezeka? (*Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza hii *findings* zake ndio nazisikia hapa. Sikumbuki mahali popote tumewahi kusema kwamba Serikali inaonekana wachokozi ni hao kundi hili au kundi hili. Mimi sikumbuki.

Ninachojua ni kwamba tunayo makundi mbalimbali ambayo wakati mwingine yamekiuka utaratibu. Lakini mimi

sikumbuki mahali ambapo tumeiweka kama Serikali ambapo kundi la wafugaji ndilo tatizo hapa sijasikia. Ninachojua ni kwamba kuna mgongano ambao unajitokeza kati ya makundi ya aina mbalimbali.

Wako wengine wafanyabiashara ndogo ndogo, wengine ni wakulima, wengine ni wafugaji kama tunavyozungumza. Tunachosema hapa ni kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa.

Sasa kama Mheshimiwa Ezekiel Maige ana mahali popote anapofikiri kwamba kuna tatizo kwa upande wa hilo kundi analolisema sisi tuko tayari tukae tuzungumze wote kwa pamoja lakini sifahamu ndio nasikia sasa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, tumetumia muda mwingi sana kwa swali hili moja naomba tuendelee na swali linalofuata atauliza Mheshimiwa Ahmed Ally Salum.

Na. 99

**Tatizo la Nyumba za Walimu Solwa**

**MHE. AHMED A. SALUM** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua na kumaliza kabisa tatizo kubwa la upungufu wa nyumba za walimu lililopo katika shule zote za Sekondari na Msingi katika Jimbo la Solwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupitia Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES II) unaotekelezwa hadi mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM), Serikali ina mikakati mbalimbali ya kuboresha Elimu ya Msingi na Sekondari ili kuondokana na changamoto mbalimbali ikiwemo upungufu wa nyumba za walimu kama ifuatayo:-

(i) Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 na 2012/2013 Serikali imepeleka katika Halmashauri zote nchini shilingi bilioni 13.9 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu. Kati ya fedha hizi, shilingi milioni 800 (896,400,000) zilipelekwa katika Mkoa wa Shinyanga na shilingi milioni 93 zilipelekwa katika Jimbo la Solwa (Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga)

(ii) Kuendelea kujenga na kupanua miundombinu ya Shule za Sekondari ili ifikapo mwaka 2015 shule 528 zikamilishwe kuwa na miundombinu muhimu ikiwemo nyumba za walimu. Katika mwaka 2012/2013 zimetengwa jumla ya shilling bilioni 56.3 kwa ajili ya shule 264 ambapo Halmashauri zipo katika hatua ya kutangaza zabuni. Shule za sekondari Sumaye na Kituli zilizopo Jimbo la Solwa zitanufaika na mpango huu.

(iii) Kujenga na kukamilisha nyumba za walimu 1800 katika shule 900 zilizo maeneo ya vijijini ifikapo mwaka 2015.

Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa shule zilizo katika Jimbo la Solwa zitapewa kipaumbele.

(iv) Kuendelea kutoa fedha za ukarabati kwa Shule za Sekondari ambazo zinatumika pia kukarabati nyumba za walimu katika shule kongwe na chakavu. Jumla ya shilingi bilioni 7.8 zimekwishatolewa kati ya mwaka 2009 na 2012.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali imetenga shilingi bilioni 31.4 kupitia mipango ya Bajeti za Halmashauri nchini kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu. Shilingi milioni 257 zitatumika kujenga nyumba mpya za walimu katika Jimbo la Solwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya elimu nchini, ikiwemo upungufu wa nyumba za walimu kadiri fedha zinavyopatikana. Natoa wito kwa Halmashauri kuweka kipaumbele na kuendelea kutenga fedha katika mipango na Bajeti kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule. *(Makofi)*

**MHE. AHMED ALLY SALUM**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni mazuri lakini si ya kweli. Nikitoa mfano wa mwaka wa fedha 2012/2013, tulitengewa milioni 462 kwa maana ya nyumba za walimu 67, madarasa 31 na madawati 300. Lakini mpaka sasa hivi ninavyokwambia hizi hela hatujazipata zipo kwenye mtandao na ni fedha nyingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye nyumba za walimu za Sekondari *ceiling* ilikuwa *zero* na hata sasa hivi iko *zero.* Hii inawaumiza sana wananchi ambao kwa kweli kwenye Jimbo la Solwa tumejenga nyumba nyingi sana kufikia usawa wa lenta.

Mheshimiwa Spika, nakuomba atakapojibu Waziri hili swali na nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha ainuke aseme hizi fedha kwenye mtandao maana yake ni nini na lini tutazipata tukamilishe hizi ahadi zetu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**: Mheshimiwa Spika, mimi nimekuja na *file* hapa lote ninalo hapa na ma-*file* mengine haya yote tunayojibu tuna ma-*file* yamekaa hapa. Siyo kwamba nakuja hapa naibuka tu. Rafiki yangu Mheshimiwa Ahmed Ally Salum anasema si kweli lakini wakati huohuo anasema kwamba ukiziangalia katika mtandao zinaonekana kama zipo.

Sasa Mheshimiwa hela zetu hapa huwa haziji zote kwa mkupuo, unaziona zote zimeletwa kama zilivyongizwa kwenye Bajeti ambayo tumepitisha sisi wote hapa. Hela hizi zinakwenda kidogokidogo. Nataka niamini kwamba kwa vile yeye anatoka kwenye *centre* ya jambo lenyewe anaweza akawa anaufahamu mkubwa kuliko sisi kama Serikali.

Mimi nitakwenda kukaa naye na hizi takwimu tutazizungumza. Wakati mwingine tumekuwa na matukio tumeambiwa katika Halmashuri hela hazijafika lakini tunakwenda kuwaonyesha tunawaambia hela hizi ziko kwenye akaunti hii na hii. Ndiyo maana tumepunguza

akaunti za Halmashuri kutoka 32 tumezipunguza mpaka akaunti sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema ndugu yangu Mheshimiwa Ahmed nipo tayari kukaa naye ninazo takwimu hapa ili tukafuatilie wote kwa pamoja tujue kwamba tumekwama wapi. Sasa kama tumekwama kwa Waziri wa Fedha sasa Waziri wa Fedha, mimi hapa nawakilisha Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Lakini nipo tayari kukaa naye. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba anatoa wito kwa Halmashauri kutenga pesa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na kadhalika, lakini Halmashauri zinatofautiana. Swali langu. Hivi zile hela za *change* ya *radar* ambazo zilikuwa zimeanishwa kwenda kufanya kazi kwa ajili ya madarasa na madawati, vitabu na kadhalika. Mchakato wake hivi sasa ukoje?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**: Mheshimiwa Spika, hapa tunazungumzia majengo hapa.

Mimi ninavyokumbuka taarifa iliyoletwa hapa na Wizara ya Elimu wakati ule tulisema kwamba tunazungumza kuhusu vitabu vya kiada na ziada ndivyo vinavyoendelea na ndiyo mchakato ambao nafahamu kama unaendelea sasa hivi. Kwamba tumefikia hatua gani? Ni jambo ambalo tutamweleza tu Mbunge tumefikia hatua gani, lakini halikuelekezwa katika nyumba.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumekuwa na maswali na majibu marefu muda unatumika mwingi kwa swali moja. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, atauliza swali linalofuata.

Na. 100

**Kuwepo kwa Mamlaka Mbili za Maji Manispaa ya Shinyanga**

**MHE. RACHEL MASHISHANGA ROBERT** aliuliza:-

Serikali iliahidi kufuatilia la utata wa kuwepo kwa Mamlaka mbili za Maji Manispaa ya Shinyanga na Maji wa Kahama (SHUWASA na KASHWASA) ambayo hatima yake ni mtumiaji wa mwisho kupata mzigo mkubwa:-

(a) Je, Serikali imefikia wapi katika kufuatilia suala hilo?

(b) Je, kwanini Serikali isitoe ruzuku kwa Mamlaka moja ikiwa inataka kuendelea na Mamlaka mbili, ili mtumiaji wa mwisho apunguziwe mzigo wa kuendesha Mamlaka mbili?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa tarehe 30 Julai, 2012, Serikali iliahidi hapa Bungeni kuupitia mfumo

uliopo wa kuwa na Mamlaka mbili za Maji za Manispaa ya Shinyanga (SHUWASA) na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama - Shinyanga (KASHWASA) ili kubaini iwapo una mapungufu. Serikali imepitia na kujiridhisha kuwa muundo uliopo wa kuwa na mamlaka mbili unastahili kuendelezwa.

Mamlaka hizo zina majukumu tofauti yaani KASHWASA ina jukumu la kuzalisha maji kutoka kwenye chanzo, kuyasafirisha na kuyauza kwa jumla *(bulk water supply)* kwenye Mamlaka za SHUWASA na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Kahama (KUWASA) pamoja na vijiji vilivyo ndani ya eneo la kilomita 12 kila upande wa bomba kuu; na mamlaka za SHUWASA na KUWASA zina jukumu la kusambaza maji kwa wakazi wa Manispaa ya Shinyanga na mji wa Kahama.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwapungizia wananchi gharama, na kuiwezesha KASHWASA iendelee kutoa huduma kwa wananchi wa maeneo hayo, Serikali inaendelea kutoa ruzuku kwa kulipia sehemu ya gharama za uendeshaji na uwekezaji, kwa kuwa bei ya maji inayotozwa na KASHWASA haikidhi gharama za uendeshaji, ikiwemo ankara za umeme na ununuzi wa madawa ya kutibu maji pamoja na sehemu ya uwekezaji.

**MHE. RACHEL MASHISHANGA ROBERT**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri lakini nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza. Taarifa nilizonazo mimi ni kwamba hakuna ruzuku inayokwenda KASHWASA na kama inakwenda nilikuwa nataka nijue ni shilingi ngapi inakwenda kwa ajili ya KASHWASA?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa mamlaka mbili Serikali imeona hauna mapungufu. Lakini mimi nasema una mapungufu kwa sababu mpaka sasa hivi ninavyozungumza Mkurugenzi wa SHUWASA amesimamishwa kazi kwa sababu ya ubadhirifu wa pesa. Nilikuwa nataka kujua Serikali haioni kuna haja tena ya ku-review haya mamlaka mbili ili uone ufanisi wake kama ni mzuri au haufai kwa wananchi kwa sababu mtumiaji wa mwisho ndiye anayepata shida?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Spika, taarifa kwamba anazo taarifa kwamba hakuna fedha zinazopelekwa KASHWASA naomba baada ya kikao hiki nimthibitishie hizo takwimu ninazo na sisi tumekuwa tunatoa ruzuku na ndiyo maana bei ambayo wanalipa wananchi pale iko chini ikilinganishwa na hali halisi ya uwekezaji uliopo kwenye mamlaka hiyo ya KASHWASA.

Kwa hiyo, ruzuku inatolewa kwenye sehemu ya umeme na kwa sababu kuendesha umeme ni ghali sana na wakati mwingine mitambo huwa inafungwa kama ukifuatilia ni kwa sababu anadaiwa *bill* za umeme na inapotokea inabidi Wizara yetu iingilie kati na kupeleka fedha mapema.

Kwa sasa hivi kwa taarifa tuliyo nayo madeni makubwa ambayo tunadaiwa kwenye hizi Mamlaka za maji za miradi ya kitaifa ikiwemo hii ya KASHWASA, ikiwemo ya Makonde na mingine mingi ambayo madeni makubwa kwa sababu gharama za uendeshaji ni kubwa na hasa kwa upande wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kwamba muundo uliopo yeye anaamini hautoshelezi mahitaji na ana taarifa kwamba Mkurugenzi amesimamishwa kazi. Labda nitoe ufafanuzi kwamba yule Mkurugenzi hakusimamishwa na KASHWASA Mamlaka ya Maji ya Shinyanga na yale ni maamuzi ya Bodi.

Kwa hiyo, Mwenyekiti na Bodi yake baada ya kubaini kwamba huyu Mkurugenzi ana mapungufu ya ubadhirifu kama tulivyo na taarifa wamemsimamisha kazi na ni haki yao kufanya vile kwa sababu wamepewa mamlaka hayo na Waziri wa Maji.

Kwa hiyo, wamefanya kazi yao vizuri. Lakini hiyo ya kumsimamisha mtu kwa sababu ya ubadhirifu haina maana kwamba mfumo ule sasa una mapungufu. Nadhani ndiyo inafanya kazi vizuri kwa sababu ndiyo mgawanyo wa majukumu waliyo nayo pale.

Naomba nirudie kwamba jukumu la KASHWASA ni kusimamia na kuuza maji kwa jumla na ieleweke kwamba sasa hivi tunao mpango wa kupeleka maji Igunga Nzega na Tabora. Kwa hiyo, Mamlaka hii itakuwa na jukumu kubwa huwezi ukaipa tena jukumu la kufanya kazi ya usambazaji. Kazi ya usambazaji kwa wananchi itafanywa na Mamlaka za Maji za Miji husika kama ilivyo SHUWASA, KUWASA na miji mingine. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea majibu yalikuwa marefu kama semina. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika. Mheshimiwa Betty Machangu, atauliza swali linalofuatwa.

Na. 101

**Kuwezesha Skimu ya Umwagiliaji ya Lower Moshi Kufanya Kazi**

**MHE. BETTY E. MACHANGU** aliuza:-

Skimu ya Umwagiliaji ya *Lower* Moshi yenye ukubwa wa hekta 2,300 haifanyi kazi kufuatia ukosefu wa maji, licha ya kuwa utafiti wa *JICA* umeonyesha kuwa maji yangeweza kupitikana kutoka mto Kikuletwa; tatizo ni kwamba uongozi wa Bonde la Pangani unapopatikana mto huo wamekataa kuruhusu maji kutoka hivyo mradi huo kushindwa kuendelea.

(a) Je, Serikali haioni kuwa kutoruhusu maji hayo kutumika kunasababisha ukosefu wa chakula na kupotea kwa gharama za ujenzi wa skimu hiyo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani mbadala wa kuhakikisha skimu hiyo inafanya kazi kwa ufanisi ili kuongeza chakula kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Skimu ya *Lower Moshi* ilianza kujengwa mwaka 1984 na kukamilika mwaka 1987 kwa mkopo wa masharti nafuu toka Serikali ya Japan, ikiwa na eneo la ukubwa wa hekta 2,300. Hekta 1,100 zimejengewa miundombinu kwa ajili ya kilimo cha mpunga na hekta 1,200 zilizotengwa kwa mazao mengine yakiwemo mahindi ambazo hizo hazikujengewa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Maji Bonde la Pangani iliruhusu maji ya Mto Kikuletwa kutumika kwenye Skimu ya *Lower Moshi* kwa kiwango cha meta za ujazo 3.71 kwa sekunde kwa ajili ya eneo la hekta 2,300 kwa masharti kuwa matumizi hayo yasiathiri mahitaji ya maji kwa miundombinu ya wadau wengine katika mto huo.

Kutokana na umuhimu wa mradi huu, Serikali ya Tanzania mwaka 1995 iliomba msaada kwa Serikali ya Japan ambapo Shirika la *JICA* lilifanya upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi huo mwaka 1997/2098 na kupendekeza kuchepusha maji meta za ujazo 9 kwa sekunde wakati wa masika na meta za ujazo 5 kwa sekunde wakati wa kiangazi kutoka Mto Kikuletwa ili kuendeleza na kupanua skimu hiyo na kufikia hekta 4,700 kwa gharama ya shilingi bilioni 61.7.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na kuendelea kupungua kwa kiwango cha maji na eneo ambalo lingeendelezwa, vigezo vya kiuchumi viliangaliwa upya na kuonekana ni vya chini hali iliyosababisha Serikali ya Japan kutoafiki kutekeleza mradi huo.

Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali pamoja na kufanya tathmini mpya ya mradi huo ili kuendeleza mradi huo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mipango mibadala ya kuhakikisha skimu hiyo inafanya kazi kama ilivyokusudiwa. Mipango hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuboresha miundombu ya skimu za Mandaka, Mnono na Kaloleni zenye jumla ya hekta 614 ili ziongeze upatikanaji wa maji ndani ya skimu ya *Lower Moshi.*

(ii) Kuchimba visima virefu (*bore holes*) vinane (8) katika vijiji vya Oria na Chekereni ambapo jumla ya hekta 100 zitamwagiliwa.

(iii) Kujenga mabwawa ya kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji na kujenga miundombinu ya Mto Kikuletwa kwa kuzingatia kiwango cha maji kilichokubalika cha meta za ujazo 3.71 kwa sekunde. *(Makofi)*

**MHE. BETTY E. MACHANGU**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri naomba niulize maswali ya nyongeza mawawili.

Mheshimiwa Spika, mapato ya ndani ya Halmashauri za Wilaya katika Mikoa ya Kaskazini na kwingineko yanatokana na mazao ya kilimo na mifugo. Idara ya Kilimo katika Halmashauri ya Wilaya inapokosa fedha za kutosha inashindwa kugharamia huduma za ughani, maonyesho ya kilimo kama nane nane, matunzo ya vyombo vya Serikali vile ambavyo vinatumia Maafisa Ugani.

Je, ni kwanini asilimia fulani ya mapato ya Halmashauri za Wilaya hasa yale yanayotokana na mazao na mifugo husika zikabaki katika Idara ya Kilimo ili kilimo ambacho ni uti wa mgongo kiweze kusimamiwa vizuri. *(Makofi)*

Swali la pili, ni Maofisa Ugani nchini wanafanya kazi zao za ugani vizuri pale ambapo wanakuwa na vyombo vya usafiri. Lakini uzoefu unaonyesha kwamba vyombo hivi hata hivyo havisimamiwi vizuri na pengine ni kwa sababu hivi vyombo sio vyao kwa hiyo hawana uchungu navyo.

Je, ni lini Serikali itawakopesha maafisa ugani vyombo hivi ili kuwepo na ufanishi katika kazi zao lakini pia na vyombo hivi viweze kutunzika?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, hili la mapato yanayotokana na kilimo kubaki ndani ya Halmashauri mimi nadhani hili ni mfumo uliopo sasa hivi TAMISEMI na hayawezi kuwa mapato ya kilimo kwa sababu Halmashauri zingine zinategemea mapato kutoka vyanzo vingine.

Sasa vyote vikibaki Halmashauri; mimi nadhani huu ni utaratibu ambao Wizara ya Fedha, TAMISEMI, Serikali Kuu na Serikali za Mitaa zimejipangia ili kuhakikisha kwamba mapato haya ya Halmashauri yanagawika kwa mfumo ambao una manufaa kwa Serikali yote kwa maana ya ngazi zote za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani hili ni jambo ambalo linaweza kuangaliwa baina ya TAMISEMI, Wizara ya Fedha na wadau wote ili tuangalie namna ambavyo linaweza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, hili la vyombo vya usafiri naomba niseme hili ni la kila Halmashauri yenyewe inaangalia namna ya kuwapa motisha wagani wao ili waweze kufika kwenye maeneo na kutekeleza kazi zao vizuri.

Kwa hiyo, naomba kuhamasisha tu kwamba Halmashauri zote zijitahidi kadri itakavyowezekana kuweza kutambua kwamba hawa wagani na watumishi wengine ambao wanafanya kazi kwa wananchi moja kwa moja wana manufaa makubwa katika misingi ya kiuchumi na kijamii ya nchi hii. Kwa hiyo, naomba wawaangalie namna ya kuwapatia motisha zaidi wa kufanya kazi zao vizuri zaidi.

**MHE. JITU V. SONI**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza. Je, ni lini Serikali itatatua tatizo kama hili la Lower Moshi kukosa maji na kwa kuwa Serikali ni moja Wizara zote zinazohusika iwe ya Maji, Kilimo na Wizara ya Mazingira wakae pamoja na kubuni namna ya kuhakikisha kwamba wanaweka mipango pamoja ili ukosefu wa maji isitokee na ni kwa Tanzania nzima na isiwe kwenye eneo moja tu la *Lower* Moshi tu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mheshimiwa Jitu Soni kwa sababu ametambua kwamba tatizo hili sio tatizo la mtu mmoja.

Ni tatizo la maji ni tatizo la Mazingira tatizo la TAMISEMI na kama walivyokuwa anazungumza Mheshimiwa Mwanri wakati wa kujibu hapa dakika zilizopita na kama nilivyozungumza juzi wakati najibu swali la Maliasili na Utalii la Bonde la Usangu ni lazima sisi Watanzania wote tujue kwamba kadiri tunavyoendelea kuharibu vyanzo vya maji,

tunavyoharibu ardhi hizi *wet lands* na kadhalika. Tutafika sehemu ambayo vyanzo vya maji vitateketea tu. Tutakuwa hatuna hata maji ya skimu za *irrigation*.

Kwa hiyo, mimi nadhani hili ni tatizo ambalo Serikali tumejipanga na nadhani katika kulikabili itabidi tulianzie humuhumu Bungeni ili sisi wenyewe tupate ufahamu wa majukumu yetu na wajibu wetu wa pamoja katika kukabiliana na tatizo hili leo ili tusianze kuulizana maswali miaka kumi na tano wakati tutakapokuwa tumekosa maji kabisa katika vyanzo vyote vya *irrigation. (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nimrod Mkono, kwanza tunafurahi umerudi na afya njema. Swali la nyongeza.

**MHE. NIMROD E. MKONO**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri, tatizo la *Lower Ruvu* linafanana sana na tatizo nililonalo Jimboni kwangu kule Bugwema. Bugwema lina eneo ambalo ni la Kilimo zuri sana.

Lilihodhiwa na Serikali kwa muda mrefu sana lakini wananchi wa Bugwema hawana mahali pa kulima na hawana mahali pa kuchungia mifugo yao. Wamekuwa wanalia kwa muda mrefu sana. Wakati wa Uchaguzi Mkuu Rais alitembelea na aliahidi atalitatua tatizo la Bugwema ili wananchi waweze kushiriki kikamilifu kupunguza hali ya waliyonayo pale Bugwema.

Je, ni lini kero ya Bugwema itamalizika ili wananchi wa Bugwema waweze kulima na kufuga kwenye maeneo hayo ambayo yako wazi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali halikuwa kwa *Lower Ruvu,* ilikuwa *Lower Moshi.* Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba niseme tu kuwa katika hizi *Schemes* za umwagiliaji maji kwa mwaka huu kuna taarifa ambayo tuna *Schemes* 149 ambazo ninayo hapa, kuhusu hatua za utekelezaji na mipango na namna itakavyotekelezwa. Kwa hiyo, inakuwa ngumu kidogo kuweza kutoa hali halisi ya utekelezaji kwa miradi yote.

Mheshimiwa Spika, ninatambua kuwa kulikuwa na ahadi ya Mheshimiwa Rais kwamba kwa ule mradi wa Bugwema pale tutaangalia namna ambavyo wananchi wanaweza kupata maslahi zaidi.

Lakini pia Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maagizo kuwa tufanye tathmini ya hali halisi ya kila mradi ulipofikia ili kwa sasa hivi tujifunge kwenye ile miradi ambayo inayoweza kukamilika haraka iwezekanavyo ili ipate maslahi.

Mheshimiwa Spika, Badala ya kuwa tunafanyia kazi miradi mingi kwa wakati mmoja na hakuna inayokamilika kwa hiyo ninamwomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kuwa tutakaa pamoja na kufanya tathmini ya hali ya mradi wa Bugwema. Kwa sasa hivi na hatua za kuukamilisha na pia hatua gani ambazo zinatakiwa kuchukuliwa kwa haraka.

Na. 102

**Bajeti ya Ulinzi na Usalama Kusomwa Hadharani**

**MHE. MARTHA M. MLATA** aliuliza:-

(a)Je, ni kwa nini Bajeti za Wizara zinazohusu Ulinzi na Usalama zinasomwa Hadharani?

(b)Je, kwa nini Bajeti za Wizara hizo hazipewi kipaumbele?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifutavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 137(1) na (2), Bunge ndicho chombo chenye mamlaka pekee ya kuidhinisha matumizi ya fedha za Umma na kupitisha Makadirio na Matumizi ya fedha kila mwaka.

Kwa kuwa, Bajeti ya shughuli za Ulinzi na Usalama ni sehemu ya matumizi ya Umma ambayo hutumia fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ni lazima zipitie mkondo huu wa Kisheria.

Ingawa Bunge hufanya shughuli zake kwa uwazi lakini mara zote limekuwa likitumia busara wakati linapopitia Bajeti za Wizara zinazohusu shughuli za Ulinzi na Usalama. Wakati wa kujadili masuala nyeti ya Ulinzi na Usalama Bunge haliyaelezi masuala hayo hayo kwa undani ili kudhibiti siri zinazohusu mambo ya Ulinzi.

(b) Mheshimiwa Spika, mara zote Serikali imekuwa ikifanya jitihada za dhati kuongeza rasilimali na kutoa kipaumbele kwa Bajeti za Wizara zinazohusu Ulinzi na Usalama. Hata hivyo, ninakiri kuwa mahitaji ya vyombo vya Ulinzi na Usalama ni makubwa. Kwa hiyo, inakuwa vigumu kwa Serikali kuyatekeleza yote kwa mara moja kutokana na ufinyu wa mapato ya Serikali.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi wa nchi pamoja na Usalama wa raia na mali zao ni muhimu sana kuliko kutumia gharama yoyote ile. Lakini Wizara imekuwa ikija na Bajeti ndogo ambayo haikidhi mahitaji ya Wizara hizi pamoja na kwamba wanawekwa hadharani.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye Katiba Wizara zote hizi za Ulinzi pamoja na Usalama *Section* ya 147 na 148 inaonekana kuwa haitakuwa vizuri kuweka waziwazi kuwa shughuli zake au ziko pale kwa nini.

Mheshimiwa Spika, huenda ndiyo inayopelekea kutokuweka kipaumbele. Je, Waziri yuko tayari kwenda kujifunza katika nchi ambazo zinatoa kipaumbele kwenye

Wizara hizi. Mfano China, Marekani pamoja na India ili kuleta kipaumbele ndani ya Bunge hili kwa Bajeti inayoweza kutosheleza Wizara hizi.

Swali la pili, amesema kuwa ni kweli wamekuwa wakijaribu kuongezea rasilimali kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ambayo yanahusu Wizara hizi, katika Mkoa wa Singida askari wamekuwa wakiishi katika mazingira magumu sana, wakifanya kazi katika mazingira magumu sana hata ofisi ya *RPC* ilikuwa ni ofisi ya kituo cha mwanzo.

Mpaka sasa hivi karne hii tunavyoongea bado hali ni ile ile, nyumba zile ni kama stoo tu ambapo askari wetu wanaishi. Je, Waziri atanieleza nini ili Watanzania na watu wa Mkoa wa Singida waweze kujua kuwa ni lini nyumba zile na hali za askari wa Mkoa wa Singida ukianzia ofisi ya *RPC* zitapewa fedha za kutosha tuwaondoe katika mazingira yale. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Ulinzi ni jambo muhimu na bila ya kuwa na Ulinzi imara mambo mengine yote yanaweza yasifanyike inavyotakiwa. Hata hivyo tukumbuke kuwa nchi yetu bado ni nchi ambayo uchumi wake haujatosheleza kuyafikia mahitaji makubwa ya vyombo vya ulinzi kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, jitihada za Serikali zinaonekana na lazima tukiri kuwa bado yako matatizo lakini Serikali haipuuzi kutoa fedha za kutosha ili kuhakikisha kuwa vyombo vya Ulinzi na Usalama vinafanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu nyumba za askari na *RPC* hili ni tatizo ambalo ninalifahamu na Singida ni mfano tu lakini nchi nzima ina matatizo yanayofanana, Serikali inafahamu hili na jitihada nyingi zinaendelea kuchukuliwa kupitia Bajeti na nje ya Bajeti ili kuhakikisha kuwa askari kwa hatua wanapata makazi bora na wao kujua kuwa wanathaminiwa ipasavyo. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, kutunza siri za jeshi ni suala muhimu kwa Usalama wa Nchi na hasa masuala yanayohusu mikakati, mifumo, mipango, zana na mambo mengine.

Ninashukuru kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ametambua umuhimu wa uwazi katika masula yanayohusu Bajeti, ningependa Mheshimiwa Waziri ajibu tu kuwa ukiondoa siri zingine za kijeshi ambazo ni muhimu kufichwa.

Ni kwa nini Serikali imekuwa na kawaida ya kuficha Mapato, Matumizi na Ufasadi unaohusisha biashara zinazofanywa na makampuni ya Jeshi kama MEREMETA na mengineyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa umuhimu wa uwazi katika mambo yake yote na masuala yaliyotajwa ya kibishara ya Jeshi la Kujenga Taifa yako wazi kama yalivyo mengine na hesabu zao pia ziko wazi zinaweza kukaguliwa na ninakumbuka hivi karibuni na hata kesi zinazowahusu askari wa Jeshi la Kujenga Taifa ambao walifanya vitendo ambavyo pengine havikuonekana kuwa ni sahihi.

Kwa hiyo, hakuna tatizo la usiri kwenye hilo, usiri upo katika ununuzi wa zana na vifaa.

Na. 103

**Malipo kwa Wasimamizi wa Sensa ya Watu na Makazi**

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Sensa ya watu na Mkazi ni zoezi muhimu sana kwa maendeleo ya nchi, Sensa ya mwaka 2012 imeleta malalamiko mengi sana hasa Bukoba Vijijini kutokana na wahusikakutolipwa stahili zao:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu, kwa niaba ya Waziri wa Fedha ninapenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kwa ujumla kwa ushiriki wao katika kufanikisha Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, zoezi la Sensa ya Watu na Makazi liliwashirikisha watu wa kada mbali mbali kwa kila ngazi au Mamlaka ya kiutawala. Kwenye ngazi ya Kata, Vijiji na Mitaa viongozi ambao walishiriki kwenye Sensa ni Watendaji wa Kata, Vijiji na Mitaa. Makarani na wasimamizi wa Sensa wao walishiriki katika kuhesabu watu katika kaya na maeneo maalum kama vile wananchi waliokuwa wamelala mahotelini, wasafiri na watu wanaoishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia makundi niliyotaja hapo juu Serikali inapenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kuwa kwa upande wa Makarani na Wasimamizi tayari wamelipwa stahili zao zote kama ambavyo ilikuwa imebainishwa kwenye mikataba na hakuna malalamiko upande huo.

Kwa upande wa kundi la Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa walistahili kulipwa shilingi 10,000/= kwa siku kwa muda wa siku saba. Hivyo kila kiongozi alistahili kulipwa shilingi 70,000/=. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti na vilevile kutokana na kuongezeka kwa kazi kutokana na changamoto zilizojitokeza, viongozi hawa katika Wilaya nyingi ikiwemo Bukoba Vijijjini walilipwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa tayari uchambuzi na uhakiki wa madai ya shilingi bilioni 4,292,501,555 umefanyika na kuwasilishwa Serikalini kwa hatua za malipo. Malipo haya yatafanyika mapema kuanzia sasa. Hivyo basi ninawaomba Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa ikiwemo ya Bukoba Vijijini kuvuta subira wakati Serikali inashughulikia malipo hayo. *(Makofi)*

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa zoezi la Sensa katika Tanzania hufanyika kila baada ya miaka 10. Kwa hiyo ni kwamba Serikali walijua, walipanga mipango na Bajeti. Je, ni kitu gani kilisababisha hawa viongozi wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa, wasilipwe wakati huo wa Sensa?

La pili, katika Mkoa wa Kagera katika Wilaya za Kyerwa, Karagwe, Bukoba Vijijini na kadhalika Wenyeviti wa Vitongoji, Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vijiji wengine hawakulipwa kabisa na wengine walilipwa kati ya shilingi 1,500/=, wengine 1800/= kwa siku zote walizofanya kazi.

Kwa kutambua umuhimu wa viongozi hawa kwa sababu wao ndiyo wako karibu na wananchi na ukizingatia zoezi la Sensa limekwisha toka mwaka jana 2012 mwezi wa nane. Tunamwomba Naibu Waziri wa Fedha atamke sasa hawa viongozi yaani Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji na Wenyeviti Mitaa watalipwa lini atamke kabisa kuwa ni siku gani watakuwa wamelipwa hiyo stahili yao ya 70,000/=?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, Kwanza kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kulikuwa kuna changamoto ambazo hatukuzitegemea, kuna watu kutokana na sababu mbalimbali walitishika kutoa taarifa na wengine hawakujitokeza, ilibidi tutumie Wenyeviti wa Vijiji kwa ajili ya kwenda ku- *identify* watu wale.

Kwa hiyo, hilo siyo suala ambalo tulikuwa tumeli-*take in to consideration* kwa sababu hatukutegemea kuwa hilo suala linaweza likatokea. Kwa hiyo, kwasababu haikuwa kwenye Bajeti Wenyeviti wa Vijiji imebidi tuwapeleke pale tumewalipa shilingi 2500/= kwa sababu ndiyo kitu ambacho tulitegemea zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini *scope* ya watu ilivyokuwa na changamoto nyingi zilivyojitokeza ikawa tumeona kuwa kulikuwa na tofauti na ilikuwa walistahili kulipwa shilingi

10,000/=. Kwa hiyo, hiyo ndiyo sababu Bajeti yao haikuwamo kwasababu *we never expected* kuwa kungeweza kutokea changamoto ambazo wao sasa ndiyo ilibidi watusaidie kwa ajili ya kuzitatua.

Suala la pili la kuwa watalipwa lini nimesema kuwa kwa sababu 4.2 ilikuwa haipo katika Bajeti ya mwaka huu kwa hiyo ninachokwambia hapa ni kwamba tutalipa kabla ya mwaka huu wa Fedha kumalizika. S*imply* kwa sababu tayari tumeshafanya tathmini ya Mikoa yote, Wilaya zote ambako kulikuwa kuna mapungufu hayo na kwa sababu fedha yenyewe haikuwa *incorporated* katika Bajeti lakini tunajitahidi kuzitafuta na tutalipa *within this financial year.*

Na. 104

**Uchakavu wa Chuo cha Ualimu Kitangali**

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA** aliuliza:-

Chuo cha Ualimu Kitangali ni miongoni mwa vyuo kongwe kinachotegemewa sana nchini, lakini majengo yake pamoja na miundombinu yake imechoka sana na kupoteza hadhi yake kwa ujumla.

Je, Serikali imetenga kiasi gani cha fedha za kukarabati majengo ya Chuo hicho pamoja na miundombinu yake ili kukirudisha kwenye hadhi yake ya awali?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Mbunge kuwa majengo na miundombinu mingine ya Chuo cha Ualimu Kitangali ni chakavu. Kwa kutambua hilo mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kupitia kitengo cha ukarababti wa majengo ilikarabati mifereji ya maji ya mvua, kujenga vizuizi vya maji ya mvua na kujenga jengo la choo chenye matundu manane (8).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara yangu inatarajia kupata fedha kiasi cha shilingi bilioni 6 kutoka idara ya Serikali ya Uingereza ya Maendeleo ya Kimataifa *(UK- Department for International Development (DFID)* ambazo zitatumika kukarabati majengo mapya katika vyuo saba vya ualimu, Chuo cha Ualimu Kitangali kikiwa ni kimojawapo.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kitakachotumika katika ukarabati wa majengo pamoja na miundombinu mingine ya Chuo cha Ualimu Kitangali, kitajulikana mara tu baada ta tathmini inayofanywa na wataalam wa Wizara yangu, kitengo cha ukarabati kukamilika. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri yenye matumaini ninamshukuru sana Waziri na niaomba Mwenyezi Mungu hizo milioni 6 zipatikane ili chuo hicho kikarabatiwe. Lakini nina swali moja tu la nyongeza, moja tu.

Mheshimiwa Spika, miundombinu itajengwa lakini chuo hicho kina tatizo kubwa la gari. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu tatizo hilo kwa sababu ni miaka minne sasa hivi hakuna gari chuoni hapo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa yeye kushukuru Serikali kwa namna ilivyojipanga kukarabati vyuo saba(7) na chuo cha Kitangali kikiwa kimoja wapo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la gari takribani karibia vyuo vingi sasa hivi vingine magari yapo na vingine magari ni ya siku nyingi yameharibika. Lakini kwa sababu Serikali imeshaanza kufanya juhudi za kutafuta fedha tuliona kwanza tuanze na ukarabati wa miundombinu na maji na mambo mengine yatafuata, kwa kutumia Bajeti yetu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tuombe Mungu kwa mwaka wa fedha ujao tuweze kuangalia suala la magari katika vyuo vyetu vya ualimu. *(Makofi)*

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona kwa kuwa chuo cha Ualimu cha Bustani tatizo lake linafanana sana na chuo cha ualimu Kitangali pamoja na jina la Bustani hakuna uhusiano wowote kutokana na uchakavu wa yale majengo.

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu kukarabati majengo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema ni kwamba tunavyo vyuo 35 vya Serikali, vyuo vya ualimu cheti pamoja na diploma lakini kwa *plan* na fedha ambazo tumepata hizi bilioni 6 tayari tumeshaviweka vyuo kutokana na uchakavu wake, katika vyuo 35 tumesema kuwa tutaanza na vyuo saba kwanza baada ya kumaliza hapo tutaendelea kuomba fedha na kuandika maandiko mbalimbali kuomba kwa Wahisani mbalimbali ili tuweze kuvikarabati vyuo vyote.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa vyuo hivi ni vya zamani pamoja na hicho chuo ulichokitaja lakini tunakwend awamu kwa awamu kadiri fedha inavyopatikana. *(Makofi)*

Na.105

**Wananchi wa Zanzibar Kumiliki Silaha**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Wananchi wa Zanzibar hawaruhusiwi kumiliki silaha ambazo zingeweza kuwasaidia kujilinda na matukio ya ujambazi ambayo yamezidi kuongezeka sana:-

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zinazosababisha Wazanzibari wasiweze kumiliki silaha hadi leo?

(b) Je, kwa nini Serikali isiangalie raia walio wema pamoja na Viongozi ili wapewe fursa ya kumiliki silaha ili kujilinda?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Zanzibar (*The Fire Arms Decree Cap. 165*), kifungu cha 4, 5 na 6 na kwa kuzingatia hali ya kijiografia ya Visiwa hivyo, Wananchi hawaruhusiwi kumiliki silaha za moto isipokuwa Taasisi za Vyombo vya Dola pekee. Jambo hili limechangia kiasi kikubwa kuwepo kwa matukio machache ya ujambazi wa kutumia silaha.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea maoni ya Mheshimiwa Mbunge juu ya kuangalia uwezekano wa kuruhusu raia wema kumiliki silaha za kujilinda wao na mali zao. Hata hivyo, kwa kuwa jambo hili ni la kisheria, Serikali italifanyia kazi kwa kuzingatia hali ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, kuwaelimisha Wananchi kuhifadhi mali zao hususan fedha zao katika Vyombo vya Fedha (Benki), pamoja na kutoa taarifa kwa watu wanaowatilia mashaka ya uhalifu kwa Jeshi la Polisi na Vyombo vingine vya Usalama, kwa lengo la kupunguza matukio makubwa ya kihalifu.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Zanzibar imefikia watu kuuawa hata nyakati za asubuhi mnamo saa nne; kwa mfano, pale Mwanakwerekwe na matukio yaliyotokea Mwera na Uzini; je, wahusika walichukuliwa hatua gani kutokana na matukio hayo?

(ii) Kwa kuwa Wazanzibari hawahusiki kumiliki silaha; na kwa kuwa matukio yanajitokeza; je, kwa dhana ya Serikali wahusika wa matukio haya wanatokea wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwenye matukio ya awali aliyoyasema, hatua za upelelezi zimefanywa na watuhumiwa wanaendelea kufanyiwa hatua za kupelekwa Mahakamani kwa matukio aliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, kwa vile Wazanzibari hawajaruhusiwa kumiliki silaha ni nani anafanya ujambazi Zanzibar? Kwanza, naomba kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, ujambazi hauna mipaka, kuna ujambazi wa kimataifa, kuna ujambazi wa kimajimbo. Hata hivyo, kwa sababu mara nyingi silaha ambazo zinatumika kwenye matukio zinakuwa hazimilikiwi kihalali, kwa hiyo, matukio yanayotokea na uzoefu unavyoonesha mpaka sasa ni kwamba, katika matukio ambayo tuna rekodi nayo, Wazanzibari wanahusika ingawa mara nyingi silaha zinatoka upande wa pili wa Muungano. Kwa hiyo, Wazanzibari na wenzao wa Tanzania Bara, wanashirikiana mara nyingi katika kufanya matukio haya ya ujambazi Zanzibar na kama hili la kuwa na uhalali wa kumiliki ingekuwa dawa, basi namwomba mara nyingi Mbunge awasilishe hoja hii kwenye Baraza la Wawakilishi ili Sheria

ibadilishwe na Wazanzibari wapate haki kama ni haki kweli. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Naomba tuendelee na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Cecilia Paresso atauliza swali linalofuata. Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, naomba ukae chini kwa sababu nimemwita Mheshimiwa Paresso.

Na. 106

**Mgogoro Kati ya Wakazi na Wamiliki wa Mashamba Karatu**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Katika Wilaya ya Karatu hususan Kata za Daa, Oldeani na Ganako ambazo sehemu ya ardhi yake inamilikiwa na Wazungu kwa Hati Miliki *(Title Deed)* za muda mrefu toka enzi za Ukoloni; na inaonekana sasa kuna migogoro mikubwa ya ardhi kati ya Wakazi na Wananchi hao:-

(a) Je, ni mashamba mangapi ambayo Hati zake zimekwisha muda wake?

(b) Je, ni mashamba mangapi ambayo matumizi yake yamebadilishwa na kwa utaratibu upi?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la

Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Karatu ina mashamba makubwa 32 yanayomilikiwa na wawekezaji mbalimbali yakiwemo manne yanayomilikiwa na Madhehebu ya Dini. Kuhusu migogoro ya ardhi, Serikali inatambua kuwepo kwa migogoro baina ya Wananchi na baadhi ya Wawekezaji wa mashamba yaliyopo Wilaya ya Karatu. Mashamba yaliyopo katika Kata za Daa ni *Tembotembo Estate* pamoja na *Acacia Hill Estate*. Shamba la Tembotembo lina ukubwa wa ekari 1,107 na limesajiliwa kwa Hati Na. 4468 kwa muda wa miaka 99 kuanzia mwaka 1948. Mmiliki wa Shamba hilo ni Bwana Christian Leons.

Mheshimwia Spika, Serikali ilitwaa na kuhifadhi sehemu ya Shamba hilo lenye ukubwa wa ekari hamsini kuwa uoto wa asili kwa sababu ya kuwa na miinuko mikali na makorongo hivyo kutofaa kwa matumizi ya kilimo. Eneo hilo kwa sasa linakaliwa na zaidi ya Kaya 15 walioingia na kuanzisha shughuli za kilimo. Aidha, mgogoro uliopo ni baina ya Mwekezaji ambaye alifungua kesi dhidi ya Wananchi katika Mahakama ya Wilaya ya Karatu kwa lengo la kuwaondoa; shauri hilo bado linaendelea.

Mheshimiwa Spika, Shamba la *Acacia Hill Estate*, lenye ekari 1556, linamilikiwa na *Christian Leons* aliyemilikishwa mwaka 1948 kwa muda wa miaka 99 kwa Hati Na. 3742. Mgogoro wa Shamba hili ulitokana na Mwekezaji wa Shamba hilo kufunga barabara inayounganisha Kijiji cha Makhoromba na Makao Makuu ya Kata ya Daa kupitia katikati ya Shamba. Uongozi wa Serikali ya Wilaya ya Karatu pamoja na Uongozi wa Kijiji na Kata chini ya Uongozi wa

Mkuu wa Wilaya, walifanya mazungumzo na Mwekezaji huyo ili kupata ufumbuzi wa mgogoro huo. Katika kikao kilichofanyika mwezi Disemba 2012, Mwekezaji alipendekeza kuwa barabara ihamishwe kutoka katikati ya Shamba na kurudi chini ya Shamba. Aliiomba Serikali ifanye tathmini ya kutengeneza barabara hiyo aliyoipendekeza ili yeye agharamie matengenezo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ombi hilo, Wahandisi wa Wilaya, walikabidhiwa jukumu la kutathmini kazi hiyo ili kujua gharama za matengenezo ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, baada ya kikao hicho, hivi sasa kuna maelewano baina ya Wananchi na Mwekezaji. Tunayo matumaini kuwa, matengenezo ya barabara hiyo yatakapokamilika, amani ya kudumu itapatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu tulizonazo, hadi kufikia Mwezi Januari 2013, hakuna mashamba ambayo Hati zake zimekwisha muda katika Kata za Daa, Oldeani na Ganako.

Mheshimiwa Spika, (b) mashamba yaliyobadilishwa matumizi kinyume na masharti ya miliki ni matano, ambayo kwanza, ni *Tembotembo Estate Oldeani,* ambalo lilipangwa kwa matumizi ya kilimo na ufugaji, kwa sasa Hoteli ya Kitalii imejengwa kinyume na matumizi yaliyopo kwenye Hati. Pili, Shamba la *New Brandon Oldeani* ambalo imejengwa nyumba ya kulaza wageni wa kitalii kinyume na matumizi yaliyopo kwenye Hati ambayo ni kilimo na ufugaji. Tatu, ni Shamba la *Kiran Coffee Estate* ambapo kwa sasa imejengwa Kambi ya Watalii *(Camp Site)*, inayojulikana kwa

jina la *Crater Forest Tented Lodge Ltd.* na Kituo cha Watoto Yatima kinachojulikana kwa jina la *Rift Valley Children Fund* kinyume na matumizi yaliyopo kwenye Hati ambayo ni Kilimo. Nne ni Shamba la *Ngorongoro Farm House Oldean*, Shamba hili lilipangwa kwa matumizi ya kilimo na ufugaji, kwa sasa imejengwa Hoteli ya Kitalii na nyumba ya kulaza wageni kwa jina la *Ngorongoro Farm House*. Mwisho ni Shamba la *Msituni Estate Oldean* ambalo lilipangwa kwa matumizi ya kilimo na sasa imejengwa Hoteli ya Kitalii maarufu kwa jina la *Neptune.*

Mheshimiwa Spika, kufuatia wamiliki wa mashamba hayo kukiuka masharti ya umiliki, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Karatu, imewaandikia wamiliki wa mashamba hayo kuwataka waondoe maendelezo yaliyofanyika kinyume cha sheria. Iwapo watashindwa kufanya hivyo, hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuwafutia umiliki zitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, nawaagiza Wakurugenzi wote wa Halmashauri za Wilaya nchini, wafanye zoezi la ukaguzi wa matumizi ya ardhi kwenye viwanja na mashamba yanayomilikiwa kisheria na kuchukua hatua kwa wamiliki waliokiuka masharti ya umiliki. Hatua hizo ni pamoja na kupendekeza kufutwa kwa umiliki wao na ardhi husika kutwaliwa na Serikali ili iendelezwe na wawekezaji wengine wenye nia thabiti ya kuchangia maendeleo ya uchumi wetu. *(Makofi)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Serikali inakiri kwamba kuna wamiliki wamebadilisha matumizi ya mashamba hayo na kwa kufanya hivyo ni kinyume cha sheria. Je, ni lini Serikali itatwaa umiliki wa mashamba hayo na kuwagawia Wananchi?

(ii) Pili, kwa kuwa Serikali inatambua mgogoro wa ardhi kwa ujumla uliopo Wilayani Karatu; na kwa kuwa kuna malalamiko ya Wananchi hasa Wajasiriamali Wilayani Karatu juu ya utata wa umiliki wa baadhi ya maeneo, mfano maeneo ya Magereza. Je, Serikali ipo tayari sasa kuchunguza utata wa umiliki huo na ikiwezekana kuwagawia Wajasiriamali hao?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa hili la ni lini Serikali itatwaa mashamba ambayo wamiliki wake wamekiuka masharti ya matumizi ya ardhi na kuwagawia Wananchi, jibu lake ni kwamba; kwanza, watu hawa walimilikishwa mashamba haya kwa mujibu wa sheria za nchi. Kwa sababu hiyo, kabla ya kuchukua hatua yoyote ni lazima tufanye uchunguzi kujua ni kwa namna gani mabadiliko haya yamefanyika. Taratibu za kubadilisha matumizi ya ardhi ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, mmiliki wa ardhi husika anapaswa kuwasilisha maombi kwa *Planning Authority,* Mamlaka Inayopanga na kugawa ardhi, katika hali hii ni Halmashauri ya Wilaya ya Karatu. Baada ya Halmashauri kupokea maombi yale. itayatafakari kupitia vikao stahiki na kuwasilisha mapendekezo kwa Sekretarieti ya Mkoa, ambao nao

wakiridhika watawasilisha kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Vijiji, ambaye atayapitia na baada ya uchambuzi atamshauri Waziri na Waziri akiridhia kwamba matumizi yale ni sawasawa, yatafanyika mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, sasa hatujui kama ni mamlaka ipi iliyowaidhinishia hawa, ndiyo maana tukasema tumewaandikia kwanza wao watoe maelezo na baada ya kupata maelezo yao ndipo tuchukue sasa hatua ya kufanya uchunguzi wa kina na tutakapobaini kwamba walifanya makusudi bila idhini ya mamlaka yoyote *then* tunachukua hatua ya kutwaa mashamba yale.

Pili, mgogoro uliopo katika eneo la Magereza; eneo lile lilitengwa kwa ajili ya Magereza pale Karatu Mjini, lakini baadaye Halmashauri ya Wilaya ya Karatu ikagawa viwanja pale baada ya Magereza kutengewa eneo lingine kwa maelezo kwamba eneo lile halitoshi. Halmashauri ya Wilaya ya Karatu iligawa viwanja pale na kuwamilikisha Wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, mimi baada ya kufika pale, nilitoa agizo kwamba eneo lile lisiendelezwe na mwaka jana, Mkuu wa Wilaya akaniletea taarifa kwamba, kuna maendelezo yameanza kufanyika pale na vijana wanataka kuanza kuvamia kwa sababu wanaamini kwamba ni haki yao nao kupata sehemu. Tulimwomba Mkuu wa Mkoa wa Arusha aunde Kamati ya Uchunguzi ikachunguze ni akina nani hasa waliohusika katika kumilikisha eneo lile, kwa sababu kilichooneshwa kwangu kuna barua zilizoletwa kwangu ambazo zinaonesha kwamba, eneo lile liligawanywa miaka ya 1990 wakati huo eneo hilo lilikuwa bado chini ya Magereza. Kwa hiyo, ni lazima tufanye

uchunguzi ili tujue hasa ni nani amehusika na baada ya hapo hatua zitachukuliwa dhidi ya wahusika na eneo lile litarudishwa na kugawiwa kwa utaratibu wa kawaida.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hata mngekaa ninyi hapa mngeona saa imeisha, hili swali Naibu Waziri anaifahamu sana Wizara yake, akipewa maswali inakuwa semina. Kwa hiyo, imetosha. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee na kuwatambua wageni waliopo hapa. Tunao wageni kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, tunao wageni wa Mheshimiwa Spika, wapo katika *Speaker's Gallery,* hawa ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wamekuja kututembelea. Nitawataja wachache wafuatao waliokuja; yupo Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mheshimiwa Ali Abdallah Ali; naomba Mheshimiwa usimame tukuone, ahsante sana. Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, karibu sana. Ameongozana na ujumbe ufuatao: Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi, ambaye ni Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma. Tunaye Mheshimiwa Mahamoud Mohamed Mussa, Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi, naomba asimame alipo. Tunaye Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Yahya Khamis Hamad, ahsante karibu. Tunaye Katibu wa msafara Ndugu Amour Amour, ahsanteni sana, karibu sana. Mtakuwa na sisi kwa siku mlizojipangia chini ya mwenyeji wenu Mheshimiwa Naibu Spika.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Kitope, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, ambao ni

Mwenyekiti wa Vijana CCM Wilaya ya Mjini Unguja, Ndugu Omar Suleiman Mohamed. Yupo Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa Wilaya ya Mjini Unguja, Ndugu Omar Justas Morris. Yupo Mjumbe wa Halmashauri Kuu pia wa Wilaya ya Amani, Ndugu Nara Juma Mohamed. Pia yupo Mwandishi wa Habari wa Gazeti la Zanzibar Leo, Ndugu Mwantanga Ame. Naona hawapo watakuja baadaye. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nina wageni waliofika kwa ajili ya mafunzo, ni Wanafunzi 100 kutoka Shule ya Msingi Hazina Dar es Salaam; wasimame mahali walipo wote, ahsante sana, nimefurahi kuwaoneni, poleni na safari na msome kwa bidii. Tunao Wanafunzi wengine 80 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* Dodoma, naomba wasimame mahali walipo; nafikiri watapata nafasi baadaye. Yupo pia Ndugu Nuru Yahya kutoka Chuo cha Mipango Dodoma; karibu sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Wabunge: Wapo wageni 150 wa Mheshimiwa Dkt. Fenella Mkangara, Waziri wa Habari, Vijana, utamaduni na Michezo, ambao ni Maafisa Habari na Mawasiliano kutoka Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali, ambao wapo hapa Dodoma kwa Mkutano wao wa Mwaka, unaoongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Habari Maelezo, Ndugu Assa Mwambene. Naomba wageni wa Mheshimiwa Waziri wasimame popote walipo; karibuni sana, tunawatakia kazi njema na kazi yenu katika miaka hii ni changamoto ya kutosha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Waziri wa Mambo ya

Ndani ya Nchi, ambao ni Kamishna wa Sheria na Utawala wa Magereza, Dkt. Juma Malewa; ahsante karibu sana.

Tunaye Naibu Kamishna wa Magereza, Bibi Edith Mallya; ahsante sana. Siku hizi wanawake hata hawawapigii makofi wanawake wenzao sijui mmekula nini; unafikiri kazi ndogo hiyo? *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna Kamishna wa Magereza, Ndugu Steven Nzawila, naomba asimame; ahsante sana.

Tuna Kamishna wa Magereza mwingine, Ndugu Vincent Marissa, naomba asimame alipo.

Tunaye Kamishna wa Magereza, Ndugu Makoti Wabare. Karibuni sana Makamishna, naamini mmekuja kwenye shughuli maalum hapa, basi niwatakie kazi njema. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Stephen Masele, ambao ni Ndugu Anascholastica Mathew Ndagiwe na Ndugu Elizabeth Marimba. Naomba wasimame hawa waliko, siwaoni nafikiri walikosa nafasi Ukumbini.

Wageni wa Mheshimiwa Joshua Nassari ni Ndugu Christina Wena. Huyu Ndugu Christina Wena ni Rais wa Shirika Lisilo la Kiserikali la Afrika, ameambatana na Maafisa wawili. Christina yuko wapi? Nadhani na yeye pia amekosa nafasi. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa John Mnyika, ambaye ni Ndugu Joel Deus Sasabo; yuko wapi huyu? Ahsante. *(Makofi)*

Halafu tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Abbas Zubeir Mtemvu, kutoka Temeke, ambao wanasimamia Mfuko wa *Poverty Fighting in Tanzania (PFT) VICOBA,* wakiongozwa na Ndugu Ali Kibwana Kipendaroho. Huyu naye yuko wapi na wenzake? Ahaa, wenyewe wako hapa; ahsante sana, naamini kabisa *VICOBA* vinawasaidia watu kupambana na umaskini mdogomdogo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Matangazo ya kazi. Ninyi mbona mnapenda maneno haya, eeh? Matangazo ya Kazi. *(Kicheko)*

Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John Momose Cheyo, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali kuwa, leo tarehe 7 Februari, 2013, kutakuwa na Kikao cha Kamati, kuanzia saa saba mchana, Ukumbi wa Msekwa *C*.

Mheshimiwa James David Lembeli, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naye anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana watakuwa na Kikao chao katika Ukumbi Namba 231.

Nina tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi

Chana, yeye anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana kutakuwa na Kikao katika Ukumbi Namba 227 na ni baada ya saa saba.

Ofisi pia inawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba, Maafisa wa Vitambulisho vya Taifa wapo hapa Bungeni, katika Ukumbi wa Msekwa, kuanzia tarehe 6 Februari, 2013, kwa ajili ya kutoa huduma zifuatazo: Kuna kupiga picha na kuchukuliwa alama za vidole, bado kuna Wabunge kama 33 hawajapiga picha hizo. Kwa hiyo, wale ambao wanajua hawajapiga picha wala kuweka alama za vidole kwa sababu ya vitambulisho, waende kule.

Kesho tarehe 8 Februari, 2013, kutakuwa kuna zoezi la kutoa Vitambulisho kwa wale waliokwishapiga picha na itakuwa siku moja. Kwa hiyo, mtakwenda kwa utaratibu, nadhani itabidi tufanye utaratibu kwa sababu siyo kila mtu atakuwa anaondoka hapa. Zoezi hili la Kitaifa ni la muhimu kwa kila Mtanzania. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kutumia nafasi hii ili kuepuka usumbufu wa kupata huduma hizo nje ya hapa Bungeni.

Tangazo lingine ambalo ninapenda kusema; Waheshimiwa Wabunge, mkiwa hapa Bungeni hamko likizo, mnapaswa kuwepo Bungeni na wale ambao hawapo wanazo sababu maalum, lakini si kila mtu anapotea tu. Kama jana jioni walihesabiwa waliokuwepo tulikuwa wachache mno na ilikuwa ni aibu kwetu sote. Kwa hiyo, mimi ninaomba sana Waheshimiwa, mjue tuko kazini. Tusianze kuchungana kama vile hatuna uwajibikaji wa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), anaomba niwatangazie Wabunge wa Majimbo ya kutoka Zanzibar, mkutane naye saa saba mchana baada ya kumaliza Kikao hiki, lakini hakuniambia akutane nao wapi; sijui wanakutana wapi sasa? Ahaa, ni hapo *Basement* hapo. Kwa hiyo, ni Wabunge wa Majimbo wa kutoka Zanzibar, wakutane pale *Basement* pale.

Matangazo mengine yanakuja wakati tumesimama, inakuwa tatizo.

Waheshimiwa Wabunge, ninapenda kueleza kwamba, mtakumbuka kuwa jana tarehe 6 Februari, 2013, Mheshimiwa Naibu Spika, alitoa ufafanuzi kuhusu uwasilishwaji wa Nakala za Mitaala ya Kufundishia. Hii ni baada ya Serikali kuwasilisha Nakala za Mitaala kama ilivyoahidi.

Kwa kutumia Kanuni ya 5(1), Mheshimiwa Naibu Spika, aliwateuwa Wajumbe sita wachunguze uhalali wa nakala zilizowasilishwa hapa Bungeni. Wajumbe wa hicho Kikao walikuwa Mheshimiwa Benardetha K. Mushashu - Mwenyekiti, Mheshimiwa James F. Mbatia - Mjumbe, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa - Mjumbe, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa - Mjumbe, Mheshimiwa Mchungaji Israel Y. Natse - Mjumbe na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa - Mjumbe. Hii ndiyo Kamati ambayo Mheshimiwa Naibu Spika, aliiunda jana.

Kamati hiyo ilipewa hadidu ya rejea moja tu, ambayo ilikuwa ni kuthibitisha uhalali wa Mitaala iliyowasilishwa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Ili kukamilisha kazi yake, Kamati ilikutana na kupitia Nakala za Mitaala ya Elimu

ya Awali, Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari. Ili kujiridhisha kama Mitaala hiyo ni sahihi, Kamati ilipitia Nakala Halisi za Mitaala hiyo kutoka Serikalini na Nyaraka za Serikali, zilizoidhinisha kutumika kwa Mitaala hiyo. Nyaraka hizo ni wa kwanza, Sheria ya Elimu ya Mwaka 1975. Wa pili, Waraka wa Elimu Namba 16 wa Mwaka 1997. Wa tatu, Waraka wa Elimu Namba 9 wa Mwaka 2004. Wa nne, Waraka wa Elimu Namba 10 wa Mwaka 2004. Wa tano, Waraka wa Elimu Namba 2 wa Mwaka 2005. Wa sita, Waraka wa Elimu Namba 1 wa Mwaka 2006; na Saba, Waraka wa Elimu Namba 2 wa Mwaka 2006.

Vilevile Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wataalamu wa Wizara hiyo, walitoa ufafanuzi wa Hoja mbalimbali zilizojitokeza. Kutokana na uchambuzi huo, Kamati ilibaini kuwa, Nakala zilizowasilishwa zilikuwa sahihi na ni Mitaala Rasmi ya Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari. Hivyo, Nakala za Mitaala hiyo sasa nitazigawa, kwa sababu nilikuwa nazo mimi, lakini nilishindwa kugawa, sikuwa na uhakika zikoje. Sasa watazigawa kwa Wabunge wote, kama ilivyoahidiwa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu nina kazi ya kufuatilia mambo mengine ambayo inatubidi kuyafanya leo na kesho, naomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Zungu, aendelee na kazi ya kuniwakilisha. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu, tuendelee.

## HOJA ZA SERIKALI

## M A A Z I M I O

**Azimio la Bunge la Kujiunga na Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo vya Ugaidi wa Kutumia Nyuklia *(International Convention for the Suppression of Acts of Nuclear Terrorism, 2009)***

**Azimio la Bunge la Kujiunga na Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu Dhidi ya Watu Wenye Kinga ya Kimataifa Pamoja na Wakala wa Diplomasia *(Convention on the Prevention and Punishment of Crimes Against Internationally Protected Persons, Including Diplomatic Agents, 1973)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumekubaliana Bunge hili litaendeshwa kwa Kanuni, ndivyo tulivyokubaliana. Sasa, taratibu za Mbunge kutaka kusimama zimeainishwa kwenye Kanuni na kikubwa, inatakiwa Mbunge akisimama Spika amwone; sijakaa, mmesimama, nitaona vipi sasa! *(Kicheko/Makofi)*

Mamlaka ya Kiti hiki, hayana tofauti na Mamlaka yoyote mengine nje ya Bunge hili. Sasa kama unayo haki ya

Mwongozo, unayo haki ya kutoa Taarifa, unayo haki ya humu ndani, lakini si twende kwa utaratibu; sijapumzika watu 20 Mwongozo! *(Kicheko)*

Sasa mimi ninaomba, kwa vile nimemwona Mheshimiwa Mbatia, nampa nafasi Mheshimiwa Mbatia. *(Makofi)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Naomba kutumia Kanuni ya 37(4); naomba kuinukuu: "Baada ya Hati kuwasilishwa Bungeni, Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Mbunge, anaweza kutoa hoja kwamba, Bunge lijadili hati hiyo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, imewasilishwa Mitaala inayoitwa na Serikali kwamba ni Mitaala Rasmi. Mitaala hiyo niliyoiomba hapa Bungeni tarehe 30 ya mwezi Oktoba, 2012, Serikali ilihakikisha kwamba, italeta Mtaala wa Mwaka 2005, ambao ulitokana na Mtaala wa Mwaka 1997.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtaala ulioletwa Mezani ni wa Mwaka 2005 uliotokana na Mtaala wa Mwaka 1998. Kwa hiyo, kwa mujibu wa *Hansard,* Mtaala uliotokana na wa mwaka 1997, bado haujawasilishwa Mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, suala la Elimu ya Sekondari ni la Jamhuri ya Muungano. Mtaala uliowasilishwa Mezani wa Elimu ya Sekondari ni wa Tanzania Bara na siyo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Mtaala uliowasilishwa Mezani, hauna *International Standard Book Number,* kama ilivyo Mihtasari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kwamba, Mwidhinishaji wa Mitaala ni Kamishna wa Elimu, kwa mujibu wa Sheria ya Elimu ya Mwaka 1975. Mihtasari yote inaonesha aliyeidhinisha ni Afisa Elimu Kiongozi, lakini Mtaala haujaonesha nani Mwidhinishaji wa Mtaala huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa ombi ambalo liko kwenye *Hansard* ya Bunge Tukufu, Mtaala utakaotokana na wa mwaka 1997 bado haujawasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lijadili Mitaala iliyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia, uliomba Mwongozo wa Kiti.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walipiga kelele)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kiti kimesema kimepokea Mwongozo na Mwongozo wangu nitakupatia baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, jana tuliahirisha Kikao kutokana na Shughuli ya Bunge, ambayo tulishindwa kuikamilisha kutokana na akidi. Kutokana na kuahirisha Kikao kile, akidi ya Bunge leo imetimia na tunatimiza hoja yetu. Sasa nitawahoji muamue hoja.

**Azimio la Bunge la Kujiunga na Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo vya Ugaidi wa Kutumia Nyuklia**
***(International Convention for the Suppression of Acts of Nuclear Terrorism, 2009)***

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kujiunga na Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo vya Ugaidi wa Kutumia Nyuklia Liliridhiwa na Bunge)*

**Azimio la Bunge la Kujiunga na Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu Dhidi ya Watu Wenye Kinga ya Kimataifa Pamoja na Wakala wa Diplomasia**
***(Convention on the Prevention and Punishment of Crimes Against Internationally Protected Persons, Including Diplomatic Agents, 1973)***

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kujiunga na Mkataba wa Kuzuia Uhalifu Dhidi ya Watu Wenye Kinga ya Kimataifa Liliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kuwasilisha vizuri. Niwapongeze Wabunge, kwa michango yao ya *reservation* ya Serikali, kuingia nayo kwenye Makao Makuu wakati mna-*register* Maazimio haya. Hivi vipengele muhimu sana vimezungumzwa na Wabunge na ni lazima mvichukue kwa *interest* ya Taifa letu. Tunaendelea, Katibu.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2012 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2012)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa *AG,* hebu subiri kidogo. Mheshimiwa Ali Keissy Mohamed.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Hansard* ambayo aliitoa Mheshimiwa Mbatia, Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi na Mbunge Mteuliwa, alisema kwamba, kama Mtaala wa 2005 hautaletwa hapa Bungeni, yeye yuko tayari kujiuzulu. Na *Hansard* yake hii ya…

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba ...

*(Hapa Wabunge fulani walikuwa wanapiga kelele)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilinde, nazungumza. Aliahidi mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba, kama Mtaala hautaletwa hapa, yuko tayari kujiuzulu na Serikali haitapata hasara yoyote kwa sababu yeye ni Mbunge aliyeteuliwa, hakuna uchaguzi utakaofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima, ajiuzulu. *Hansard* hii hapa, ukurasa wa 64, inasema atajiuzulu kwa manufaa ya Wananchi wake na Chama chake. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy, kaa. Mheshimiwa *AG.*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Nimewaomba Waheshimiwa Wabunge, nawasihi sana tujaribu kuliendesha Bunge hili kwa haki na utaratibu wa Kanuni. Nimetoa nafasi kwa Mheshimiwa Mbatia, ndiyo mwenye hoja. Jana nilimpa nafasi Mheshimiwa Machemli na Kikanuni wala nafasi ile hairuhusiwi, lakini kwa sababu alikuwa na hoja ya msingi, nikaona nimpe nafasi. Sababu ni *interest* ya nchi na *interest* ya watu wake, kama Serikali haikuja na majibu sahihi, basi wakae pamoja waje na majibu sahihi; mnapotaka humu ndani kutupiana maneno, *not with this Chairman. (Makofi)*

Mheshimiwa *AG,* endelea.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona Mheshimiwa Keissy, umempa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG?*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, nakuomba ukae, nitakupa nafasi baadaye.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za 2007, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada uitwao Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Namba 3) wa Mwaka 2012, *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2012),* sasa usomwe mara ya pili na Bunge lako Tukufu liujadili na hatimaye liupitishe kuwa Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawasilisha hoja hii na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kwa mwaka huu, ninaomba kumshukuru Mungu, Mwenye Huruma, kwa kutujalia afya ya mwili na akili. Aidha, kwa kuwa Mwaka Mpya wa Shughuli za Mahakama Nchini unaanza, ninapenda kutumia nafasi hii, kuwatakia kazi njema Mahakimu wote na Majaji Nchini. Ninawatakia moyo thabiti wa kudumisha Utawala wa Sheria na kutenda haki pekee kwa mujibu wa masharti ya Katiba, Sheria, Kanuni na Desturi zinazofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kwa kipekee, kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, walioupitia Muswada huu na kutoa ushauri wao ambao umezingatia marekebisho haya tuliyofanya. Aidha, kwa aina ya pekee, napenda kumshukuru Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bwana George Masaju na Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa utendaji wao wa kazi mzuri na hususan *Division* ya Uandishi wa Sheria, kwa kuandaa Muswada huo, pamoja na Wataalam wa Asasi mbalimbali waliohusika katika utayarishaji wa Muswada huu. Natarajia kwamba, tutaendelea kuwa na weledi wa kuwatumikia Watanzania wote na kuwaondolea kero zao katika Sekta ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa mara nyingine, kuliomba Bunge hili liendelee kuwa na weledi na utulivu kwa Wabunge. Kwa heshima na taadhima, naomba sasa kuwasilisha mbele yako Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho ya Muswada ambalo limeambatanishwa na ambalo nina uhakika, Waheshimiwa Wabunge, wameshagawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wagawiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria nane tu, kwa lengo la kuondoa upungufu uliobainika wakati wa matumizi ya sheria hizo, kuongeza masharti mbalimbali ili kuleta uwiano wa sheria zinazorekebishwa na kusaidia utekelezaji madhubuti wa sheria hizo pamoja na mageuzi katika Sekta ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hizi kwanza ni Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu, Sura ya 423, Toleo la 2002, Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432, Toleo la 2002, Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11, Toleo la 2002, Sheria ya Ardhi, Sura ya 113, Toleo la 2002, Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma, Sura ya 418, Toleo la 2002, Sheria ya Mafao ya Wastaafu ya Watumishi wa Umma, Sura ya 371, Toleo la 2002, Sheria ya Kusimamia Umiliki wa Ardhi katika Vijiji vilivyokwisha anzishwa, yaani Sura ya 267, Toleo la 2002 na Sheria ya nane ni Sheria ya Mabaraza ya Kata, Sura ya 206, Toleo la 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wenyewe umegawanywa katika sehemu tisa:-

Sehemu ya kwanza, inaweka masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Sheria inayokusudiwa.

Sehemu ya pili ya Muswada, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu kwa kuongeza kifungu kidogo cha (c) kwenye tafsiri ya neno kufadhili ugaidi, yaani *terrorist financing*. Sehemu hii imefanyiwa marekebisho kwa kuzingatia ushauri wa Kamati kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho. Marekebisho yanayopendekezwa, yanalenga kuongeza kwenye tafsiri ya kosa la kufadhili ugaidi kwa kuweka bayana vitendo vinavyohusika na ufadhili wa ugaidi, ikiwa ni pamoja na kutaka ufadhili au kutoa misaada ya kifedha kufadhili ugaidi. Tafsiri ya neno hilo kama ilivyo sasa, haijumuishi matendo hayo na hivyo tunaona unaachwa mwanya kwa wahalifu kutumia fursa hii kufanikisha malengo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu. Marekebisho haya yanayopendekezwa ni kuongeza tafsiri ya neno Mahakama kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa Mahakama zenye uwezo wa kusikiliza mashauri chini ya Sheria hii kuwa ni Mahakama za Mahakimu Mkazi na Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mahakama za Mahakimu na vifungu vya nane na tisa vya kwenye Muswada vimerekebishwa kwa sasa. Naomba Waheshimiwa Wabunge, waangalie kwenye Muswada, kwa sasa kuna Jedwali la Marekebisho linalopendekeza marekebisho katika kifungu cha 6, 7, 13, 18 na kifungu cha 58 pamoja na sehemu ya sita ya Sheria hiyo ambavyo havikuwepo mwanzoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho haya ni kuboresha mfumo wa utoaji wa haki nchini, yanayohitaji kuongeza elimu ya Mahakimu katika ngazi ya Mahakama za Mwanzo na kifungu cha 6, kifungu 58 pamoja na sehemu ya sita ya Sheria hiyo, vinarekebishwa ili kuwapa Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu wa Kazi, mamlaka ya kusikiliza Mashauri katika Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 6 cha Sheria ya Mahakimu kinatoa mamlaka ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo kusikiliza kesi katika Mahakama za Mwanzo. Tunafanya marekebisho sehemu hiyo ili kuwawezesha Mahakimu wa Kazi pamoja na Mahakimu wa Wilaya kukaa na kusikiliza kesi katika Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kufikiria suala la Wazee wa Mahakama katika ngazi ya Mahakama za Mwanzo. Kifungu cha saba kinarekebishwa ili kutoa fursa kwa Washauri wa Mahakama kuhusishwa katika mashauri ya kimila, mirathi pamoja na mashauri ya Kiislamu (kesi za Kiislamu tu). Vilevile inapendekezwa kuwa ushauri wa Washauri hawa uwe kwa dhumuni la kushawishi Mahakama na siyo Mahakama kufungwa na ushauri huo kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa Washauri wa Mahakama ni wa kihistoria na ulitetwa na Sheria ya Mapokeo iitwayo *Tanganyika Order in Council* ya 1920, iliyoanza kutumika nchini hapa tarehe 22 mwezi Julai, 1920. Kwa mujibu wa Sheria hiyo ya Mapokeo, Washauri wa Mahakama walikusudiwa kuwasaidia watoa maamuzi, yaani Mahakimu pamoja na Watendaji wa Serikali waliokuwa wanafanya kazi ya Hakimu, kutoa maamuzi ya haki ambayo yalikuwa yanazingatia mila za Watu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kubwa wakati huo lilikuwa ni kujenga imani ya Wanachi dhidi ya dhana ya kuwa Sheria za Mkoloni zilikuwa ni kandamizi. Kwa kuwa kwa wakati huo mila na desturi zilitawala katika kuamua masuala yote ya kijamii, basi ilikuwa ni muhimu kuhifadhi mila hizo. Kwa sasa Washauri hawa wana jukumu la kushauri katika masuala yasiyo ya kisheria na badala yake wanamwachia Hakimu jukumu la kushughulikia masuala ya kiufundi katika Sheria, yaani wao ni waamuzi katika *Matters of Facts* lakini Mahakimu ni waamuzi katika *Matters of Law*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 18 kinarekebishwa ili kuzingatia mamlaka ya kusikiliza mashauri ya ndoa kama yalivyowekwa kwenye Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, Sura ya 29, Toleo la 2002. Marekebisho haya kwa ujumla yatawezesha mashauri katika Mahakama za Mwanzo kusikilizwa na Mahakimu wa aina zote na hivyo kuimarisha utoaji wa haki na kupunguza mlundikano wa kesi katika Mahakama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama hizi kama tujuavyo, zipo karibu na Wananchi wengi na Mahakimu wa Cheti cha Sheria na Diploma ya Sheria waliopo sasa wataendelea na kazi ya Uhakimu ila kada hiyo sasa haitarajiwi tena kuajiriwa Mahakamani baada ya hawa waliopo sasa kumaliza muda wao. Aidha, utaratibu huu hautaathiri utaratibu wa kukata rufaa uliopo sasa, kinachobadilika ni ngazi ya elimu ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo tu, lengo likiwa mwishoni Mahakimu wote wawe na Shahada ya Sheria kwa kuwa kwa sasa bado utaratibu wa kada tatu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo unaendelea kuwepo, yaani Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo Wenye Cheti cha Sheria, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo Wenye Diploma ya Sheria na Mahakimu Wakazi Wenye Shahada. Uwezekano wa kuruhusu Mawakili katika Mahakama za Mwanzo hivi sasa hautawezekana hadi hapo tutakapobaki na kada moja ya Mahakimu Wakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ardhi kwa kufuta tafsiri ya neno *Land Division of the High Court,* yaani Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi na badala yake kuweka tafsiri ya neno *High Court,* yaani Mahakama Kuu na vile vile

inapendekezwa kuwa maneno *High Court Land Division* yafutwe katika Sheria hiyo popote yanapoonekana na badala yake yasomeke maneno *High Court*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha Mahakama Kuu ya Tanzania kwa ujumla wake, kusikiliza mashauri ya ardhi ambayo awali yalikuwa yakisikilizwa tu na Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi pekee. Tunategemea hii itaongeza kasi ya usikilizaji wa kesi za ardhi nchini. Hata hivyo, marekebisho yanayopendekezwa hayafuti Kitengo cha Ardhi cha Mahakama Kuu ya Tanzania bali yanaondoa mamlaka ya upekee, yaani *exclusive jurisdiction* kwa Kitengo cha Ardhi kusikiliza mashauri ya ardhi pekee. Marekebisho ya msingi kuhusu jambo hili yalifanywa na Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Namba 2) ya Mwaka 2010, ambapo maeneo yaliyo kwenye Muswada huu hayakufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma. Kifungu cha 38 kinaandikwa upya ili kutoa nafasi kwa Bunge kujadili majibu ya Serikali na Taasisi zake kuhusu hoja zilizoibuliwa kwenye Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyo kwa Taarifa za Kamati za Kudumu za Bunge. Ilivyo sasa, Serikali huwasilisha Bungeni majibu ya Hoja zilizoibuliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu pasipo kuwa na masharti ya Bunge kujadili majibu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii imefanyiwa marekebisho na napenda kuishukuru sana Kamati iliyopitia Muswada huu. Tumefanya marekebisho katika Ibara ya 19 inayorekebisha kifungu cha 39 kwa kuongeza kifungu

kidogo cha pili. Marekebisho haya yanalenga katika kuweka utaratibu wa Bunge katika kujadili taarifa zinazowasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Sheria hii. Kwa msingi huo, taarifa zitajadiliwa na Bunge baada ya kupitiwa na Kamati husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii pia imefanyiwa marekebisho kwa kuandika upya kifungu cha 40 ili kumruhusu Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali kujumuisha taarifa ya utekelezaji wa Serikali katika taarifa yake ya mwaka. Marekebisho haya yanalenga katika kuweka bayana utekelezaji wa Serikali juu ya Hoja za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, marekebisho yanafanywa ili kumuwezesha Waziri wa Fedha kuwasilisha taarifa ya majibu ya Serikali ya Hoja ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu sambamba na uwasilishwaji wa taarifa hiyo kwa Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya saba inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mafao ya Wastaafu ya Watumushi wa Umma. Lengo la marekebisho haya ni kuweka masharti ya umri wa kustaafu kwa hiari kwa Maafisa na Askari wa Magereza kwa kuongeza umri wa kustaafu kwa baadhi ya Maafisa wa Jeshi hilo. Maafisa ambao umri wa kustaafu unapendekezwa kuongezwa ni wale wenye vyeo vya *Corporal* hadi *Sergeant* ambao watastaafu kwa lazima wanapofikia umri wa miaka 55 badala ya miaka 50 ya sasa. Maafisa wengine ni Mkaguzi Msaidizi na Mkaguzi wa Magereza ambayo inapendekezwa kuwa wastaafu kwa lazima wafikishapo umri wa miaka 60 badala ya miaka 55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itawezesha Jeshi la Magereza kuendelea kunufaika na utaalam na uzoefu wao. Aidha, marekebisho haya yanaendana na marekebisho tuliyofanya kuhusiana na Jeshi la Polisi, Jeshi la Zima Moto na Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nane ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kusimamia Umiliki wa Ardhi katika vijiji vilivyokwisha anzishwa na tunafuta tafsiri ya neno *High Court* kuwa ni Kitengo cha Ardhi cha Mahakama Kuu ya Tanzania. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa mamlaka ya upekee kama nilivyosema hapo awali kwa Kitengo cha Ardhi cha Mahakama Kuu kusikiliza Mashauri chini ya Sheria hii peke yake ili kuwezesha masjala zote za Mahakama Kuu ya Tanzania kusikiliza mashauri hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho haya yanaoanisha Sheria hii na marekebisho yaliyofanywa na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) ya Mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tisa na ya mwisho, inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Mabaraza ya Kata ili kuwawezesha Mahakimu Wakazi au Mahakimu wa Wilaya katika Mahakama za Mwanzo kushughulikia masuala yaliyoainishwa ndani ya Sheria hiyo kwa ajili ya kusikilizwa na Mahakama za Mwanzo. Marekebisho haya yanalingana na marekebisho tuliyofanya kwenye Sheria ya Mahakimu hapo mwanzo. Hii ni pamoja na kusikiliza rufaa na kuidhinisha adhabu zilizotolewa na Baraza la Kata na kwa sasa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ndiyo wanaotambulika chini ya Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuwasilisha Muswada huu na kwa ujumla bila kuwataja majina, napenda kuishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Andrew Chenge, kwa msaada wao na ushauri wao waliotupa kwenye Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitamwita Mwenyekiti au Msemaji wa Kamati.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2007, ili niweze kutoa maoni na ushauri kwa niaba ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali kwa mwaka 2012 *(Written Laws (Miscellaneous Ammendments) (No. 3) Act, 2012* uliowasilishwa hivi punde na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipewa kazi ya kupitia na kujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya

Sheria mbalimbali ya mwaka 2012. Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria nane, yaani Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu *(Anti Money Laundering Act)*; Sheria ya kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu *(The Anti Trafficking in Persons Act)*; Sheria ya Mahakimu *(The Magistrates Courts Act)*; Sheria ya Ardhi *(The Land Act)*; Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma *(The Public Audit Act)*; Sheria ya Mafao ya Wastaafu ya Watumishi wa Umma *(The Public Service Retirement Benefit Act)*; Sheria ya Kusimamia Umiliki wa Vijiji vilivyokwishaanzishwa *(The Regulation of Land Tenure), Establish Villages Act* na Sheria ya mwisho ni Sheria ya Mabaraza ya Kata *(The Ward Tribunal Act).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho haya yana lengo la kuondoa upungufu uliobainika wakati wa utekelezaji wa sheria hizi na pia yanakusudia kuongeza masharti mbalimbali ili kuleta uwiano katika sheria zinazorekebishwa na hivyo kusaidia utekelezaji wa sheria hizo.

Kamati yangu ilitekeleza kazi hiyo kikamilifu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wadau mbalimbali waliowasilisha mapendekezo yao mbele ya Kamati. Ushauri na maoni yao yote tumeyazingatia katika kujadili na kuuchambua Muswada huu kwa niaba ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni Maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2012:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato mzima wa Muswada huu ulianza katika Mkutano wa Bunge uliopita, yaani mwezi Novemba, 2012. Hata hivyo, hawakuweza kuuwasilisha kipindi hicho kwa kuwa Serikali iliomba ipewe muda zaidi wa kufanyia kazi Muswada huo ili kuleta tija katika matumizi ya sheria zinazopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zinazofanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu kama nilivyosema awali, zinagusa maeneo mengi ya kijamii hasa katika maeneo ya haki za binadamu, umiliki wa ardhi, mafao, pamoja na ukaguzi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hali hii ni dhahiri kwamba, Muswada huu unaoletwa na Serikali mbele ya Bunge lako Tukufu ni muhimu. Kwa upande wa marekebisho ya kwenye eneo la Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu, marekebisho hayo pamoja na mambo mengine, Kamati ilikubaliana na mapendekezo yanayoletwa na Serikali kupitia Muswada huu kwenye eneo hilo. Hata hivyo, ilitoa angalizo kwamba, pendekezo la Serikali linalokusudia kupanua tafsiri ya maneno *terrorist financing* katika sheria hiyo, ambayo yanasomeka *any other act constituting terrorist financing as provided in the prevention of terrorism act;* Kamati inaamini pendekezo hilo limeandikwa kwa lugha pana mno.

Kamati iliishauri Serikali ione uwezekano wa kulifanyia marekebisho eneo hili ili lisilete mkanganyiko. Serikali iliafiki pendekezo la Kamati na tayari eneo hili limefanyiwa marekebisho na Serikali ambayo Kamati inayaafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho yanayohusu Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, ambayo ipo katika sehemu ya pili ya Muswada, marekebisho hayo yanayopendekeza ni kuongeza tafsiri neno Mahakama kwenye Sheria hiyo, yaani *the court* na lengo lake ni kutoa ufafanuzi wa Mahakama zenye mamlaka ya kusikiliza mashauri chini ya Sheria hii kuwa ni Mahakama ya Hakimu Mkazi au Mahakama ya Wilaya. Kamati inakubaliana na pendekezo la Serikali na madhumuni ya marekebisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya tatu inayofanyiwa marekebisho ni Sheria ya Mahakama za Mahakimu na kwenye eneo hili tunaishukuru sana Serikali kupitia maelezo iliyotoa kwenye Kamati; na kama mlivyomsikia Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwenye eneo hili; Kamati inayaafiki mapendekezo ya Serikali katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakimu Wakazi au wa Wilaya kuweza kusikiliza mashauri katika Mahakama za Mwanzo tofauti na hali ya sasa ambapo Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo tu ndiyo wenye mamlaka ya kusikiliza mashauri yote katika Mahakama hizo. Kamati inaamini pia kuwa mapendekezo haya yataweza mashauri katika Mahakama za Mwanzo ambayo yatasikilizwa na Mahakimu wa aina zote, kuimarisha utoaji wa haki nchini, kwa sababu Mahakama hizi za Mwanzo ziko karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini marekebisho haya iwapo Bunge lako litayaafiki na Kamati inaomba Bunge lako liyaafiki, yatatoa changamoto kwa Mahakimu wa Stashahada na Diploma ya Sheria, waweze kujiendeleza katika ngazi za juu za elimu, kwa kuwa kada ya Hakimu wa

Mahakama ya Mwanzo haitaajiriwa tena kama Mahakimu. Hii ina maana kada hiyo inafutwa hatua kwa hatua na hivyo kwa wale waliopo watalazimika kujiendelea kama watapenda. Hata hivyo, Kamati inatoa angalizo kwa Serikali kuanza mchakato wa kuifanyia marekebisho Chuo cha Uongozi wa Mahakama kilichopo Lushoto ili kiweze kutoa elimu ya shahada kwa ajili ya kufidia upungufu utakaojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine linahusu Sheria ya Ardhi; kesi zinazohusu masuala ya ardhi, zinazidi kuongezeka na mashauriano yake yanakuwa yanachukua muda mrefu sana kupata maamuzi. Kwa mantiki hiyo, Kamati inakubaliana na marekebisho katika Sheria ya Ardhi ambapo sasa kesi hizo zitasikilizwa na Majaji wa Mahakama Kuu na kama alivyoeleza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lengo lake ni kuondoa ule upekee wa mamlaka ya Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi ambacho ndiyo kinasikiliza mashauri hayo.

Hata hivyo, marekebisho haya hayafuti Kitengo hicho bali yanaondoa mamlaka ya kipekee kwa Kitengo hicho kusikiliza mashauri ya ardhi. Na hivyo Kamati inakubaliana kabisa na pendekezo la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria nyingine inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Kusimamia Umiliki wa Ardhi katika Vijiji Vilivyoanzishwa na Sheria hiyo, Sura ya 267. Mapendekezo katika eneo hili yanashabihiana na hilo ambalo Kamati imelieleza kupitia marekebisho kwenye Sheria ya Ardhi na tunakubaliana na pendekezo la Serikali kwa madhumuni hayo hayo ya

kuharakisha usisitizwaji na kukamilika kwa mashauri yanayohusiana na ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imelipitia na kulijadili kwa kirefu sana, pendekezo la Serikali la marekebisho yanayopendekezwa kwenye Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma *(The Public Audit Act),* Sura ya 418 ya Sheria za Nchi. Dhana kuu hapa ni kuwa marekebisho haya sasa yatawezesha Bunge lako Tukufu kujadili Taarifa ya Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na kujadili majibu ya Serikali na Taasisi zake kuhusu hoja zilizotolewa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, pamoja na kujadili Taarifa za Kamati za kudumu zinazosimamia matumizi ya fedha za umma. Kamati inaamini kuwa mapendekezo yaliyoletwa na Serikali, yatasaidia kuondoa mkanganyiko uliokuwa unajitokeza wakati Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ilipokuwa inawasilishwa Bungeni na hatimaye kupelekwa kwenye Kamati husika kwa uchambuzi zaidi.

Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwenye eneo hili kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya nane ni Sheria ya Marekebisho ya Mafao ya Wastaafu ya Watumishi wa Umma na hii inalenga kwa Maafisa na Askari Magereza, kwa kuongeza umri wa kustaafu kwa baadhi ya Maafisa wa Jeshi hilo. Maafisa wanaolengwa ni wale wenye Vyeo vya *Corporal* hadi *Sergeant* kutoka miaka 50 hadi 55 pamoja na Mkaguzi Msaidizi na Mkaguzi wa Magereza kutoka miaka 55

hadi 60, itasaidia nchi pamoja na Jeshi hilo kunufaika na huduma, utaalam na uzoefu unaotolewa na askari hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tisa ya Muswada ambayo Kamati inakubaliana na pendekezo la Serikali yenye madhumuni ya kuwezesha Mahakimu Wakazi au Mahakimu wa Wilaya katika Mahakama za Mwanzo kushughulikia masuala yaliyowasilishwa katika Sheria ya Mabaraza ya Kata pamoja na kusikiliza rufaa na pia kuidhinisha adhabu zilizotolewa na Mabaraza ya Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha maoni na na ushauri huu, sasa napenda kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia maoni na ushauri wa Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula - Makamu wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Josephine Ngezabuke, Mheshimiwa Eustas Katagira, Mheshimiwa Maulidah Anna Valerian Komu, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, Mheshimiwa Abul-Aziz Mohamed Abood, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Amina Abdulla Amour, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Alhaji Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu na mimi

mwenyewe Mheshimiwa Mtemi Andrew John Chenge - Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Fredrick Werema na Watumishi wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, kwa kuweza kufanikisha Muswada huu. Tunawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kumshukuru Ndugu Michael Kadebe, Katibu wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa kukamilisha maandalizi ya taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, nawashukuru sana wapiga kura wa Jimbo langu la Bariadi Magharibi, kwa upendo wao kwangu na imani waliyoionesha kwangu na wanaendelea kuionesha kwangu. Mimi ninawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa uwezo wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inawashukuru Wadau wote waliojitokeza mbele ya Kamati kuwasilisha mapendekeo na maoni ambayo yamesaidia sana Kamati katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali ya mwaka 2002 ulichapishwa katika Gazeti la Serikali, tarehe 5 Oktoba, 2012 na kusomwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Tisa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa kadiri ya taarifa tulizo nazo, Muswada huu ulipelekwa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi ambayo hata hivyo, haikuujadili kwa kipindi chote cha Vikao vya Kamati za Bunge vilivyofanyika Dar es Salaam. Aidha, kwa sababu hiyo hiyo, Kamati ya Fedha na Uchumi haikufanya mkutano wowote na wadau mbalimbali nje ya Bunge hili Tukufu ili kuwapa wadau hao fursa ya kutoa maoni na ushauri wao juu ya uboreshaji wa Muswada.

Mwisho, kwa kadiri ya taarifa tulizonazo, hadi kufikia jana mchana, Kamati ya Fedha na Uchumi yenyewe ilikuwa haijakamilisha jukumu lake la kujadili Muswada na kuandaa taarifa yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Kamati kutokamilisha kazi ya kuujadili, Muswada huu uliwekwa katika Orodha ya

Shughuli ya tarehe 6 Februari, 2013 kwa ajili ya kusomwa Mara ya Pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo vyote hivi vinadhihirisha ukiukwaji mkubwa wa masharti ya lazima ya kanuni ya 84 ya Kanuni za Kudumu za Bunge hili Tukufu. Katika mazingira haya, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kujua kutoka kwako, kama Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, iliyopelekewa Muswada huu, amewahi kumjulisha Mheshimiwa Spika kwa maandishi kwamba Kamati yake imemaliza kujadili Muswada huu kama inavyotakiwa na masharti ya lazima ya kanuni ya 85 (1) ya Kanuni za Kudumu na lini Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi alifanya hivyo.

Kama Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi hajawahi kumjulisha Mheshimiwa Spika kwa maandishi kama inavyotakiwa na Kanuni za Kudumu za Bunge, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kutoka kwako, Mheshimiwa Spika amepata wapi mamlaka ya kuagiza kwamba Muswada huu uwekwe katika orodha ya shughuli za jana kwa ajili ya Kusomwa kwa Mara ya Pili, wakati taratibu za kutunga sheria zilizoainishwa katika kanuni za 84 na 85, za Kanuni za Kudumu za Bunge zilikuwa hazijakamilika, au zilikuwa zimekiukwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hii ya ukiukaji wa wazi wa Kanuni za Kudumu za Bunge hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itaachaje kuamini kwamba uongozi mzima wa Bunge umeshindwa kutimiza wajibu wake wa kutilia nguvu Kanuni zote za Bunge, kama inavyotakiwa na Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, itaachaje kuamini

kwamba, Uongozi mzima wa Bunge, unaendesha shughuli za Bunge na kutoa maamuzi bila haki wala uadilifu, kwa hila na upendeleo kwa Serikali na bila kufuata Kanuni za Kudumu za Bunge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuendelea na mjadala wa Muswada huu katika mazingira haya, ni kuliburuza Bunge na Kamati zake za Kudumu, na kulifanya Bunge lishindwe kutimiza majukumu yake ya Kikatiba ya kutunga sheria kwa kufuata Kanuni za Kudumu za Bunge, kama inavyoelekezwa na Ibara ya 89 na 97 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakutaka umwamuru mtoa hoja wa Muswada huu, aombe ruhusa ya kuondoa hoja ya Muswada huu kwa mujibu wa Kanuni ya 58(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, au atoe hoja ya kubadilisha mjadala wa Muswada huu chini ya kanuni ya 69 (1) hadi masharti yote ya Kanuni za 84 na 85 za Kanuni za Kudumu yatakapokuwa yametekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo utashindwa ama kukataa kutilia nguvu za Kanuni zote za Bunge katika Muswada huu, naomba kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kujadili *under protest* mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria mbalimbali yaliyoko katika Muswada huu, nikianzia na Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu, Sura 423 ya Sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada unapendekeza kufanya mabadiliko katika sehemu ya tafsiri iliyoko kwenye kifungu cha 3 cha Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu kwa kubadili tafsiri ya maneno kufadhili Ugaidi kwa kuongeza

aya mpya ya (c) yenye maneno, “Kitendo kingine chochote kinachohusu kufadhili ugaidi kama kilivyoainishwa kwenye Sheria ya Kuzuia Ugaidi”, kwa mujibu wa maelezo ya madhumuni na sababu za Muswada huu. Lengo la marekebisho haya ni kujumuisha matendo yanayokatazwa chini ya Sheria ya Kuzuia Ugaidi, kama matendo yanayozuiwa chini ya sheria hii. Kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia Ugaidi, matendo yanayohusu kufadhili ugaidi ni yale yaliyoainishwa katika vifungu vya 7(1) na 7(2) (d),(e), na (f) na vifungu vya 13, 14, 15,16,17 na 18 vya sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu hayana maana yoyote kwa sababu hayaongezwi wala kupunguza kitu chochote katika sheria hiyo. Hii ni kwa sababu Sheria ya Kuzuia Ugaidi ambayo ndiyo sheria mahsusi katika masuala ya ugaidi, tayari ilikwishakataza vitendo vya kufadhili ugaidi hata kama sheria hiyo haikuviita vitendo vilivyokatazwa kuwa ni vitendo vya kufadhili ugaidi. Hivyo, kwa mfano, kifungu cha 7(1) cha sheria hiyo kinakataza kuomba msaada au kutoa msaada kwa namna yoyote ile kuhusiana na kitendo cha kigaidi au kuomba msaada au kutoa msaada kwa kikundi kilichopigwa marufuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine kifungu cha 7(2)(d), (e) na (f) cha Sheria ya Kuzuia Ugaidi kinatoa tafsri ya neno ‘msaada’, kwamba linajumuisha kutoa fedha na huduma zinazohusiana na fedha, kufanya biashara wazi wazi au kisirisiri kwa kutumia mali inayomilikiwa au kudhibitiwa moja kwa moja; au kisisiri na kikundi cha kigaidi au kikundi kinachomilikiwa au kudhibitiwa na kikundi cha kigaidi na kuingia au kuwezesha moja kwa moja, au

kisirisiri mabadilishano ya fedha yanahusu mali iliyotajwa hapo juu.

Aidha, kifungu cha 13 cha Sheria hiyo kinakataza kutoa au kukusanya fedha kwa ajili ya kutekeleza vitendo vya kigaidi wakati kifungu cha 14 kinakataza kukusanya au kutoa mali na huduma kwa ajili ya kutekeleza vitendo vya kigaidi. Vile vile kifungu cha 15 kinakataza matumizi ya mali kwa ajili ya kutekeleza vitendo vya Kigaidi, wakati kifungu cha 16 kinakataza vitendo vya kusimamia au kudhibiti mali za kugaidi.

Mwisho, vifungu vya 17 na 18 vinakataza biashara ya mali inayomilikiwa kudhibitiwa na vikundi vya kigaidi na kuomba au kutoa msaada kwa vikundi vya kigaidi kwa lengo la kutekeleza vitendo vya kigaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwa uchambuzi huu kwamba Sheria ya Kuzuia Ugaidi inajitosheleza kabisa katika nyanja za kudhibiti vitendo vya kufadhili ugaidi. Itakumbukwa kwamba Sheria ya Kuzuia Ugaidi ilitungwa na Bunge hili Tukufu mwaka 2002, wakati Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu ilitungwa mwaka 2006. Hii ina maana kwamba, wakati tafsiri ya maneno “kufadhili ugaidi” yanaingizwa katika Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu. Vitendo vya kufadhili ugaidi tayari vilikuwa vimekwishafafanuliwa na kukatazwa na Sheria ya Kuzuia Ugaidi. Ndiyo kusema kwamba, kuingizwa kwa maneno hayo katika Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu mwaka 2006, hakukuwa na maana wala tija yoyote kisheria. Ndiyo kusema kwamba, mapendekezo ya sasa ya kufanya marekebisho ya maneno hayo, hayana maana wala tija yoyote kisheria. Ndiyo maana hata Serikali iliyoleta

mapendekezo haya, haijaeleza ni kwa jinsi gani tafsiri ya sasa ya maneno kufadhili ugaidi, imekwaza jitihada za kupambana na ugaidi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ieleze ni kwa vipi uwepo wa maneno "kufadhili ugaidi" na tafsiri yake katika Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu umeleta tija katika jitihada za kupigana na ugaidi. Aidha, Serikali itoe maelezo kwa Bunge hili Tukufu, ni tija ipi kisheria itapatikana kwa kuifanyia marekebisho tafsiri ya maneno "kufadhili ugaidi" kama inavyopendekezwa katika Muswada huu.

Vile vile, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli mbele ya Bunge hili kama, kwa kuzingatia vifungu mbalimbali vya Sheria ya Kuzuia Ugaidi vilivyofafanuliwa katika Maoni haya ya Kambi Rasmi, kuna sababu yoyote ya maana kwa maneno "kufadhili ugaidi" na tafsiri yake kuendelea kuwepo katika Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu.

Mwisho, Serikali itoe kauli kama, kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Kuzuia Ugaidi, kutakuwa na madhara yoyote kisheria endapo maneno hayo na tafsiri yake yatafutwa kabisa katika Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila ya maelezo ya kutosheleza juu ya masuala haya kutolewa na Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haitakuwa tayari kuunga mkono mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu kama yaliwasilishwa katika Muswada huu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiwezi kuridhia

marekebisho ambayo yana lengo la kuifanya Serikali ionekane inafanya kazi wakati hayana tija yoyote kisheria. Kwa upande mwingine, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza maneno “kufadhili ugaidi” na tafsiri yake yafutwe kabisa katika Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu. Hii ni kwa sababu vitendo vya kufadhili ugaidi tayari vimefafanuliwa vya kutosha na kukatazwa katika Sheria ya Kuzuia Ugaidi ambayo ndiyo sheria mahususi inayohusu vita dhidi ya ugaidi. Aidha, uwepo wa maneno hayo na tafsiri yake katika Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu hauna tija yoyote kisheria zaidi ya kuongeza ugumu wa kuitafsiri na kuitekeleza sheria hiyo pamoja na Sheria ya Kuzuia Ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu. Muswada unapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432 ya Sheria za Tanzania kwa kuongeza neno Mahakama katika kifungu cha (3) cha Sheria hiyo na kulitafsiri kuwa ni Mahakama ya Hakimu Mkazi au Mahakama ya Wilaya. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba mapendekezo haya hayajafanyiwa tafakari ya kutosha kwa sababu hayana tija wala maana yoyote kisheria. Inaelekea kuwa lengo pekee la kuleta mapendekezo ya marekebisho haya ni kuifanya Serikali ionekane inafanya kazi wakati ambapo marekebisho yanayopendekezwa hayatapunguza wala kuongeza tija ya kisheria katika sheria husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya madhumuni na sababu za Muswada yanasema kwamba kwa sasa Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, haina tafsiri ya neno Mahakama. Aidha, kwa mujibu wa maelezo hayo,

marekebisho yanayopendekezwa yana kusudio la kutoa ufafanuzi juu ya Mahakama inayopaswa kufungua mashtaka endapo sheria imekiukwa. Ni kweli kwamba licha ya neno “Mahakama” kutajwa katika vifungu mbalimbali vya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, neno hilo halijatafsiriwa mahali popote katika Sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kukosekana kwa tafsiri hiyo siyo na hakujawahi kuwa na tatizo la kisheria. Hii ni kwa sababu, kwa vile Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu ni Sheria ya Jinai, inatakiwa kusomwa pamoja na Sheria ya Mwenendo wa Jinai, Sura ya 20 ya Sheria za Tanzania. Sheria hiyo ndiyo sheria mama katika masuala ya uendeshaji wa kesi za jinai kwa sababu siyo tu inaweka utaratibu wa uendeshaji wa kesi hizo bali pia inatoa mamlaka kwa Mahakama mbalimbali juu ya kesi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwa mujibu wa kifungu cha 165(1) cha Sheria hiyo ya Mwenendo wa Jinai, kosa lolote chini ya sheria nyingine yoyote isipokuwa Kanuni ya Adhabu litashughulikiwa na Mahakama ambayo imetajwa kwa ajili hiyo katika sheria hiyo. Hata hivyo, kifungu cha 165(2) cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai kinaelekeza kwamba pale ambapo hakuna Mahakama iliyotajwa, kosa hilo litashughulikiwa na Mahakama ya chini iliyotajwa katika Sehemu B ya Nyongeza ya Kwanza ya Sheria hiyo kuwa ni kosa la kushughulikiwa na Mahakama ya chini. Sehemu B ya Nyongeza ya Kwanza ya Sheria ya Mwenendo wa Jinai inahusu makosa chini ya sheria nyingine isipokuwa Kanuni ya Adhabu. Safu ya pili na ya tano ya Sehemu B ya Nyongeza ya Kwanza inaelekeza kwamba kama adhabu ya kosa hilo ni kifungo cha miaka miwili au zaidi lakini

kisichozidi miaka 15, basi kosa hilo litashughulikiwa na Mahakama ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha pili cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai Mahakama ya chini, maana yake ni Mahakama iliyo chini ya Mahakama Kuu. Mahakama hizo za chini, kwa mujibu wa Sheria hiyo ni Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Hakimu Mkazi. Kufuatana na matakwa ya kifungu cha 4(5) cha Sheria ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu, mtu yeyote atakayepatikana na hatia ya makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu yaliyoainishwa katika kifungu cha 4(1) cha Sheria hiyo, anaweza kupata adhabu ya kifungo kisichopungua miaka miwili, lakini kisichozidi miaka kumi.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 5(3) cha sheria hiyo, adhabu ya mtu yeyote atakayepatikana na hatia ya makosa ya kuendeleza au kuwezesha usafirishaji haramu wa binadamu kama yalivyofafanuliwa na kifungu cha 5(2) inaweza kuwa kifungo kisichopungua mwaka mmoja, lakini kisichozidi miaka saba. Vile vile, kwa mujibu wa kifungu cha 7(3), mtu yeyote anayepatikana na hatia ya kosa la wakala *intermediary* katika usafirishaji haramu wa binadamu anaweza kufungwa kifungo kisichopungua miaka saba lakini kisichozidi miaka 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, kwa mujibu wa Sehemu B ya Nyongeza ya Kwanza ya Sheria ya Mwenendo wa Jinai ikisomwa pamoja na Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Mahakama zenye mamlaka ya kusikiliza kesi zinazohusu makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu ni Mahakama za Wilaya na Mahakama za Hakimu Mkazi. Hivyo basi, mapendekezo ya

marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu kama yalivyoletwa katika Muswada huu, hayana msingi wowote, wala tija kisheria na kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiwezi kuyaafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Muswada unapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11 ya Sheria za Tanzania. Hapa inapendekezwa kwamba maneno "Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo" yafutwe kila yanapoonekana katika Sheria hiyo na badala yake liwekwe neno jipya "Hakimu." Kwa mujibu wa mapendekezo ya marekebisho, neno "Hakimu" litakuwa na maana ya Hakimu wa Wilaya au Hakimu Mkazi, Hakimu wa Kiraia *(Civil Magistrate)* au Hakimu wa Heshima *(Honorary Magistrate).* Maelezo ya Madhumuni na sababu za mapendekezo haya yanataja kuwa marekebisho haya yana kusudio la kufuta sifa za Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ili kuwawezesha Mahakamu Wakazi au Mahakimu wa Wilaya kusikiliza kesi katika Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya ni mfano mwingine wa jinsi ambavyo Serikali hii ya CCM haina tena uwezo wa kutekeleza shughuli za nchi kwa weledi na baada ya tafakari ya kutosha ya masuala ya kitaalamu na kisera. Kwanza, mapendekezo haya yanadhihirisha kwamba Serikali hii na hata Mahakama ya Tanzania, kama mhimili mmojawapo wa dola, haina sera ya raslimali watu *(manpower policy).* Kila Taasisi ya umma na hata za binafsi inayoajiri watumishi wa aina mbalimbali ina sera ya raslimali watu inayoweka vigezo vya elimu, ujuzi au uzoefu kwa ajira katika ngazi mbalimbali za utumishi wa Taasisi hiyo.

Kwa upande wa Mahakama ya Tanzania, sera ya raslimali watu katika utumishi wa kimahakama, siku zote imesisitiza vigezo vya elimu na ujuzi tofauti katika ngazi tofauti za utumishi wa Kimahakama. Hivyo, kwa mfano, watumishi wa Mahakama wanaoteuliwa kuwa Mahakimu wa Mwanzo wanatakiwa kuwa na Cheti cha Sheria *(Certificate in Law)* cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam au Chuo Kikuu cha Mzumbe au Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto. Kwa upande mwingine, watumishi wa Mahakama wanaoteuliwa kuwa Mahakimu wa Wilaya wanatakiwa kuwa na Stashahada ya Sheria *(Diploma in Law).*

Aidha, sifa ya watumishi wanaoteuliwa kuwa Mahakimu Wakazi ni kuwa na Shahada ya Sheria ya Chuo Kikuu kinachotambuliwa na Mamlaka ya Ithibati Tanzania. Vile vile, sifa ya watumishi wa Mahakama kuteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani ya Tanzania inalingana na sifa ya kuteuliwa Hakimu Mkazi, yaani elimu ya Shahada ya Sheria ya Chuo Kikuu kinachotambuliwa na Mamlaka ya Ithibati Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama yatapitishwa na kuwa sheria, mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu yatafuta tofauti za kitaaluma zilizoelezwa hapo juu. Kwa maana hiyo, Mahakimu wa ngazi zote kuanzia Mahakama ya Mwanzo hadi Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Rufani na wa Mahakama Kuu ya Tanzania watakuwa na sifa zinazolingana za kitaaluma. Matokeo au madhara ya kuwa na sifa za kitaaluma zinazolingana ni makubwa na inaelekea hayakufikiriwa kabisa wakati wa kuandaa Muswada huu.

Kwanza, pamoja na ukweli kwamba wamebaki wachache katika mfumo wa Kimahakama, bado kuna Mahakama za Wilaya ambazo ziko chini ya Mahakimu wa Wilaya ambao wana Stashahada za Sheria badala ya Shahada za Sheria. Kwa vile Mamlaka ya Rufaa zinazotoka Mahakama ya Mwanzo ni Mahakama ya Wilaya, wananchi watapata wapi imani kwamba rufaa zao zitasikilizwa kwa haki na watumishi wa Mahakama wenye uwezo kitaaluma kama maamuzi wanayoyakatia rufaa yametolewa na Mahakimu wenye kiwango kikubwa cha elimu kuliko wenye kusikiliza rufaa hizo?

Pili, utendaji katika ngazi mbalimbali za Mahakama ya Tanzania utaathirika kwa sababu watumishi wote kuanzia Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo mpaka Jaji Mkuu watakuwa na sifa zinazolingana kitaaluma. Mfumo mzima wa *hierarchy* ya Kimahakama unaashiria kuwepo kwa tofauti za kitaaluma na kiweledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi ya Mahakama za juu yanaheshimiwa na kufuatwa na Mahakama za chini kwa sababu, pamoja na mambo mengine, ya imani kwamba Watendaji wa Mahakama ya Wilaya au ya Hakimu Mkazi au wa Mahakama Kuu au wa Mahakama ya Rufani wana uwezo mkubwa zaidi kitaaluma kuliko Watendaji wa ngazi za chini yao. Sasa kama sifa za kielimu zitakuwa zinafanana kama inavyopendekezwa na Muswada huu, ni Hakimu gani wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya au ya Hakimu Mkazi atakayeheshimu maamuzi ya Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani ya Tanzania ambaye analingana naye kitaaluma?

Tatu, Mamlaka za Mahakama mbalimbali zinatofautiana kwa kufuatana na maeneo ya kijiografia *(territorial jurisdiction)* au kwa aina za kesi zinazoweza kusikilizwa na Mahakama za kila ngazi au kwa thamani ya mali inayobishaniwa *(pecuniary jurisdiction).* Kwa mfano, kwa mujibu wa kifungu cha 18(1)(a) cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu, kiwango cha thamani ya mali kwa kesi za Mahakama ya Mwanzo ni kati ya Shilingi milioni 10 na Shilingi milioni 12, kiwango hicho kwa kesi za Mahakama ya Wilaya au Hakimu Mkazi ni kati ya Shilingi milioni 100 na Shilingi milioni 120 wakati Mahakama Kuu haina kikomo cha thamani ya mali.

Aidha, ukomo wa mamlaka ya kijiografia ya Mahakama ya Mwanzo ni eneo ambalo Mahakama hiyo iko wakati mamlaka hayo kwa Mahakama ya Wilaya ni eneo la Wilaya iliko Mahakama hiyo. Vile vile kwa Mahakama ya Hakimu Mkazi, mamlaka yake ya kijiografia ni eneo la Mkoa ambako Mahakama hiyo imeanzishwa wakati Mahakama Kuu haina ukomo wa mamlaka ya eneo. Swali la msingi la kujiuliza hapa, ni kwa nini watendaji wenye kiwango kinachofanana cha elimu wafanye kazi ya aina hiyo hiyo katika ngazi tofauti? Je, watalipwa mishahara inayolingana kwa ngazi zote kwa kuwa kiwango chao cha elimu kinalingana? Au watalipwa mishahara tofauti kwa sababu ya ukubwa wa maeneo ya kijiografia ya kazi zao au aina za kesi watakazosikiliza au thamani ya mali itakayokuwa inabishaniwa? Maswali yote haya hayajapatiwa majibu katika mapendekezo ya marekebisho yaliyoko katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kwa mujibu wa kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Mawakili

na waendesha mashtaka wa Serikali wanakatazwa kuwakilisha wadaawa au washtakiwa katika Mahakama za Mwanzo. Hii ni kwa sababu ya kiwango kidogo cha kitaaluma walichonacho Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na wazee wa Mabaraza ambao karibu wote ni wananchi wa kawaida wa maeneo ya vijijini. Endapo yatapitishwa kuwa sheria, mapendekezo ya Muswada huu yataongeza kiwango cha kitaaluma cha Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo kufikia kiwango cha Jaji Mkuu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, wakati Mawakili na waendesha mashtaka wana haki ya kuwakilisha wateja wao katika Mahakama za Wilaya na za Hakimu Mkazi na katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani ya Tanzania, mawakili na waendesha mashtaka hao wataendelea kukatazwa kufanya kazi katika Mahakama za Mwanzo kwa sababu Serikali haijaona umuhimu wa kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imefadhaishwa sana na mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu. Kwa maoni ya Kambi Rasmi, lengo halisi la marekebisho haya ni kujaribu kuhalalisha *ex post facto,* ukiukaji mkubwa wa Sheria hiyo uliofanywa na uongozi wa juu kabisa wa Mahakama ya Tanzania mwezi Septemba, 2012. Kwa mujibu wa taarifa zilizoripotiwa na vyombo mbalimbali vya habari, mnamo tarehe 15 Septemba, 2012 Jaji Mkuu wa Tanzania - Mheshimiwa Mohamed Chande Othman aliwaapisha Mahakimu Wakazi wa Mahakama za Mwanzo wapatao 372 katika sherehe iliyofanyika katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto.

Kwa kadri ya taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo, Mahakimu Wakazi hawa wamekwishatawanywa katika sehemu mbalimbali za Tanzania, lakini wameshindwa kuanza ajira zao mpya kwa sababu ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu haitambui cheo cha Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mwanzo.

Hata hivyo, watumishi hawa wameendelea kulipwa mishahara na stahili nyingine za ajira hiyo pamoja na kwamba hawafanyi kazi yoyote ya Uhakimu waliyoajiriwa kuifanya. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli mbele ya Bunge hili Tukufu, kwa nini imeruhusu kada ya watumishi wasiotambuliwa na sheria za nchi, kuajiriwa na Mahakama ya Tanzania na kulipwa mishahara kwa fedha za umma wakati utumishi wao hautambuliwi na sheria yoyote?

Aidha, Serikali itoe kauli mbele ya Bunge hili Tukufu kama kuna hatua zozote za kinidhamu au za kisheria ambazo zimekwishachukuliwa au zinatazamiwa kuchukuliwa dhidi ya wote waliohusika katika ukiukaji huu wa sheria za nchi? Zaidi ya hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kujua ilikuwaje mpaka Jaji Mkuu wa Tanzania akaenda kubariki uvunjaji huu wa sheria kwa kuapisha watumishi wa Mahakama ya Tanzania ambao nafasi zao hazitambuliwi kisheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuajiriwa na kuapishwa kwa watumishi wa Kimahakama ambao nafasi zao hazitambuliwi kisheria ni mfano mwingine wa wazi wa kukithiri kwa vitendo vya kuajiri watumishi wa Kimahakama katika ngazi zote za Mahakama ya Tanzania bila kujali

masharti ya kikatiba na ya kisheria yanayohusu ajira ya Mahakimu na Majaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani ya Tanzania. Tatizo hili ni kubwa, la muda mrefu na limelalamikiwa mara nyingi na Watendaji wa ngazi za juu wa Mahakama ya Tanzania na hata Serikali yenyewe.

Kwa mfano, mwaka 2005 aliyekuwa Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Bukoba, alihoji Uhalali Kikatiba kwa Majaji Kufanya Kazi kwa Mkataba baada ya kustaafu. Katika taarifa yake kwa aliyekuwa Jaji Kiongozi - Hamisi Msumi, Jaji Bernard Luanda alisema kwamba na ninaomba nimnukuu: "Suala la Majaji kupewa Mikataba, linakwenda kinyume na Katiba". Jaji Luanda alifafanua kwamba, kwa kuwa Jaji amestaafu, basi kiapo chake nacho kimeondoka. Kwa bahati mbaya hawaapishwi ili washike kazi hizo za Ujaji. Ni hoja yangu kwamba Majaji waliostaafu na kupewa Mikataba sio Majaji kwa mujibu wa Katiba." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wa Mheshimiwa Jaji Luanda uliungwa mkono mwaka mmoja baadaye na Jaji wa Rufaa - Mheshimiwa Augustino Ramadhani wakati huo akiwa Kaimu Jaji Mkuu.

Katika mawazo kuhusu vifungu vinavyohusu Mahakama na Majaji aliyomwandikia aliyekuwa Jaji Mkuu – Mheshimiwa Barnabas Samatta na kunakiliwa kwa Majaji wa Rufaa wote, Jaji Ramadhani alisema kwamba, sio sahihi kwa Jaji Mkuu kustaafu na kupewa Mkataba wa kuendelea na wadhifa huo kupindukia umri wa miaka 65, ambao ndiyo umri wa kustaafu kwa lazima kwa Jaji wa Rufaa na Jaji Mkuu.

Kuna ushahidi wa nguvu zaidi juu ya ukiukaji mkubwa wa Katiba kuhusiana na uteuzi wa Majaji. Mnamo tarehe 6 Desemba, 2007, Mkutano kuhusu ajira ya Majaji waliostaafu ulifanyika Ikulu, Dar es Salaam chini ya Uenyekiti wa Katibu Mkuu Kiongozi wakati huo Philemon Luhanjo. Wajumbe wengine walikuwa pamoja na Mwanasheria Mkuu - Johnson Mwanyika; Naibu wake, Sazi Salula; Katibu Mkuu (Utumishi) - George Yambesi, Msajili wa Mahakama ya Rufani - Sophia Wambura na Susan Mlawi wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kumbukumbu za Mkutano huo, kwa utaratibu unaotumika sasa, baadhi ya Majaji wanaofikisha umri wa kustaafu kwa mujibu wa Ibara ya 110(1) kwa Majaji wa Mahakama Kuu na Ibara ya 120(1) ya Katiba wanaongezewa muda wa kuendelea na Utumishi wao kwa Mkataba, baada ya wao kuwasilisha maombi rasmi. Baada ya mjadala juu ya jambo hilo, Wajumbe wa Mkutano walikubaliana kwamba, utaratibu wa kuongeza muda kwa njia ya Mkataba unakiuka masharti ya Katiba na kuleta mkanganyiko kama Majaji hao wanastahili kulipwa mshahara au pensheni au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya Mkutano wa Ikulu ilikuwa ni kuundwa kwa Kikundi Kazi kwa ajili ya kuchambua na kushauri kuhusu ajira ya Majaji baada ya kustaafu chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kikundi Kazi hicho kiliwasilisha taarifa yake tarehe 7 Machi, 2008. Katika taarifa yake, Kikundi Kazi kinakubaliana na msimamo wa kikatiba kwamba, kwa kuzingatia Ibara za 110 na 120 za Katiba, inaonekana wazi kuwa suala la ajira za Mikataba kwa Majaji ambao wamekuwa wakifanya kazi

za Jaji baada ya kufikia umri wa kustaafu ni kinyume cha Katiba.

Kwa mujibu wa Taarifa hiyo, hadi mwezi Machi 2008, walikuwepo Majaji wawili wa Mahakama ya Rufani na Majaji tisa wa Mahakama Kuu, ambao wapo katika ajira za Mkataba, na Jaji mmoja wa Mahakama Kuu aliyeongezewa muda wa ajira kwa mujibu wa masharti ya Katiba. Hii ina maana kwamba, kulikuwa na Majaji 11 ambao walikuwa wanafanya kazi kinyume na Katiba na kwa maneno ya Jaji wa Rufaa, Luanda, hawakuwa Majaji kwa mujibu wa Katiba. Aidha, kwa mujibu wa ushahidi wa nyaraka hizi, kulikuwa na Jaji mmoja tu ambaye alikuwa ameongezewa muda wa ajira ya Ujaji kwa mujibu wa Katiba. Katika mapendekezo yake, Kikundi Kazi hakikuficha msimamo wake juu ya uhalali wa ajira hizo za Majaji.

"Mikataba iliyopo hivi sasa iko kinyume cha Katiba. Hii ina maana kwamba Majaji hao wanafanya kazi ya Jaji kinyume cha Katiba, hivyo kazi zote ambazo wamezifanya na wanaendelea kuzifanya wakiwa chini ya ajira mpya za Mikataba, hazina uhalali wowote kisheria. Kazi hizo ni sawa kama vile zimefanywa na mtumishi mwingine yeyote asiye na madaraka ya Jaji. Hivyo basi, Rais ashauriwe kuifuta Mikataba hiyo mara moja kwa vile ina madhara makubwa kwa jamii na katika uteuzi wa Majaji wapya kuchukua nafasi zao. Majaji waliofutiwa Mikataba waendelee na pensheni zao kama kawaida." Mwisho wa nukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka minne imepita tangu Kikundi Kazi kiwasilishe mapendekezo yake Ikulu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli, kwa

nini Serikali hii ya CCM imeendekeza vitendo vya uvunjaji Katiba katika uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Tanzania?

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli mbele ya Bunge hili Tukufu kama mapendekezo ya Kikosi Kazi cha Ikulu yalitekelezwa na ni Majaji gani wa Mkataba ambao ajira zao zilisitishwa kama ilivyopendekezwa. Vile vile, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilihakikishie Bunge hili Tukufu kama bado wapo Majaji ambao bado wameajiriwa kwa Mkataba kinyume cha Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya yanathibitisha kwamba mapendekezo ya Muswada huu hayajafanyiwa tafakari ya kutosha licha ya madhara makubwa yanayoweza kutokana na mapendekezo haya kupitishwa. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiwezi kuyaafiki mapendekezo haya ya marekebisho ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada unapendekeza marekebisho ya *Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 ya Sheria za Tanzania*. Mapendekezo haya yanafuta tafsiri ya neno 'Divisheni ya Ardhi ya Mahakama Kuu ya Tanzania' na badala yake kuweka maneno 'Mahakama Kuu.' Kwa mujibu wa maelezo ya Madhumuni na Sababu za Muswada, mapendekezo haya yanalenga kuipa mamlaka Mahakama Kuu ya Tanzania kusikiliza kesi za ardhi badala ya Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi pekee. Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, lengo la marekebisho haya ni kuifuta kabisa Divisheni ya Ardhi ya Mahakama Kuu ya Tanzania na hivyo kurudisha mamlaka ya Mahakama Kuu kutatua migogoro ya ardhi kama ilivyokuwa kabla ya

kutungwa kwa Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 ya Sheria za Tanzania iliyotungwa mwaka 2001. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono mapendekezo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani chini ya Uongozi wa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman A. Mbowe kwa ushauri na ushirikiano uliowezesha maandalizi ya hoja hii. Vile vile nichukue fursa hii kuwashukuru Wasaidizi wa Kambi Rasmi ya Upinzani – Mkurugenzi wa Masuala ya Bunge na Halmashauri John Mrema, Msaidizi wa Masuala ya Kibunge Oliver Mwikila na timu yao ya watafiti ikiongozwa na Mratibu wa Shughuli za Kambi – Ndugu Zubeda Sakuru, Ndugu Onesphory Mbuya na Ndugu Emmanuel Masonga, kwa msaada na ushauri wa kitaalam uliofanikisha maandalizi ya hoja hii.

Mwisho naomba nichukue fursa hii kuwashukuru viongozi, wanachama na wapenzi Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wananchi wote wa Tanzania ambao wameendelea kutuunga mkono na kututia nguvu katika kipindi hiki muhimu katika historia ya nchi yetu. Msimamo wetu ni ule ule, “Hakuna kulala mpaka kieleweke!”

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba yale ambayo sijayakamilisha yaingie katika rekodi rasmi ya Bunge. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendea na mjadala. Tunaanza kwa mujibu wa orodha niliyokabidhiwa, mtu wa kwanza ameomba udhuru. Tunaingia mtu wa pili, Mheshimiwa Halima Mdee, kama hayupo Mheshimiwa Peter Msigwa, naye kama hayupo namwita Mheshimiwa Pindi Chana.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii adimu kwa mara nyingine tena kuchangia Muswada huu unaohusu Marekebisho ya Sheria Mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na niseme tu kwamba kwa kweli umekuja kwa muda mwafaka. Kwa hiyo, napongeza sana Ofisi ya *Attorney General* kwa kutuletea Muswada huu. Nitaanza moja kwa moja ndani ya Muswada, sehemu ya pili inayohusu *Anti Money Laundering.* Kwa kweli marekebisho haya yaliyoletwa ninayaunga mkono, ila tu ningeomba kushauri kwamba, neno "*financing"* liwe miongoni mwa tafsiri ambazo zimo katika *Terrorist Act*, *otherwise* maoni yaliyoko hapa ninayaunga mkono.

Nikienda sehemu ya tatu ya Muswada, naunga mkono marekebisho ambapo yanahusu *Anti Trafficking in Person* na ushauri wangu ni kwamba, sasa hivi masuala ya *Anti Trafficking in Person* yanafanyika kwa namna mbalimbali. Kwa hiyo, wakati umefika sasa kuangalia maendeleo

ambayo yamefikiwa ambayo yanatumika katika *Anti Trafficking in Person.* Haya yaliyopo nayaunga mkono, lakini sambamba na kuunga mkono, natoa ushauri kwa sababu sasa hivi *Anti Trafficking* inafanyika kwenye *email*, kwenye *website*, watu wanatafutiwa *passport* wanapelekwa maeneo mbalimbali wanaambiwa kuna kazi, lakini ni *Anti Trafficking.*

Kwa hiyo, ningeomba sana masuala ya *Digital* yaangaliwe katika utaratibu huu wa *Anti Trafficking in Person.* Kwa hiyo, hayo ni mambo ambayo ningeomba sana maana yake kumekuwa na tatizo kubwa sana la ajira. Sasa ili vijana wetu wapate ajira, unakuta kunakuwa na *agent* ambaye anafanya *Trafficking in Person* akiwaahidi watoto wetu, hususan wa kike kwamba kuna ajira maeneo mbalimbali, lakini itakuwa ni *Trafficking in Person.*

Kwa hiyo, masuala haya lazima tuyaangalie sana na wakati mwingine wanachukuliwa hata kupelekwa katika nchi za nje. Kwa hiyo, naomba sana *Trafficking in Person* tuiangalie maana yake kadri maendeleo yanavyozidi kwenda na utaratibu huu wa kusafirisha wanadamu ambao huko nyuma ulikuwa unafanana ya utumwa, unafanyika katika utaratibu wa kidigitali. Kwa hiyo, tuangalie sana masuala haya kwa maslahi ya vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja nakwenda sehemu ya nne, ambapo inaondoa neno *Primary Court Magistrate* na kuweka neno "*Magistrate"*, marekebisho haya nayaunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Kwa maana hivi sasa pia tumekubaliana sasa kwamba hata Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wawe wakati

mwingine wana *degree* na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilipokwenda kutembelea na tulipata taarifa kwamba kuna Mahakimu wameajiriwa na wanaendelea kuajiriwa wenye shahada ya kwanza ambao pia watatumika Mahakama za Mwanzo. Haya ni maendeleo ya hali ya juu na ni wakati muafaka kutumia vijana wenye *degree* Mahakama za Mwanzo.

Kwa hiyo, marekebisho haya ambayo yameletwa, tuondoe neno *"Primary Court Magistrate"* na kubakiza neno *"Magistrate"* kwa kweli yanafaa sana na ningeomba Bunge hili tuyaunge mkono. *(Makofi)*

Vilevile, tukienda katika sehemu ya tano, kwa mujibu wa Muswada huu wa Marekebisho inaondoa neno "*Land Division of the High Court"* na kuweka neno "*High Courts*," marekebisho haya yanafaa. Tuna kesi nyingi sana za masuala ya ardhi, sasa kama kesi hizi za masuala ya ardhi tukisema zitashughulikiwa na *Land Divisions* za *High Court* peke yake, hizi *Land Divisions za High Court* hatunazo nyingi nchini, ziko chache, lakini *High Courts* ziko nyingi. Kwa hiyo, tukiruhusu *High Courts* kushughulikia masuala ya ardhi, itasaidia sana *backlog* ambayo tumekuwa tukiizungumzia muda mrefu, kwamba kuna kesi nyingi zinashindwa kumalizika. Kwa sababu wataalam walikuwa wametushauri kwamba masuala ya ardhi yawe yanashughulikiwa katika utaratibu wa Mahakama za Ardhi. Kumbe Mahakama za ardhi ukifikia *High Courts* ziko chache.

Kwa hiyo, migogoro ya ardhi tunayo mingi sana. Sasa ukisubiri Mahakama za Ardhi peke yake ndizo ambazo zishughulikie masuala ya kesi za ardhi, kwa kweli wananchi wanasubiri na bila kutenda haki kwa haraka, mwisho

inakuwa kama ni kero. Kwa hiyo, ni sahihi kabisa kwamba masuala ya kesi za ardhi wakati mwingine yashughulikiwe na Mahakama kuu za kawaida, lakini ni masuala ya ardhi. Kwa hiyo, ni safi kabisa kuondoa neno “*Land Division of the High Court”* na kubakiza neno “*High Courts”* pale tunakuwa tuna wataalam pia wa masuala ya ardhi. Sambamba na hilo, naungana na marekebisho ya sehemu ya sita.

Vile vile naungana na sehemu ya saba na marekebisho ambayo yapo sehemu ya nane, nianze na yale ya sehemu ya saba ambapo tumebadili, umri wa kustaafu kwa nafasi za *Warder* na *Wardress,* kutoka umri wa kustaafu sasa utakuwa ni miaka 40 kustaafu kwa kawaida na kustaafu kwa lazima miaka 45.

Hapa ningeomba badala ya kuwa miaka 40 na 45 kama ilvyoshauriwa, iwe 50 na 55. Hiyo ni sehemu ya saba. Kwa hiyo, nashauri badala ya kufanya 40 na 45 iwe ni miaka 40 na 45, kwa sababu umri wa miaka 40 kustaafu au 45, kwa kweli Watanzania wanakuwa bado wana nguvu, wana uwezo wa kufanya kazi, wana uwezo wa kuhimili mikiki mikiki. *(Makofi)*

Hususani taaluma hizi za kijeshi na kipolisi, kwa hiyo, umri huo kwa kweli bado ni mdogo. Kwa hiyo, wastaafu miaka 50 na 55, kwa hiyo, hapo ningeomba kufanya marekebisho. Maana hapa inasema: “*in case of rank of a warder or wardress, the age of voluntary retirement shall be 45 years and compulsory age of retirement shall be 50 years.* Pale iwe *50 and 55.*

Moja kwa moja nakwenda katika marekebisho yanayohusu Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji. Naunga mkono

marekebisho yaliyopo sehemu ya nane. Baada ya kuunga mkono marekebisho haya natoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji. Mabaraza haya ya Ardhi ya Vijiji, yapo chini ya Wizara ya Ardhi, lakini chombo cha kutoa haki nchini Tanzania kwa mujibu wa Katiba ni Mahakama.

Kwa hiyo, Mabaraza haya ya Ardhi ya kule Vijijini, kuna migogoro ya mashamba, ardhi ya kijiji wameingiliana na wananchi, shamba, mtu na mtu, kampuni na kampuni, badala ya kuwa chini ya Wizara ya Ardhi, yawe chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, maana ndiyo Wizara ambayo ina vyombo kama Mahakama ya kutoa haki, lakini siyo Wizara ya Ardhi! Lakini pia kuna swali, Mabaraza haya ya Ardhi yamekuwa hayatengewi pesa ya kuweza kutumia.

Kwa hiyo, kinachotokea, mtu mwenye mgogoro wa ardhi akienda kwenye kwenye Baraza la Ardhi anaambiwa basi ulipe, ulete mashahidi, yeye mwenyewe kwa sababu hayajapangiwa mafungu, na hivyo inakuwa ni vyanzo vya kutotenda haki.

Wale wanaokaa kusimamia kesi za ardhi za vijiji, hawana mafungu. Halmashauri za Wilaya hazisogei katika Mabaraza hayo ya Ardhi. Kwa hiyo, shughuli zinakwenda tu. Kwa hiyo, kero za ardhi ziko nyingi sana na wanapokuwa wana hizi kesi za ardhi, wakienda katika mhimili wa Mahakama wanaambiwa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji hayako chini ya mhimili wa Mahakama au Wizara ya Katiba na Sheria.

Kwa hiyo, haya ni marekebisho ambayo nayapendekeza naomba yaingie vizuri sana kwenye *Hansard* na mimi nayasubiri wakati wa bajeti. Wakati wa bajeti Kamati ya Katiba na Sheria tutakuwa macho sana kuona huu ushauri tumeutoa zaidi ya mara tatu, kwamba haya Mabaraza, vyombo vya kutenda haki kwa mujibu wa Katiba ni Mahakama, ndiyo mhimili. Sasa Wizara ya Ardhi na kero za ardhi, inakuwa changamoto kweli! Kesi za ardhi ni nyingi sana. Kwa hiyo, tungeomba hizo *Reforms* zifanyike mapema sana, kama hapa tunavyosema *Land Division* iwe *substituted* na *High Court*, vivyo hivyo Mabaraza haya ya Ardhi yaangaliwe ni namna gani yatakuwa chini ya mhimili wa Mahakama tena kwa haraka. *(Makofi)*

Eneo la pili linahusu pia *Ward Tribunal.* Haya ni Mabaraza ya Kata. Kwa hiyo, kunapokuwa na migogoro, ngazi ya Serikali ya Mitaa, chombo cha kwanza kabla ya kufika kwenye Mahakama ya Mwanzo, wanakwenda kwenye Mabaraza ya Kata, *Ward Tribunal*.

Vivyo hivyo, naungana na haya marekebisho ambayo yameletwa hapa, lakini sambamba na marekebisho haya, natoa ushauri unaofanana na Mabaraza ya Ardhi. Mabaraza haya ya Kata, mimi nina maswali, fedha za kufanya kazi, kuendeshea, kununua *file*, karatasi, *stationary* zinatengwa wapi? Sisi Kamati ya Katiba na Sheria, huwa hatuzipitishi. Kwa hiyo, ni Mabaraza ambayo kwa kweli tunakuwa kama tumeyaachaacha.

Kwa hiyo, ni muhimu sana tukaweka jicho na kuwalipa watu kama *Assessors,* wale Wazee wa Mabaraza, lakini tukiacha bila kuwapangia mafungu, kuwapa mafunzo, kuwaelekeza namna gani haki inatendeka, matokeo yake

yule anayelipa zaidi, akienda pale kushitaki ndiye ambaye atasikilizwa kwa umakini zaidi. Kwa hiyo, jambo hili lazima tuliangalie. Lakini naunga mkono kwa asilimia 100 marekebisho haya. Naomba ushauri ambao nimeutoa uangaliwe na wakati wa kupitisha bajeti sasa tutakuwa makini kuona kama haya maboresho ambayo tumekuwa tukishauri mara kwa mara yametekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kusimama leo hapa nikawa na afya nzuri. Nilikuwa naumwa na hivi sasa nimeshapona.

Pili, nampongeza Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Fedha na Uchumi katika kuijadili hii na mimi nilikuwepo na tulijadili pamoja. Hata hivyo, siendi kinyume na Mwenyekiti wangu wa Fedha na Uchumi lakini nina maelezo kidogo tu, nataka niyazidishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye Sheria ya Ardhi. Mahakama Kuu ya Kitengo cha Ardhi ndiyo iliyokuwa ikisikiliza migogoro ya ardhi, lakini sasa imehamishwa kupelekwa *High Court*. Sipingani naye sana, lakini nataka nipate maelezo tu kwamba je, hii migogoro ya ardhi itapungua? Je, Kitengo kilikuwa na Majaji wangapi na sasa watakuwepo Majaji wangapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye Sheria za Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu. Hili ni jambo zito na kubwa sana. Kuna wengine wanasafirishwa lakini wakifika nje wanakuta mazingira siyo mabaya sana, lakini kuna wengine huko nje hufanyishwa kazi ambapo mwanadamu yeyote hastahiki kufanya. Nakubaliana nayo hii ya kusema kuwa hizi kesi zianze kusikilizwa na Mahakama ya Mwanzo, lakini kwa yale masuala mazito, nachelea kuanza kusikilizwa kwenye Mahakama ya Mwanzo.

Kwa hiyo, naiomba Serikali kwa haya masuala mazito ya kuchukuliwa binadamu, wakienda nje ya nchi wakafanyishwa kazi ambazo hazistahiki kufanywa na binadamu, na sote tunazijua na nyingine ni matusi siwezi kuyasema hapa. Kwa hiyo, naomba kwa masuala haya yawe yanasikilizwa na *High Court* moja kwa moja.

Jambo lingine ni kuhusu umri wa kustaafu kwa Askari Magereza. Umri wa kustaafu kwa Askari Magereza umeongezwa kutoka miaka 50 mpaka 55 kwa lazima. Kuna Maafisa wengine wamepewa muda wa miaka mitano, wanaweza kuzidisha.

Sasa hapa nina swali dogo ambalo nataka kuuliza kwamba: Je, katika kuzidisha hawa, mnatazama kile cheo na afya ya mtu, au inakuwaje? Kwa nini isiwe kwa kila anayeweza akaweza kuongezewa muda wa miaka mitano? Halafu: Je, haya mafao yake analipwa baada ya miaka 55 na ile miaka mitano mingine inakuwa kwenye Mkataba au halipwi mafao yake mpaka atimize miaka 60?

Jambo la mwisho ambalo ni dogo tu la kuhusu mabadiliko ya Sheria Ukaguzi wa Hesabu. Mimi nakubaliana

nalo moja kwa moja, lakini muda. Naomba katika kukusanya, Serikali na Mkaguzi wa Serikali wahakikishe yanafika Ofisi ya Bunge kwa wakati muafaka na pia Kamati za *Oversight Committee* wapatiwe kwa haraka ili wapate kuzijadili kwa haraka na wazilete Bungeni zikiwa zimejadiliwa vizuri sana. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, nasema naunga mkono hoja mia chini ya mia.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Amour. Sasa namwita Mheshimiwa Shekifu.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nakushukuru kwa kunipa nafsi na nitamke mwanzoni kabisa kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu. Kama tulivyoambiwa kwenye *briefing*, nilikuwa na hitilafu katika afya nikaenda kupimwa na inaonekana afya yangu ni timamu, kwa hiyo naendelea na kazi vizuri.

Vilevile naomba kutangaza hapa kwamba namshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Tanga, kwa hiyo, mtu anapoitaja CCM bila utaratibu, napata uchungu sana. Mimi naamini Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya kazi vizuri na asiyeona ukweli huo ni juu yake, lakini aliye na macho haambiwi tazama na aliye na masikio halazimishwi kusikia. Lakini niombe tu kwamba busara zitawale katika kuona ukweli. Haiwezekani katika mapendekezo haya basi yote hayafai. Mimi nafikiri busara

zitumike tu kwamba kuna yanayofaa na mengine ni kushauri ili yawe mazuri zaidi. Hizi ndiyo busara za kupinga na ndiyo busara za kutoa ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, nakubaliana na hoja zote na pengine nitakayochangia zaidi ni mapendekezo. Nakubaliana kabisa na suala hili la uhamishaji fedha haramu. Mapendekezo yaliyoletwa ni kusisitiza, pengine kitu muhimu ni kuongeza kasi na kutoa maamuzi haraka ya kesi zinazohusiana na fedha hizi haramau. *(Makofi)*

Pili, suala la kuzuia usafirishaji wa binadamu, hakuna binadamu aliye na akili kweli anayepinga kwamba matendo ya kumdhalilisha binadamu mwenzako ni tendo la dhambi na dhamira yako wewe mwenyewe. Kwa hiyo, katika Serikali kuleta mapendekezo ya kuimarisha sehemu hii, ni busara kubwa. Mimi ninachopendekeza ni kwamba hebu tuangalie chimbuko la tatizo hili ni nini? Kwa nini watu wamefikia mahali ambapo anakwenda kufanya biashara ambazo ni haramu? Mimi naamini ajira ni tatizo kubwa. Watu wameamua kwenda katika maeneo ya hatari kwa kuhatarisha maisha yao. Leo asubuhi nikasikia na Lushoto nako wanasafirishwa. Nilisikitika sana! Sikuamini! Lakini kwa ugumu wa maisha watu wanafika hapo. Kwa hiyo, juhudi za Serikali katika kutafuta ajira kwa vijana ziimarishwe. Huo ndiyo ushauri wangu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuhusu masuala yanayohusiana na Mahakama kupewa mamlaka katika ngazi zote na mabadiliko ya sheria ile ya Mahakimu, mimi naunga mkono. Nashangaa sana mtu anapouliza kwamba Mahakimu watafanana elimu yao ya msingi; ama! Jaji

Mkuu anaweza kuwa na *degree* ya kwanza na Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo anaweza kuwa na *degree* ya kwanza.

Kinachohitajika hapa ni utambuzi na hekima. Huyo Jaji Mkuu ataangaliwa kwa uamuzi na uzoefu wake na hekima alizonazo. Hapa pa kuingilia ni daraja tu, lakini nia nzuri ni kwamba vijana hawa wanachukuliwa kwa kuanzia mwanzoni kwa sababu tunaamini mtu akishakuwa na Shahada ya kwanza, atakuwa na uelewa wa kasi zaidi na uelewa mkubwa. Hiyo ndiyo mantiki yake tu. Sasa kama Serikali iliwachukua hao vijana wakaenda wakakaa na sasa inarekebisha ili waajiriwe, kosa lipo wapi? Mbona mtu unatafuta kazi na unafanya vibarua? Sasa leo tukifanya kibarua kikawa halali ni kosa? Mimi naamini kilichovunjwa kama ni kuvunjwa ni kwa nia nzuri na hakuna kitu kilichovunjwa. Kwa hiyo, mimi nakubaliana na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine nijielekeze katika kifungu cha (8) na (9). Kifungu cha (8) kinazungumzia zaidi masuala ya kusimamia umiliki wa ardhi vijijini. Ni ukweli kwamba sheria ile imebadilika kuwapa mamlaka Mahakimu wa Mahakama zote. Lakini nisisitize tu kwamba tatizo kubwa linaanzia hata kama huku juu utawapa Mahakimu wengi au Mahakama Kuu isikilize matatizo ya ardhi. Kama hutajenga msingi huku chini ambao una nguvu, bado haki haitatendeka. Kule vijijini kwa sasa Mabaraza ya Kata na hata Mabaraza ya Vijiji bado hayajatenda haki. Kwa hiyo, utakuta haki inapopotoshwa pale, hata kuja kuitoa huku juu ni kazi kubwa sana kwa sababu Mahakama Kuu haziendi kule vijijini, wanasikiliza maandiko yaliyofanywa na Mahakama za chini. Sasa mimi nina mfano mzuri. Lushoto,

mwananchi amenyang’anywa haki yake kesi imepelekwa Mahakama Kuu, inachukua muda mrefu na inakuja inaamuliwa kinyume na haki iliyopo katika eneo. Sasa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata yamewekwa ili yaweze kutekeleza haki, lakini siyo yanayotendeka.

Kwa hiyo, naomba sana katika hili, Wizara ya Ardhi ambayo mimi nakubaliana na Mheshimiwa Pindi Chana kwamba ni ukweli kwamba ili tutende haki nafikiri chombo kimoja kishughulikie tatizo la haki, maana hao Mahakimu wa chini, wenzetu, ambao lipo tatizo la elimu yao; kwa mfano, Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, Wajumbe, elimu yao ni ndogo sana. Wanapopotosha haki pale kwenda kuijenga huku juu inakuwa ni kazi ngumu sana. Ukienda kwenye Kata, nao pale kweli wale ni Wanasheria walioajiriwa kwenye Mabaraza ya Kata, lakini wengi wa wale ni watu ambao hawana uzoefu katika kesi hizi. Matokeo yake, hukumu zinazofanyika kwa kweli wakati mwingine unajiuliza kwamba sasa huyu mtu haki yake iko wapi?

Kwa hiyo, nafikiri, kwa sababu uanzishaji wa kesi na utenguaji wake badala ya kuhama kwenda Mahakama Kuu, ni vyema Watendaji wote wawe katika eneo moja, yaani wawe chini ya Wizara ya Sheria, chini ya Mahakama Kuu. Mimi nafikiri hapo tutatenda haki.

Napendekeza pia kwamba ili uteuzi ufanyike, hawa Wajumbe wa Mabaraza katika ngazi ya Kijiji, elimu izingatiwe. Kuna umuhimu kutamka wazi kwamba angalau kima cha chini cha elimu kiwe ni Darasa la 12 kwa sababu uelewa utakuwa mkubwa hata kusoma nyaraka itakuwa rahisi na hata utoaji wa hukumu na ushauri unapotolewa

unaonekana unazingatia kiwango fulani cha uelewa. Kwa hiyo, hata hizi Mahakama za juu hazitapata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba sana, pia waimarishwe katika kupata haki zao au posho zao. Sasa hivi Mahakama hizi za Kata na Vijiji wale wanaosimamia kwa kweli hawapati posho na haijulikani hizo posho ziko wapi.

Kwa hiyo, Serikali ingetamka hapa kwamba posho za hawa Wajumbe wa Kamati za Ardhi za Vijiji ziko wapi? Vile vile Hili Baraza la Kata posho zao zipo wapi? Maana kama mtu hajamotishwa siku zote atakwenda kupotoka. Rushwa zinatafutwa kwa sababu watu hawa hawalipwi. Lakini watawajibishwa kama wanalipwa na tutawawajibisha kwa haki kama tumewalipa. Sasa mtu anakufanyia kazi yako humlipi mshahara, unategemea aifanye kwa ufanisi? Siyo rahisi!

Ushauri wangu ni kwamba fedha zitafutwe katika maeneo haya ya kutenda haki, watu walipwe vizuri; siyo kwa Wazee wa Baraza tu lakini kwa kweli watu wote, Mahakimu na hata Majaji Wakuu walipwe vizuri na hata Wajumbe wa Kamati hizi walipwe vizuri ndiyo mtaona haki inatendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashauri na ninaomba sana Serikali, nakubaliana nayo katika mabadiliko haya. Mabadiliko haya yanakuja juu, lakini chini bado hayajazingatiwa.

Kwa hiyo, haki za kuteua Wajumbe wenye uwezo katika ngazi za Vijiji ni lazima ichukuliwe. Wizara ya Katiba

na Sheria ichukue madaraka sasa ya kusimamia haki kuanzia chini mpaka juu.

Tatu ni kuhusu maslahi ya viongozi wanaowatendea watu haki yaangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, naunga mkono hoja na ninaomba sana tutambue kwamba Serikali yetu inafanya kazi vizuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Shekifu. Sasa namwita Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache katika Muswada huu uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nisisitize yale ambayo yaliweza kusemwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba Muswada huu umefanyiwa zimamoto na inaonyesha kwamba hata Kamati yenyewe haikupata nafasi ya kuucheki vizuri na hii inatokana na hali halisi ambayo tunaona Bunge linayumba, yale mambo ya msingi kama hoja binafsi yanawekwa pembeni lakini sasa mambo yanaletwa kwa zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie mambo mawili katika Muswada huu. Naamini Kanuni zile ambazo zimetajwa kwamba zimekiukwa zitaangaliwa na wakati mwingine haya mambo yasijirudie.

Jambo la kwanza ni kuhusu suala zima la hesabu za Mkaguzi Mkuu kuweza kujadiliwa na Bunge hili. Hili jambo ni

la msingi. Kimsingi tunaona kwamba limechelewa kwa sababu Mkaguzi Mkuu anapokuwa amefanya ukaguzi katika hesabu za Mashirika mbalimbali na katika hesabu za Halmashauri zetu, ni vizuri Bunge likajadili hesabu hizi na tukaona ni wapi ambapo fedha za Serikali hazitumiki vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, nisisitize kwamba kumekuwa na utamaduni wa Bunge hili kujadili masuala ya msingi kwa zimamoto au muda kutengwa mdogo sana. Hili la Mkaguzi wa Hesabu za Serikali leo linapita katika Muswada huu. Naomba sasa ratiba ya Bunge iangalie kwa upana wake endapo hesabu hizo zitaletwa, basi muda wa kutosha utengwe kwa ajili ya kujadili hesabu hizo kwa sababu ni hesabu nyingi na pia Wabunge wanatakiwa waangalie kwa makini ni mambo gani yanafanyika katika mashirika mbalimbali katika Halmashauri zao. Isiwe inaletwa hesabu hapa, tunatengewa siku mbili au moja tukajadili hesabu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ratiba izingatiwe na Wabunge wapewe muda wa kutosha na waangalie hata ikibidi wiki moja tujadili hesabu hizo kwa sababu kuna madudu mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la Hesabu za Mkaguzi Mkuu, mimi naomba nisisitize kwamba hata utaratibu ambao unatumika, uangaliwe sasa katika Halmashauri zetu, hesabu hizo zinajadiliwa katika wakati gani? Katika Halmashauri nyingi Madiwani wengi hawafahamu, ukiachilia Bunge hili kwamba sasa linakuja kwetu, tunakwenda kupanga kwa upya kwamba ni jinsi gani tunajadili hizi hesabu.

Nitoe mfano. Katika Halmashauri mbalimbali, Mkuu wa Mkoa anaweza akaitisha sasa Baraza la Madiwani wakati kisheria hatakiwi. Anaitisha Baraza hilo likajadili hesabu hizo labda za Halmashauri husika, lakini cha kusikitisha katika hesabu hizi wale Watendaji wa Halmashauri wengi wao hawajui jinsi gani ya kujibu *queries* za Mkaguzi Mkuu. Unaweza ukafika kwenye kikao ambacho kinashikiliwa na Mkuu wa Mkoa ambaye kisheria haruhusiwi kushikilia kile kikao au kuongoza kile kikao lakini ukasikia, Baraza la Madiwani sasa mtoe majibu ya hizo hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalisema kwa sababu nimelikuta katika Halmashauri yangu. Inasikitisha sana pale ambapo Watendaji wa Halmashauri wamepewa dhamana ya kusimamia zile fedha. Fedha zimetoka Serikali Kuu, zimefikishwa kwenye ngazi za Halmashauri, halafu Madiwani ambao mnatakiwa msimamie watendaji wale ambao wametumia zile fedha vibaya mnaambiwa kwamba sasa ninyi mtoe majibu ya zile fedha ambazo zimetumika vibaya.

Kwa hiyo, natoa tahadhari kwamba pamoja na kwamba Bunge tunatakiwa tujadili hizi hesabu, hebu huu mfumo mzima uangaliwe mpaka ngazi za chini mpaka ngazi ya Mabaraza ya Madiwani kwamba ni jinsi gani zile hesabu zinatakiwa zisimamiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la Wakuu wa Mikoa pia liangaliwe kwa sababu wao kuwa Wakuu wa Mikoa, sheria hairuhusu kuweza kusimamia au ku-*chair* nafasi za Wenyeviti wa Halmashauri. Kama wanafanya hivyo, naamini mwongozo utatoka wasiweze kufanya vitu kama hivyo ambavyo kisheria vimekatazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la wale ambao wametumia fedha vibaya ni adhabu zipi zinatolewa? Nimeona kwamba ni barua nyingi za onyo wanapewa, utakuta kwamba mtu ameambiwa asimamie ukusanyaji wa ruzuku fulani katika ngazi fulani au katika ngazi ya Halmashauri, utakuta vitabu vimepotea, lakini Mkurugenzi anasema kwamba huyu mtu amepewa onyo, onyo anapewa mara ngapi? Lakini hatuoni kama wanachukuliwa hatua kinidhamu zaidi ya onyo wakati fedha nyingi za walipa kodi zinapotea katika hizo ngazi, lakini wanaishia kupeana barua za onyo ambazo hazina tija kwa wananchi ambao wanalipa kodi.

Kwa hiyo, nisisitize kwamba suala zima la kuwachukulia hatua hawa watu ambao wanatumia vibaya hizi raslimali au kodi za wananchi, hili suala zima liangaliwe kwa upya kwani haiwezekani wananchi wanavuja jasho, wanalipa kodi lakini kuna kikundi fulani cha watu au Watendaji wanatumia hizo fedha vibaya kwa maslahi yao na siyo maslahi ya kitaifa, lakini pia wanaishia kupeana onyo au kuhamishana *department*, anahamishwa kutoka nafasi hii anapelekwa nafasi nyingine. Naomba utaratibu huu pia uweze kukaziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala zima la Mahakama ya Mwanzo au kada hizi kwenda kufutwa kupitia Muswada huu. Mimi kwanza nilisikitika kuona hili.

Nilikuwa nikijiuliza kwamba katika utumishi wa nchi hii sijawahi kuona popote kwamba *qualification* ya chini inatakiwa *degree*. Hii ndiyo ya kwanza tunaisikia. Kwa nafasi zozote zile kuna *job specification*, kuna *job description* kwamba kuna wale wa chini ambao ni *messengers*, kuna

*supporting staff*. Lakini katika kada hii ya Mahakama Muswada huu leo unapendekeza kwamba wale Mahakimu wenye Diploma na wale wenye *certificate* waanze kujisomesha kwa sababu hizo nafasi sasa hazitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najiuliza, hata walimu ambao wanafundisha hawa Mahakimu mpaka sasa kuna *Certificate,* tunazo; mpaka sasa tuna Diploma za Ualimu, mpaka sasa tuna *degree* za Ualimu. Hebu Mwanasheria Mkuu aje atuambie ni kwanini amekwenda ku-*focus* tu ngazi ya Mahakama eti Mahakimu wenye Diploma hawatakiwi, wenye C*ertificate* hawatakiwi na Mahakama ya Mwanzo inakwenda kufutwa. Tunatoa ujumbe gani kwa watumishi wa Serikali wa Tanzania ambao wako kwenye nafasi hizi za Mahakama? Ni muda gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Muswada ukaeleza kwamba ni muda gani sasa hizi nafasi zinakwenda kukoma? Kwa sababu hata Chuo hiki ambacho tunacho pale Lushoto cha Uongozi wa Mahakama, sasa hivi tunaongea kuna wanafunzi wanasoma huko. Tunawapa ujumbe gani hao wanafunzi na hasa tukizingatia mfumo wa elimu nchini mwetu? Ni wiki iliyopita tu tulikuwa tunajadili mitaala ya elimu jinsi ambavyo haieleweki. Lakini leo tunakuja na hili tunasema tunakwenda kuondoa hizi nafasi, wakati kuna watu ambao tunafahamu kwamba wanafanya kazi nzuri kwenye ngazi hizo za Mahakama, lakini kuna Mahakimu ambao kesi zimelundikana, mazingira yanafanya washindwe kuwa *efficiency* katika kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea Serikali ingeangalia mfumo mzima wa utendaji katika Mahakama zetu. Tatizo siyo elimu, tatizo siyo Diploma, tatizo siyo

*certificate!* Hebu tutafakari kama Taifa, tatizo linalosababisha ucheleweshwaji wa kesi katika Mahakama zetu ni *Diploma* na hizo C*ertificate?* Mimi naona Serikali inayumba. Inazunguka kama inaogelea, haitaki kwenda kwenye *point* ya msingi kwanini kuna matatizo katika ngazi zetu za Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ninaloliona, kwanza mazingira yenyewe ya utendaji jinsi ambavyo ofisi zao zimetekelezwa kwa muda mrefu tunazifahamu. Serikali haizingumzii ni lini itaboresha majengo ya Mahakama za Mwanzo. Ukienda kwenye Mahakama hizo, pamoja na teknolojia tuliyonayo sasa ya kompyuta na *software* lakini unakuta ma-*file* yamelundikana tangu miaka ya 80.

Ukiangalia kompyuta zenyewe zinahesabika, ukiangalia vumbi limetimka, sakafu imemomonyoka kwa muda mrefu, mazingira hayaridhishi. Hao ambao tunasema lazima wakawe na *degree* watakwenda kufanya kazi katika mazingira hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni kama tatizo ni *Certificate* au *Diploma*. Tatizo ni jinsi ambavyo tumesikia mara nyingi kada ya Mahakama wanasema kwamba wanatengewa fedha kidogo. Bajeti inakwenda finyu, lakini pia mazingira hayaridhishi. Ndiyo maana kuna rushwa imekithiri katika Mahakama zetu. Badala ya kuboresha maslahi yao, kuboresha utendaji kazi wao tunakurupuka tunasema tunataka wenye *degree*. Hili Taifa tunalipeleka wapi? Mimi sioni kama hii ni tija na sidhani kama Wabunge, hili tuna sababu ya kuliridhia. Kwa sababu kama tunakwenda kuridhia hili, lazima tuangalie hata tukiwapeleka hao wenye *degree,* watakwenda kukaa huko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia kada ya Ualimu. Serikali imesema kwamba tunawapa *special consideration* Walimu na Elimu ya Juu wanapewa mikopo au Walimu wanakuwa *considered* na Madaktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano kada ya Ualimu, ni walimu wangapi wamekwenda kusoma *degree,* wanarudi katika zile shule ambazo tulitegemea wangekwenda kufundisha? Tumeona walimu wengi wameishia kubadilisha kazi ile waliyokuwa wanafanya baada ya kupata *degree* zao. Hili Serikali mnalijua na sijui kwanini mnafikiri kwamba mkiwasomesha hawa Mahakimu wakapata nafasi ya kuwa na *degree* hizo, watarudi katika zile Mahakama. Mimi naomba Serikali isipate kigugumizi. Mkaangalie maslahi ya Mahakimu hao.

Kwanza wametumikia Taifa hili katika mazingira magumu kwa muda mrefu, leo kuwaambia wakapate hizo *degree* ni kuwasumbua kiakili, ni kuwavuruga kabisa pamoja na kwamba wamevumilia kwenye mazingira magumu ya vumbi, viti havitoshi, sakafu zimemomonyoka unawaambia sasa leo tunataka *degree*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo zuri, lakini tuangalie: Je, lina tija? Itawasaidia watu wetu? Tutakuwa tumeboresha utendaji kazi kupitia hawa Mahakimu kupata *degree*? Haya mambo hayatakiwi papara. Haya mambo yanatakiwa yaangaliwe kitaifa na Mwanasheria Mkuu atuambie sasa baada ya Mahakama tunawapa ujumbe gani na Walimu, Madaktari na Manesi? Hatutaki *Certificate* na *Diploma?* Kama tunawapeleka huko, ni vizuri hili Bunge Tukufu likajulishwa kwa sababu mimi naona hapa

mnakimbia tatizo, mnaleta *paracetamol* badala ya tiba ya halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana*. (Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili kusudi nami niweze kuchangia kwenye mabadiliko ya Sheria mbalimbali ambayo yameletwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuzungumzia juu ya suala la Mawakili kutokuruhusiwa ku-*practice* katika Mahakama za Mwanzo. Napenda kuishauri Serikali kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambayo amewasilisha mabadiliko haya mbalimbali ambazo zimeletwa ndani ya Bunge letu. Kuendelea kuwazuia wananchi ambao wana kesi mbalimbali katika Mahakama zetu za Mwanzo wasiwe na haki ya kuajiri Mawakili ili kusudi wakawatetee ni kutokuwatendea haki wananchi hawa. Hii ni kwanini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, iko wazi. Ukijaribu kuangalia ni wananchi wachache sana ambao wana weledi mpana katika masuala ya Sheria. Wakati tunaridhia lile Azimio ambalo lililetwa ndani ya Bunge juu ya suala la kuweza ku-*promote* Kiswahili, nilizungumza hapa tukasema kwanza Sheria mbalimbali zimeandikwa kwa lugha ambayo wananchi wengi hawana uelewa nayo. Sasa wakati tunajua tatizo hilo, Sheria nyingine zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza na ni Watanzania asilimia ngapi ambao wanafahamu lugha ya Kiingereza ambayo ndiyo inatumika katika suala zima la uandishi wa Sheria zetu?

Sasa leo tunasema kwamba ni marufuku kuwaruhusu Mawakili mbalimbali kwenda kusimama kwenye Mahakama za Mwanzo kuwatetea wananchi. Hii ni kuwanyima wananchi haki yao ambayo niite ni haki ya msingi ya kuweza kutetewa na Mawakili katika Mahakama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna *contradiction* katika hili. Wakati huo huo unasema kwamba Mawakili hawa wasiende ku-*practice* kwenye Mahakama za Mwanzo. Serikali inatwambia kwamba itaajiri na wameajiri, na kwa sababu nikirejea kwenye Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, baadhi ya Mahakama zetu zimeajiri watu ambao wana shahada za kwanza katika *field* ya Sheria ambao leo hii hawafanyi kazi, jambo ambalo tunaona kwamba hilo suala halijakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vyema tu labda pengine katika mabadiliko haya bora, hata Serikali ingesema pale ambapo katika Mahakama za Mwanzo kuna Hakimu ambaye ana kiwango cha taaluma cha kuanzia Shahada ya Kwanza, Mawakili waruhusiwe kwenda kuwatetea wananchi ili haki iweze kutendeka. Kwa sababu inafahamika wazi kwamba lengo kuu la kuzuia Mawakili wasiende kwenye Mahakama za Mwanzo ni kwa sababu Mahakimu walioko kule chini viwango vyao vya kitaaluma vilikuwa ni vya chini sana kwa maana ya kiwango cha Cheti pamoja na Stashahada kwa maana ya Diploma.

Sasa, kwa kuwa Mwanasheria Mkuu ameleta mabadiliko kwamba lengo ni kutaka watu ambao wamesoma kwenye kiwango hadi cha kufikia *degree* ya Sheria ndiyo wakafanye kazi huko, ni vyema mabadiliko

haya yakaenda sambamba moja kwa moja kwa kueleza kwamba pale ambapo itabainika kwamba Hakimu aliyepo ana Shahada ya Kwanza, basi Mawakili wakaruhusiwe kwenda kusimama na kuwatetea wananchi ili kuweza kuhakikisha kwamba haki inatendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nyongeza katika hilo, Serikali inapaswa kutoa *justification,* hii programu ya kuhakikisha kwamba Mahakama zetu za Mwanzo zinaondokana na tatizo la uhaba wa Mahakimu ambao hawana shahada litatatuliwa hadi lini? Kwa sababu nakumbuka kwa mfano kwa upande wa walimu, wakati Serikali imeweka mkakati wa kuondoa walimu waliokuwa Daraja B kuhakikisha wote wamekuwa na Daraja A, tuliona walisisitizwa wasome kwa juhudi.

Kwa hiyo, ni vyema Mwanasheria Mkuu atakapokuwa ana-*wind up* kwa niaba ya Serikali atoe *timeframe* kwamba hii programu itakwenda mpaka lini? Kwa sababu ametuacha *pending*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kwamba hadi itakapoonekana inafaa. Ni lini? Ni lazima tuwe na *program.* Hatuwezi kufanya vitu bila kuwa na programu kwamba ni miaka mitatu, ni miaka mitano, ni miaka sita au ni miaka mingapi? Kwa hiyo, ningeomba Serikali ihakikishe kwamba inapofanya mabadiliko, kuwe na *exception*.

Baadhi ya maeneo katika Mahakama za Mwanzo zilizobahatika kuweza kupata Mahakimu wenye Shahada ya Kwanza ya Sheria, basi Mawakili waende waka-*practice,* lakini pia tuweze kupata *timeframe* ni namna gani ambavyo tunaweza kuondoka na tatizo hili la kutokuwa na

Mahakimu ambao wana viwango ili kusudi haki iweze kutendeka. Sasa huu mpango utakwenda mpaka lini kuhakikisha Mahakama zote zimekuwa na Mahakimu wenye Shahada ya kwanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine ingewezekana kabisa tukasema kwamba Hakimu ambaye bado ana Cheti au ana Stashahada, huo muda ukipita, tuna m-*phase out* au ndiyo tuwafanye kuwa Makarani wa Mahakama, sio Mahakimu tena? Hii itaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kuhusiana na Mahakama, nimesikitika sana na nimestuka sana kusikia kwamba kuna baadhi ya Mahakama za Wilaya ambazo bado zinaendeshwa au zinaongozwa na Mahakimu wenye kiwango cha elimu ya Stashada. Nimestuka sana! Mimi binafsi sikutegemea.

Sasa mifano ambayo imetolewa na Msemaji Mkuu na Kambi ya Upinzani, uende kwenye Mahakama ya Mwanzo, Hakimu ambaye alihukumu shauri fulani, ana Shahada ya kwanza halafu unakwenda kukata rufaa kwenye Mahakama ya Wilaya ambayo unakuta kiongozi wake ana taaluma ya Sheria lakini ana Stashahada. Hiyo itakuwa kesi ya nyani unaipeleka kwa ngedere.

Kwa sababu hawa ni watu wawili tofauti na itakuwa haina tofauti na lile suala kwamba tumezuia Mawakili wasiende ku-*practice* kwenye Mahaka za Mwanzo kwa kuwa wana viwango vikubwa vya kitaaluma, lakini unamruhusu mtu kwamba akate rufaa kwenye Mahakama ya Wilaya halafu Hakimu ana Stashahada.

Naomba niishauri Serikali, wala hili halihitaji mjadala. Serikali ihakikishe Mahakama zote za Wilaya zina Mahakimu ambao wana viwango vya shahada ili kuhakikisha kwamba fursa za watu kukata rufaa wasikutane tena kukata rufaa Wilayani au uende kwenye Mahakama za Mahakimu Wakazi wa Mikoa. Hili jambo halijakaa vizuri. Kwa hiyo, naomba Serikali iweze kulizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni suala la Mahakimu wapya ambao wametajwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani ambao wameajiriwa na leo hii hawapo kazini, lakini taarifa zinazopatikana wanalipwa mishahara. Tungependa Serikali itueleze, wanawalipa mishahara watu ambao hawafanyi kazi kwa kutumia vigezo gani? Tungependa tupate maelezo, kushindwa kutoa maelezo ambayo yanaweza kutushawishi, Serikali na wote wanaohusika tukiwaita mafisadi, tutakuwa hatujawaonea. Huu utakuwa ni ufisadi mwingine. Unawezaje kumwajiri mtu, kwanza unamwajiri kinyume cha sheria? Mimi nafikiri ni busara kwa Serikali kuona kwamba wangeleta kwanza mabadiliko haya ambayo leo hii yanaletwa, halafu ndiyo hawa watu wangekuja kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuwaajiri, halafu mmeshindwa kuwapeleka baada ya kugundua kwamba kwenye suala la *technicalities* mlikosea, kwa sababu hamkukidhi matakwa kisheria, halafu mnawalipa mshahara, kwanza kosa la kwanza ilikuwa ni kuajiri watu kinyume cha Sheria.

Pili, mnajiongezea makosa kwa kuendelea kuwalipa mishahara wakati mnajua taratibu zilikiukwa. Huu ni ufisadi mkubwa na uhujumu wa uchumi kwa sababu yako

maeneo mengine ambako watu wanatafuta ajira na taratibu ziko *obvious* lakini mliacha kwenda kuajiri, mmeona huko. Hiyo unaweza ukasema kwamba kuna watu wachache walikaa wakaona ngoja watoe ulaji kwa watu fulani fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa makosa kama haya na nafikiri kwamba pengine hapa tunapowaambia ije kuwa ni fundisho *next time*, hili tatizo lisijirudie tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nijielekeze kwenye suala la umri wa kustaafu kwa Askari wa Jeshi la Magereza. Ni ukweli usiopingika kwamba mtu yeyote ambaye anatakiwa kuwa Askari, anapaswa kuwa ni mtu mwenye umri ambao mtu huyo bado ana nguvu. Vijana ndio wenye nguvu.

Mimi nashangaa sana kusema kwamba umri wa wale mabwana wakubwa ndani ya Jeshi, umri wao unaenda mpaka miaka 60. Wakati huo huo ukijaribu kuangalia taarifa mbalimbali kuhusiana na afya za binadamu, *life expectance* inatajwa kuwa ni umri kama miaka 40 na kidogo. *Life expectance* inazidi kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mnatuambia kwamba hawa watakwenda miaka 60, kama siyo kupeana ulaji ni kitu gani? Hivi ndiyo kusema kwamba ndani ya Jeshi la Magereza hakuna vijana ambao wana weledi mpana ambao wamesoma vizuri kitaaluma, ambao wana nguvu ambao wana uzalendo wa kuweza ku-*take* hizo *position* ambazo zimekuwa zinakaliwa na hawa viongozi wa Jeshi la Magereza ambao leo hii wameweza kulitumikia Jeshi la Magereza, ule umri uliokuwepo wakaachwa wakastaafu

kwenye umri ule, mnawaongezea tena umri mwingine bila kujali kwamba mnahitaji watu wenye nguvu, lakini mnakwenda mnazidi kuwaongezea umri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata huu umri wa hawa Askari ambao mnasema Koplo na *Sergeants* mtu ambaye tangu akiwa kijana ameajiriwa ndani ya Jeshi la Magereza kwa vigezo vile ambavyo vimeainishwa kwa mujibu wa Sheria, amekuwa muda mwingi ana-*deal* na wafungwa.

Wakati mwingine usiku na mchana mnapokuja kutuambia kwamba umri wa miaka 50 sijui 55, huyu mtu atatakiwa awe amestaafu, anakuwa ameshachoka. Serikali mnapaswa mliangalie hili. Mimi napendekeza, ni vyema sheria itamke na iweke wazi, bayana, hawa Koplo na *Sergeants* kama ni umri wa kustaafu iwe ni miaka 50 peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Serikali mmeleta mabadiliko ya vitu vidogo vidogo, mmesahau kuleta mabadiliko juu ya masuala ya pensheni za Askari wetu wa majeshi yote. Kwa sababu kwa utaratibu huu wa sasa kwamba Askari ili aweze kuingia kwenye mfumo wa pensheni hadi awe ametumikia jeshi lake.

Magereza wanalalamika, Askari Polisi wanalalamika hadi awe amefanya kazi kwa miaka 12. Wapo Askari waliolalamika kwamba mimi nikistaafu sasa hivi nitakuja kupata pensheni ya Shilingi milioni tano. Shilingi milioni tano Askari aliyelitumikia Jeshi kwa kipindi kisichopungua miaka 30, hii ni kuwaonea Askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe *task* kwa Serikali; ni lini Serikali italeta Muswada wa Mabadiliko ya Sheria katika masuala ya mafao ya Askari wa Majeshi ya Magareza pamoja na Polisi kwenye kuangalia suala lao la pensheni, wanaingia kwenye umri gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile mizengwe yote inayojitokeza ndani ya Jeshi, haiingii akilini kuona kwamba mtu unafanya kazi mpaka baada ya miaka 12 mtu ndiyo anakuja kuingia kwenye utaratibu wa kuingizwa kwenye pensheni. Hili jambo halijakaa vizuri. Nitaomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali aje atueleze.

Mimi nimetumwa na wananchi, wewe kama unashangaa, shauri yako! Nimetumwa na wananchi wakiwemo Askari, wanataka kujua kitendawili hiki cha mafao yao, huu utaratibu wa kuingiza baada ya kutumikia miaka 12 kitakwisha lini? Wanataka kusikia suala hili litakwisha lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo, naomba niseme tu kwamba nyie mnaokatisha tamaa, Serikali mnawakatisha tamaa Askari wa Jeshi la Polisi, Askari wa Jeshi la Magereza na Askari wengine ambao wako kwenye utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuwafanyie hilo ili kusudi kabla hawajaingia Mtaani, Askari wetu wamekuwa ni wavumilivu sana. Naomba hilo jambo liangaliwe, kwa kweli halijakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, sasa tunamalizia na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba kuunga mkono hoja hii muhimu ambayo inatuletea mabadiliko ambayo kwa sisi watendaji wa sekta ya ardhi yatatusaidia sana. Ni ukweli usiopingika kwamba pamekuwepo na mlundikano wa kesi za ardhi katika Mahakama Kuu. Kwa hiyo, kwa hatua hii kama alivyoelezea mtoa hoja, tutaweza kupiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nifafanue na kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba hoja hii haituingizi kwenye matatizo mapya ambayo sio ya lazima. Naomba wakati tunachangia hoja hii, ni muhimu sana tujiulize chimbuko la Mabaraza ya Ardhi. Chimbuko la Mabaraza ya Ardhi, ni Tume ya Ardhi iliyoundwa na Rais Mstaafu, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, akamteua Prof. Issa Shivji kama Mwenyekiti wake. Wakati ule, matatizo ya ardhi yalikuwepo na sina haja ya kufafanua kwamba yapo sasa hivi na ardhi na uhai tunakwenda pamoja yaani yanaendelea kuwepo. Sijawahi kupita katika nchi yoyote ambayo haina matatizo ya ardhi na migogoro ya ardhi kwa sababu ni maisha yenyewe. Kwa hiyo, kila Taifa linajiwekea utaratibu kutokana na mila zake, desturi zake, mapato yake, kiwango cha maendeleo, sheria ambazo zitawasaidia katika sekta hii ya ardhi. Kwa hiyo, hoja hii leo inatusaidia sana kwa ngazi ambapo Sheria za

Ardhi zinaangaliwa moja kwa moja usoni bila tena uwezekano wa kusuluhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie na kufafanua kwamba Mabaraza ya Ardhi sio *Court* za Ardhi. Kwa lugha ya Kiingereza *these are Land Tribunals, they are not Land Courts* na ni muhimu hapa kujua tofauti. Ningetegemea wengine wangejua tofauti hii na yamesimikwa kwa mujibu wa Sheria ya *Land Tribunal Act* sio Mahakama ya Ardhi.

**T A A R I F A**

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Naomba kutoa taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Taarifa!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba Mabaraza ya Ardhi yameanzishwa chini ya Sheria inayoitwa Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi ya mwaka 2001. Kwa hiyo, hicho anachosema kwamba *these are not Land Courts, she is wrong,* amekosea, ni sehemu ya Mahakama za Ardhi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru, Mheshimiwa Waziri, taarifa unaipokea?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui hapa Waingereza watatusaidia kati ya *Tribunals* na *Courts,* lakini naendelea kukaza kauli yangu kwamba kuna tofauti katika

lugha ya Kiingereza kati ya *Tribunals* na *Courts*. Sasa kama kuna Waingereza zaidi ya mimi na Mheshimiwa Lissu, naomba wajitokeze. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nafafanua na hapa tatizo ni tafsiri na linaweza likatukwaza. Mabaraza ya Ardhi yameundwa kusudi kuwawezesha wananchi kulingana na tamaduni zetu, kutatua migogoro ya ardhi na kutoa haki kama inavyoeleweka kwa tamaduni zetu. Kwa hiyo, Mabaraza ya Ardhi yanaundwa hapohapo ambapo mgogoro wa ardhi upo na Mabaraza ya Ardhi yameundwa baada ya mapendekezo ya Wanasheria waliokubuhu nchini hapa kama Prof. Shivji baada ya kuona kwamba *system* ilikuwa haifanyi kazi. *Primary Courts* zilishindwa kusimamia matatizo ya ardhi wakati ule, ikaonekana kwamba yaundiwe Mahakama zake. Sasa hapo ndio Kiswahili na lugha, itabidi sasa wana wa UKUTA, wale Waswahili, mtutafutie neno lingine kusudi tusipingane hapa bila ya sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaposema kwamba Baraza la Ardhi la Kata lisiwepo, inamaanisha sasa ndio moja kwa moja unakwenda kwenye *Primary Courts* zetu. Hamna tena nafasi ya usuluhishi, sasa hapo ni moja kwa moja mwenye nguvu, inabidi sasa uanze wewe uonyeshe kwamba haki iko upande wako. Kwa sasa hivi, utaratibu tulionao, sheria tuliyonayo, inaruhusu watu kuchangia, Wajumbe wa Baraza wapo na wanajua mazingira ya pale. Kwa hiyo, kama tupo Singida kwa Mheshimiwa Lissu, tunategemea kwamba wapiga kura wake ndio watakuwa pale kidogo wako kwenye hilo Baraza lakini unaweza ukajikuta una *Primary Court* labda sasa mtu anatoka

Muleba ndio Hakimu wa pale moja kwa moja anajitosa kwenye mgogoro wa ardhi, maafa yanatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila ya kwenda mbali nitoe mfano mambo yanavyoweza kwenda kama huna Baraza la Ardhi. Kule kwangu Wilaya ya Muleba, kuna Mahakimu kadhaa wamejiingiza kusikiliza kesi za ardhi kabla hazijapita kwenye Mabaraza, kinyume cha sheria kabisa na matokeo yamekuwa maafa. Mkuu wa Wilaya wetu, mara mbili amelazimika kuingilia migogoro ya ardhi ambayo, kwa kinyume cha sheria na kwa ubabe na kwa ujanja imepelekwa kwenye Mahakama za Mwanzo. Kwa hiyo, unakuta wanakijiji wanaelewa kwamba mwenye haki ni fulani, lakini sasa kwa sababu anazozijua mwenyewe *Primary Court Magistrate*, Hakimu ameamua kwamba anayeshinda ni fulani. Kwa hiyo, panatokea uvunjifu wa amani na Mkuu wa Wilaya anajikuta analazimika kuingilia kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeliona, labda Waheshimiwa wenzangu na Mheshimiwa Mwenyekiti na ninyi mnaweza kuwa mmeshaona kesi kama hizi. Hizi ndizo zilifanya sheria ile kuundwa sio kwamba imeibuka tu, ikaanguka tukajikuta tuna Mabaraza ya Ardhi. Ninaposimama hapa kama Waziri wa Ardhi, ni jukumu langu kuijulisha nyumba hii Tukufu kwamba tusije tukapendekeza mambo kwa ushabiki au kwa sababu yanaonekana ni mazuri tu lakini maafa ni makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Primary Courts* zetu nyingi, ni vyombo vya haki lakini sina uhakika kama vinatoa haki. Kwa hiyo, pale ambapo wanashindwa kwenye kesi ya ardhi sasa uvunjifu wa amani na Wakuu wa Wilaya mara nyingi,

Muleba nimeliona mara mbili, wanalazimika kuingilia kati, kuzuia utekelezaji wa kesi ambayo ukiitekeleza wananchi watachukua sheria mikononi mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, katika Kata ya Buganguzi, akaingia tena Hakimu wa *Primary Court,* akaamua mama afungwe kwa sababu mwanawe amemshtaki. Kwa hiyo, mtoto amemshtaki mama yake katika mgogoro wa ardhi ambao tulikuwa tumeshaumaliza kwenye Baraza kwa kufuata jadi zetu na mila zetu na usuluhishi. Matokeo ni nini? Yule mama akaenda kufungwa kwa sababu mtoto wake kwa sababu ambazo Hakimu anazielewa ameshinda kesi ya ardhi. Kilichotokea, yule mama alipotoka jela, ikabidi mimi nitoe sasa mdhamana kumtoa jela maana sikuelewa kwa nini yule mama amefungwa na mwanawe wa kuzaa wala sio mtoto wa kambo wala nini, ni mtoto wake wa kuzaa. Kilichotokea kijijini ni kitu gani? Wananchi wakachukua mapanga, wakakata migomba yote ya yule kijana.

**MBUNGE FULANI:** Niliona kwenye televisheni.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Hata Mheshimiwa hapa anasema aliona kwenye televisheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nichangie kwa kusema kwamba, hoja imekaa vizuri, Mwanasheria wetu amelichunguza, inapofika ngazi ya *High Court* kweli pale tunahitaji Majaji wote watusaidie, kuna malimbikizo lakini kwenye ngazi za Kata, Wilaya, nakubali na nimeshasema mara nyingi kinachotokea, sasa hivi kweli Wilaya nyingi hazina *District Land Tribunals* kwa sababu ya

ufinyu wa bajeti. Waheshimiwa mnaosikiliza, ninachokiomba wakati wa bajeti mniangalie kwa jicho la huruma, Mabaraza yaweze kuundwa kila Wilaya, tuondoe ile adha ya watu kuwa wanahangaika kwenda kwenye Mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kimsingi tuna Mabaraza ya Mikoa au sio? Tunayo 39 wakati tunahitaji 136, hilo ndilo tatizo lakini tusi-*confuse*. Baraza inapokuja ngazi ya Wilaya pamoja na maneno ya Mheshimiwa Lissu, hata kwenye ngazi ya Wilaya bado sheria kama tunavyojua kwenye Mahakama inakuwa haijafanya kazi. Kwa hiyo, pale Mwenyekiti wa Baraza la Wilaya na mwenyewe anafanya kazi mbili, ingawaje tunawaweka Wanasheria lakini ni wasuluhishi wale. Anasuluhisha, ana Wajumbe wanakwenda kwenye tukio, unapata nafasi, katika *Courts* zetu hizi hakuna utaratibu kama huo, utaratibu unaleta pale *evidence in court,* mnaleta ushahidi pale mliposimama lakini katika Mabaraza yetu wanakwenda wanaangalia mipaka ikoje, wale Wazee wa Baraza, wanamshauri hata huyo Mwenyekiti wetu ambaye kwa kawaida anakuwa Mwanasheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nifafanue tu na nilizungumze kidogo hili kwa uchungu kwa sababu tukifanya kosa, tukakurupuka, tukaondoa Mabaraza ya Ardhi, tunarudi hukohuko ambapo Mheshimiwa Rais Mwinyi alitutoa. Kwa sababu wakati ule, naomba watu msome *literature* hasa watu wasomi kama Mheshimiwa Lissu, lazima mrejee hivi vitu, muangalie nyuma muone kulikoni, mbona tuko hapa tulipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona nichangie hilo kwa wadhifa wangu, lakini naamini kwamba Mwanasheria Mkuu atakaposimama yeye ana uwezo mkubwa zaidi hata kuyaweka vizuri zaidi kisheria. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Sasa nitamwita Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kwa mujibu wa Kanuni ya 64(2) ambayo ninaomba niisome. Inasomeka kwamba:-

*"Mbunge yeyote anayeamini kuwa Mbunge mwingine amevunja au amekiuka masharti ya fasili ya (1) ya Kanuni hii, atasimama mahali pake na kumwambia Spika wa Bunge "Kuhusu Utaratibu" na atakaporuhusiwa na Spika kusema, atalazimika kutaja masharti ya Kanuni hii yaliyovunjwa au kukiukwa na Mbunge huyo mwingine, na kama Mbunge huyo mwingine atakuwa anasema wakati huo, atakaa chini kusubiri maelekezo na mwongozo wa Spika kuhusu jambo hilo".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kanuni hii ya 64(2) isomwe pamoja na ile fasili ya (1) kipengele cha (a).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitumie Kanuni ya 68 fasili ya (7) inayohusiana na kuomba mwongozo

wako ili nipate mwongozo kuhusiana na jambo ambalo lilitokea leo hii hapa asubuhi. Jambo hili lina historia kidogo kwamba katika siku za karibuni Bunge lako Tukufu limeonekana kwamba ni genge fulani la wahuni, linaleta zogo na baadhi ya vyombo vya habari vimeandika ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, umeomba Mwongozo, hujaomba kutoa maelezo. Naomba ukae chini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jioni tuna wachangiaji wengi bado na baadaye nitawasiliana na Meza kujua tutapanga vipi. Naomba kusitisha Bunge mpaka saa 11.00 jioni hii.

*(Saa 6.52 Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2012 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.3) Act, 2012]*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji wetu wa kwanza, ni Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninakushukuru. Nitaanza mchango wangu kwa kuungana na maoni ya Kambi ya Upinzani lakini zaidi ya kutoa angalizo kwa *Miscellaneous Amendments* ambazo zinakuwa zinaletwa kwa kipindi kifupi, lakini unakuta ndani

yake kuna vipengele vizito sana ambavyo vinaweza kuwa na athari kubwa kwa nchi, ama kwa Bunge, ama kwa Taasisi mbalimbali ambazo zimetengenezwa kutokana na na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa nini? Wabunge wenzangu mnakumbuka mwaka jana baada ya Kamati, ama *Oversight Committees* hususani ambazo zinashughulika na masuala ya fedha, walipotoa taarifa zao hapa Bungeni na kuonyesha ni kwa namna gani fedha za umma zinatumika vibaya na kwa kuainisha Wizara mbalimbali ambazo matumizi yake ya fedha yalikuwa ni mabovu, kukapelekea pendekezo la kutaka kupiga kura ya Kutokuwa na Imani na Waziri Mkuu na saini zikapatikana na kubakia hatua ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla hatujaja kwenye hatua ya utekelezaji, yalifanyika mabadiliko makubwa ya Baraza la Mawaziri. Msingi mkubwa wa mabadiliko ya Baraza la Mawaziri, ni taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye kwa kipindi kirefu sana amekuwa akiainisha kwa namna gani mabilioni kama siyo matrilioni ya fedha za Kitanzania yanatumika pasipokuwa na utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida na kwa mujibu wa Katiba, taarifa ama ripoti ya Mkaguzi Mkuu inaletwa mwezi wa nne baada ya kukabidhiwa kwa Rais. Vilevile, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge, Kamati ambazo zinasimamia masuala ya fedha *POAC, PAC* na *LAAC* zenyewe zinaleta taarifa mwezi wa nne lakini tofauti ni kwamba wao wanaleta taarifa za mwaka mmoja uliopita wakati *CAG* analeta taarifa mpya ambayo bado haijaangaliwa na zile Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa imekuwa ni kawaida kwamba kwa kuwa *CAG* anakagua mahesabu na yale mahesabu mengine ambayo anakosa majibu yake kwa mfululizo, ndio analeta kama *query* ili sisi Bunge kama chombo cha kutunga Sheria, kama chombo cha kuisimamia Serikali, tuweze kutekeleza wajibu wetu kuielekeza Serikali. Kwa mabadiliko yanayoletwa leo na Serikali ya ku-*amend the Public Audit Act,* yanatoa maelekezo kadhaa. La kwanza, Bunge letu halitajadili ripoti ya *CAG* pekee pasipokuwa na majibu kutoka Serikalini, kutoka kwenye Wizara mbalimbali ambazo taarifa za *CAG* zime-rise *query*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake hapa ni nini? Maana yake ni kwamba inaletwa Sheria lakini madhumuni ya Sheria ni kusaidia Serikali ifiche madhambi yake wakati *CAG* ameonyesha kwamba kuna tatizo hili, Wabunge tunataka kujadili, Serikali iseme tena kuwa sisi ambao wakati *CAG* anafanya kazi katika kipindi cha mwaka mmoja wa kukagua na kuwaomba Maafisa Masuuli walete ushahidi wa kiwango cha fedha ambacho uhalali wa matumizi yake hauonekani, Serikali imekosa majibu katika hatua ya CAG na imekosa majibu katika hatua ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuelewe kuwa mara taarifa inapotolewa, Kamati za Hesabu za Mashirika ya Umma na yenyewe inakaa, inaangalia *CAG* amefanya nini halafu inaita Mashirika husika, ama Kamati ya Fedha za Serikali, inaita Idara na Wizara za Serikali ili kuhoji. Baada ya hapo, taarifa zinazokuja hapa Serikalini, zinakuwa zina maelezo ya *CAG*, zina maelezo ya Taasisi baada ya kuitwa na Kamati ambazo zinafanya kazi kwa niaba ya Wabunge na kisha

Wabunge wanaanza ku-*react* kutokana na hayo maelezo matatu. Kwa Sheria hii, inatuambia kwamba, *CAG* majibu yameshindwa kupatikana, kwenye Kamati za Bunge majibu yameshindwa kupatikana lakini kuna miujiza ambayo itaisaidia Serikali kuja hapa kueleza ni kwa nini huko kote kulikuwa kuna mapungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachokiona, Bunge linanyang'anywa meno yake pasipo kujua kwa sababu ukiangalia Sheria ya zamani ilikuwa wazi kabisa, inaeleza kuwa, *the Public Accounts Committee, Local Authorities Accounts Committee and Parastatal Organization Accounts Committee, shall discuss the report of the CAG after they have been tabled in the National Assembly.* Ya pili, inasema, *upon completion of hearings, the Parliamentary Oversight Committee shall prepare and submit to the National Assembly reports which may include comments and recommendations.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri hii ilivyo, ni kwamba ripoti inaletwa, Kamati za Hesabu zinaenda kuangalia, zinatuletea sisi taarifa, Wabunge tunajadili, tunatekeleza kazi yetu ya Kibunge ya kusimamia Serikali lakini kwa hili tunaambiwa wanatoa taarifa *CAG,* wanaileta hapo, Kamati inaenda inakagua, baada ya kukagua, tunakuja inasomwa taarifa ya Mkaguzi Mkuu, maoni ya Kamati pamoja na taarifa nyingine ya Serikali, kwa lipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nawaomba Wabunge wenzangu, haya masuala ni muhimu sana na ubaya ni kwamba ukiangalia hii Sheria ya zamani hiki ambacho kimeletwa kwenye mabadiliko katika kipengele cha 38, kilikuwepo katika kipengele cha 40 cha Sheria

iliyopita, tofauti ni kwamba licha ya kusema kuwa *Pay Master General* anatakiwa atoe maelezo kwa Waziri, kipengele hiki kipya kinachokuja kinatubana zaidi kwa kusema kuwa Bunge halina mamlaka ya kujadili taarifa yoyote ya CAG pasipokuwa na majibu kutoka Serikalini, hii ni biashara gani? Sasa kama chombo cha Serikali kimekagua ambacho ndiyo *CAG* na ambacho ndicho kinatambulika Kikatiba, kama Kamati ya Bunge imekagua, imewaita wataalam, majibu yameshindwa kupatikana, hivi ni miujiza gani kutoka Mbinguni ambayo itaifanya Serikali ije itoe majibu ya ziada Bungeni ili hizo taarifa zote mbili tuzijadili kwa pamoja? Bunge tunaingizwa kwenye chaka na hili chaka ni kwa kuwa hizi Sheria wamezileta haraka, hatujazisoma, hatujapata muda wa kudadavua, tutajikuta kuwa tunaiingiza hii nchi mahali ambapo hapastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia taarifa ya *CAG* kwa mfano kuhusiana na majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali yaliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ripoti za Serikali Kuu kwa miaka ya nyuma. CAG anasema hivi, mapendekezo mengi yaliyotolewa katika ripoti ya Serikali Kuu kwa miaka iliyopita hayakutekelezwa na Serikali. Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali, hayazingatii maoni ya mapendekezo yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, (b) anasema, ninazidi kusisitiza kwa Serikali kutekeleza mapendekezo ambayo yalilenga kuboresha moja kwa moja mifumo na michakato mbalimbali pamoja na kuepusha madhara kwa mambo yanayoendelea kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonyesha kabisa kuwa hawa ambao wamepewa mamlaka ya kulinda fedha zetu hawatekelezi wajibu wao ipasavyo kulinda fedha zetu. Tunapoleta taarifa ya *CAG*, tunapoleta taarifa za Kamati za Bunge na kuleta maelezo mengine ya Serikali hapa, tutaletewa taarifa zingine za uongo kama ambavyo *CAG* anasema deni la Taifa linakuwa kubwa, anakuja Waziri hapa anatupa ma-*calculation* ya uongo wakati nchi inaendelea kuangamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati *CAG* kwenye ripoti yake anasema kwamba, jamani deni la Taifa limezidi, misamaha ya kodi imezidi, tunapata majibu ya hovyohovyo, majibu mepesi lakini kwa kuwa kuna kauli ya Serikali lazima itawalainisha Wabunge wengine watajikuta wanaiamini Serikali inasema ukweli lakini kumbe kiuhalisia kuna malalamiko mazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ushauri wangu ni kwamba Bunge liachiwe lijadili taarifa ya Mkaguzi wa Serikali kwa uhuru kama ilivyo Sheria ya sasa, tukiruhusu kuingiliwa na Serikali, ni kukwepa uwajibikaji na Serikali inakwepa uwajibikaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tunajua *CAG* analeta zile *outstanding issues* ambazo zimekosa majibu, sasa kama *outstanding issue* zimekosa majibu ndani ya miaka miwili, mwaka wa kwanza Wakaguzi wa *CAG*, mwaka wa pili wa Kamati za Bunge, hivi mwaka wa tatu Serikali watakuja kutupa sera gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnapokwa mamlaka yenu kwa sababu watu hawataki kutekeleza wajibu wao. Mkikubali kupokwa mamlaka yenu, itakula kwenu na mtahukumiwa. *CAG* anafichua maovu ya Serikali, anatusaidia Wabunge kuona, mkiruhusu mambo yafichwe, tufunike kombe mwanaharamu apite, haitasaidia nchi. Kwa hiyo, mimi niwaombe Wabunge tutekeleze wajibu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile yamefanyika mabadiliko ya Sheria ya Ardhi, mimi sina tatizo na mabadiliko hayo lakini kumekuwa kuna malalamiko makubwa sana. Kuna gharama ama ada zimepanda sana ili mwananchi aweze kusajili nyaraka mbalimbali katika Wizara ya Ardhi. Kwa bahati mbaya Waziri wa Ardhi hayupo wala Naibu wake sijamwona, fedha inapanda toka elfu kumi kwa mfano kwenye *Power of Attorney* mpaka laki moja na sitini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ninakushuru Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** *Official search*...

**MWENYEKITI:** Halima kaa chini.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Naomba Wabunge tukileta mabadiliko mtuunge mkono, Bunge limetolewa meno yake, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Wewe kaa chini, sasa namwita Mheshimiwa John Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, sikutegemea kama ungeniita sasa hivi lakini ninaona ni lazima nijaribu kufafanua mambo mawili, matatu juu ya Muswada wa mabadiliko yaliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaangalia *amendments* ambazo Mwanasheria ameleta kuhusu ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Sasa nilikuwa ninajiuliza, kila Sheria kwa kawaida unaitengeneza ili kuzuia kitu fulani kisifanyike. Hata kama Mwanasheria ukituambia tukitunga Sheria hapa, ukasema kuwa Bunge halijadili ile taarifa mpya, kusema kweli husemi lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumetunga Sheria hiyo ya *Audit* na tumesema mara tu ripoti inapowekwa Mezani inakuwa ni mali ya Bunge na umma. Unawaambia wawakilishi wa umma wasiizungumzie lakini ruksa kwa waandishi wa habari, kwa wanaharakati na watu wengine. Mimi ninafikiri ni kuleta madhara zaidi kwenye hiyo ripoti kuliko kupata faida ambayo Serikali inayotaka kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nimekuwa nikikumbana na Maafisa Masuuli wengi *(Accounting Officers)*, nafikiri hofu ya Serikali haiwezi kuondoshwa na *amendment* hizi. Hofu ya Serikali ni kwamba tunajadili vitu ambavyo baadaye vitajibiwa na ma-*Accounting Officers.* Hawa ma-*Permanent Secretary* ambao wamekuja mbele ya Kamati yangu, tumewaeleza njia siyo kutengeneza hoja,

njia ni kuzuia hoja kwa sababu hoja zikishaandikwa na *CAG* kwenye kitabu, hizo zinakuwa hoja zinazozunguka kwenye umma mzima, Kimataifa na ndivyo vile Taifa hili linaangaliwa kwamba Wizara ya Fedha haijaweza kuweka wazi nyaraka moja, mbili, tatu ambazo thamani yake ni shilingi bilioni 230, hiyo ndiyo inayotoka kwa watu wote. Kwa hiyo kwa kuwaambia Wabunge kuwa msijadili, haina maana kwa sababu dunia nzima itakuwa inajadili kuwa Tanzania haiwezi kutoa *documents* pale ambapo wanaombwa na *CAG* watoe *documents.* Kwa hiyo, *cure* ingerudi kwenye Serikali kwamba Maafisa Masuuli ni lazima watoe nyaraka zote zinazohitajiwa na *CAG* ili pasiwe na hoja za kujibiwa. *To me,* hii ndiyo ingeonekana ndio ufanisi wa Serikali siyo kuwakataza Wabunge tusijadili jambo hili. Kusema kweli hii inarudisha uwajibikaji nyuma na haisaidii Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, watu wanasema Kambi ya Upinzani kila wakati inakosoa, kukosolewa ni kuzuri, kwa sababu tunawakosoa mara nyingi sana ndiyo kusema tunawawezesha mpate nafasi ya kurudi humu Bungeni kama Chama Tawala. Wakati mwingine labda tungeacha kukosoa ili tukutane na ninyi huko mbele ya safari lakini kwa sababu Taifa hili lazima liendelee, ni vizuri kama kuna matatizo yasemwe na yasemwe wazi. Najua kuwa tutapitisha hapa lakini mimi kwangu ninasema kuwa haina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haina maana yoyote kwa kuwa watu watayazungumza, Wabunge watayazungumza na sioni itakuwa ni namna gani mtu umeletewa taarifa iko hapa na taarifa ya *Public Accounts Committee* iko hapa, kwa nini usiseme, hivi mwaka jana umeonywa na *Public*

*Accounts Committee* kuwa ondoa dosari hii, mwaka huu tena dosari hiyohiyo imekuja, kuna ubaya gani? Mimi ningekuwa na uwezo, ningefuta hii *amendment* ya kuwaambia Wabunge wasijadili, hiyo ndiyo ingekuwa busara zaidi lakini turudi kwa *Accounting Officers* na kuwaambia wafauate mawazo ya *Public Accounts Committee* ambayo inawaambia zuieni hoja, msiwe mafundi wa kujibu hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutumia nafasi hii kuwasifu, kuna Ma-*Permanent Secretaries* wengi sana ambao walikuwa na *queries* labda 20, leo unakuta ana *query* moja tu au mbili, wamefanya kazi nzuri. Kwa hiyo, sasa unataka kuwalegezea kamba kwamba hiyo ripoti hata ikija itaonekana lakini haitajadiliwa, kwa hiyo, ninyi fanyeni tu mnachopenda, mtajibu baadaye, mimi naona *we are being retrogressive* na nchi hii inasifika kiulimwengu kwa kuchukua hatua za kuwajibisha watu ambao hawafanyi kazi yao vizuri. Tunamsifu Rais, tumeleta hoja hapa *Public Accounts Committee* pamoja na *CAG*, amechukua hatua na leo tunamzungumza katika *forum* mbalimbali za ulimwengu *like an Accounting Officer number one* kwa kuonesha *political will,* kwamba kama ukifanya makosa mimi nitakuchukulia hatua, Rais amefanya hivyo lakini nashangaa Serikali hiyohiyo tena inaleta sheria ya kutafuta njia ya Ma-*Accounting Officer* kujificha. Kusema kweli mimi nimesikitika sana, kwamba tunaenda kwa njia hiyo na haitasaidia Serikali, haitasaidia wananchi, tungetafuta njia za kuweza kuzuia hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua bajeti ya mwaka huu ambayo itakaguliwa mwaka kesho, ni lazima itakuwa na hoja kwa sababu mpaka leo tarehe 17 Januari sijui ni Wizara

gani ambayo imepokea fedha ya maendeleo? Miezi sita imepita, *not a single disbursement* ya Serikali imetoka kwa ajili ya bajeti ya maendeleo, ndiyo kusema miezi sita mingine ndiyo zitoke sijui kwa kasi gani, Mungu atusaidie ili bajeti hii iweze kutekelezeka. Kwa hiyo, tayari Mheshimiwa Waziri wa Fedha umeshatengeneza mazingira ya kuwa na hoja katika bajeti tuliyonayo ya mwaka huu kwamba bajeti ile ya maendeleo haijafanya kazi kwa sababu pesa hazijatoka, lakini ungeweza kuzuia hoja hiyo kwa kuhakikisha kwamba pesa zinatoka na usipotoa pesa za maendeleo ndiyo miradi mingi haitakuwa imelipwa, kutakuwa na madeni, miradi itachelewa, kutakuwa na riba na hapo umetengeneza hoja, kwamba mradi huu ulikuwa ni shilingi bilioni 50 sasa umekuwa shilingi bilioni 55! Tunacheza ngoma gani? Kama tunataka kucheza ngoma ya uwajibikaji, *then* twende na utaratibu uliopo kwa sasa, kwamba Maafisa Masuuli wawajibike ipasavyo na kama tunayo bajeti tumesema *so many trillion* zitatumika, pesa zitoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi hili Bunge ninalishangaa, tunazungumza mambo mengine ya ujingaujinga tu mara nyingine, samahani kwa kusema hivyo, mtu anasimama anaomba utaratibu, mbona hatuulizi? Tunamaliza sasa tunaenda nyumbani, mbona hatuiulizi Serikali itupe ripoti, bajeti yetu tangu tumeiidhinisha imetekelezwa namna gani? Hicho ndicho wananchi wanachosubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanasubiri maji, wananchi wanasubiri shule, wananchi wanasubiri dawa na sasa hivi ni mwaka mbaya huu, wananchi wana njaa, wananchi wanategemea Serikali yao iwasaidie kwa

chakula, sasa hivi ghala la chakula limekauka. Tungetegemea Serikali ingetueleza kabla hatujaondoka hapa, pesa kiasi gani zimetoka kwa ajili ya kuwasaidia watu walio na njaa? Hayo ndiyo mambo ambayo tungependa kusikia katika Bunge hili, siyo kila wakati sijui utaratibu, tutafika wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni lazima ifuate utaratibu mkubwa ambao ni kufuata bajeti, la sivyo tunakaa hapa miezi mitatu tunazungumza bajeti na kama bajeti haitekelezwi, ni afadhali turudi nyumbani na tu-*save* pesa ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu wa kuzuia Wabunge kuzungumza, haufai. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Cheyo. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Kebwe.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja hii ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako niseme *preamble* kidogo, kwa sababu nimepata fursa hii na Serikali iko hapa na inanisikia. Zoezi ambalo Wizara ya Maliasili wamefanya hususani mwaka jana mwishoni la kuainisha mipaka kulingana na Tangazo la Serikali Na. 212 la mwaka 1968 wakati wa Serikali ya Awamu ya Kwanza. Zoezi hili la mipaka limeleta adha kubwa na ni kwa nchi nzima, Serikali isitishe pale walipofikia waanze upya kwa njia shirikishi. Kwa mfano, Wilaya yangu ya Serengeti zaidi ya kaya 150 karibu wananchi 1000 wameambiwa kwamba

wapo ndani ya hifadhi. Hivi miaka yote hiyo kweli idadi kubwa ya watu hiyo imekuwaje katika eneo la hifadhi na Serikali ilikuwepo inaona? Kwa sababu timu hizi tumeona zinakwenda mbili, tatu tangu mwaka 2008 kuainisha mipaka kulingana na Tangazo la Serikali na kila timu inavyokwenda, kwa mfano ilivyokuwa 2010 na mwaka 2012 kila timu kutoka Wizara ya Maliasili inakosoa timu ambayo ilikwenda kabla yake na ni Wizara moja hiyohiyo. Kwa hiyo, naomba suala hili Serikali ichukue hatua za haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najielekeza katika sehemu ya Hakimu wa Mahakama. Tukijaribu kuangalia ushauri ambao umekuja katika *Miscellaneous Amendment* hii, kwa sehemu kubwa ni nadharia, sidhani kama itawezekana. Kwa sababu gani? Leo hii tunakwenda kutoka kwa Mahakimu wa Cheti kupata Mahakimu wale wa Shahada, mazingira haya katika upungufu mkubwa wa watumishi tulionao, itawezekana vipi? Kwa sababu mazingira haya ndiyo ambayo yamesababisha kumekuwa na adha kubwa sana katika sehemu hii ya Mahakama hususani Mahakama ya Mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano pale Jimboni kwangu kuna Mahakama moja ya Mwanzo Majimoto, yule Hakimu aliyepo pale kwa sababu ya udhaifu hafuatiliwi, Hakimu yule utamkuta anakwenda kazini saa tano na wakati mwingine ameshakaa sawa, amepiga maji yake vizuri, unamwona katika mazingira ya kawaida na hata hukumu na ku-*refer* kesi anatoa rufaa hizi akiwa kwenye kilabu cha pombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa mazingira kama haya ambayo tunakwenda kupata wataalam wa ngazi za

juu, kweli ni halali tunasogeza huduma karibu halafu na kuboresha kama nchi nyingine zilivyo duniani? Mfano, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo wa cheti, kesi ziko nyingi huwezi kumchukua *Advocate* ambaye ni *graduate,* ana shahada halafu akaenda kumtetea mteja wake, haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la msingi, vitu vingine vya msingi viangaliwe. Kwa mfano, katika usimamizi, hawa wa Mahakimu tumewaandalia mazingira gani kulingana na elimu hii ambayo tunakwenda nayo, vyombo vya usafiri vikoje, mazingira ya kazi yakoje, makazi yakoje? Tusirudi kule nyuma tulipokuwa kipindi kingine unakuta hukumu inatolewa halafu unaambiwa changia kuandika hiyo hukumu tena kwenye daftari na wakati mwingine hata kwenye karatasi tu la sigara, yale ambayo tumeyaona enzi hizo. Kwa hiyo, ni vizuri mazingira haya twende kwa kuyaboresha vizuri kweli yaendane na matakwa ya Watanzania. Mafao yameangaliwa kivipi kwa sababu unapoboresha sheria, unataka *higher standard and high skilled staff,* ni lazima viendane na mafao. Huwezi leo ukasema *graduate* Hakimu Mahakama ya Mwanzo ana shahada halafu unamlipa mshahara wa shilingi laki mbili au laki tatu, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine katika *amendment* ilivyokuja tunaambiwa Chuo cha Mahakama cha Lushoto kitaboreshwa kwa ajili ya kudahili wanachuo watakaokwenda kusoma digrii. Hivi ni kipi kianze, upate wataalam kwanza ndiyo uboreshe sheria au uboreshe sheria ndiyo utafute watalaam? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo ushahidi katika nchi hii mwaka 2008, wakati Serikali yetu chini ya Chama shupavu cha Mapinduzi, walileta utaratibu mzuri wa rufaa kwa upande wa wagonjwa, kwamba Hospitali za Rufaa za Mikoa ziweze kuwa na hadhi hiyo, lakini wataalam wale wako wapi mpaka leo hii? Hospitali zilizo nyingi zimebaki katika makaratasi. Mazingira haya nayafananisha na hali ilivyo katika rufaa kwenye afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri kwanza tungewapata hawa wataalam kama ambavyo imeanza kujitokeza katika elimu, wapo Walimu wengi siku hizi wamesoma mpaka shahada lakini wapo shule za msingi. Kwa hiyo, linakuja wazo zuri kusema kwamba sasa Walimu wenye shahada waweze kufundisha katika shule za misingi hivi ndivyo *amendment* yake itakuwa *practical*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijaribu kuangalia suala zima ambalo ni nyongeza na nashangaa kwa nini halikuja katika kipindi hiki. Ukijaribu kuangalia Sheria Na. 8 ya mwaka 2002 ya masuala ya kuajiri watumishi, ni kwa nini mpaka leo hii haijaletwa hapa Bungeni? Kwa sababu hali halisi, unamchukua dereva anatoka Mtwara unampeleka Mara-Serengeti, ni kuongeza gharama za bure tu, kuna sababu gani ya msingi? Kwa hiyo, mimi natarajia kipindi kingine kijacho tupate hii *Miscellaneous Amendments* ili sheria hii iweze kuhuishwa, la sivyo tunaongeza gharama bure kwa Serikali na kuleta adha. Dereva unamwajiri anatoka Serengeti kwenda Mkoa wa Lindi, unamwambia njoo katika usaili Dar es Salaam na wanakuja maelfu kweli kwa sababu madereva wako wengi siku hizi ambao wanatafuta kazi, kwa hiyo, suala hili la mabadiliko ya sheria hiyo ije ili kusudi tuijadili vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukijaribu kuangalia utekelezaji kwa ujumla wa muda wa sheria inapotungwa halafu baadaye unaunda Kanuni, kuna ucheleweshaji mkubwa sana. Ushahidi kwa mfano Sheria Na. 5 ya mwaka 2009 kuhusu Wanyamapori, mwaka juzi Bungeni hapa tumeambiwa kwamba Sheria hiyo, Kanuni zipatazo tano kati ya 16 zimeshaandaliwa, hivi mpaka leo hii kanuni hizo 11 tunaingia mwaka 2013 zipo wapi? Kwa sababu sheria hizi zinatungwa, wataalam wanakwenda wanakaa halafu wanakalia kwa sababu ya maslahi ambayo wanayapata kutokana na udhaifu wa sheria. Kwa hiyo, hili suala liangaliwe kwa umakini, *amendments* hizi ziwe zinakuja mapema tunazifanyia kazi kwa maslahi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo niliona tushauriane ni kwamba *powers* ambazo Mawaziri wanapewa kisheria zinanyima haki. Kwa mfano, katika utungaji wa Kanuni, kwa nini Kanuni zisije hapa Bungeni tuzipitie, tuone zinaendana kweli na tulivyopitisha sheria? Kwa sababu Bunge likishapitisha sheria, ndiyo mwisho pale, unakuja kuona *regulations* katika *operational level* na zingine zina upungufu, zingine zimepindishwa na zingine hazikuingia kulingana na ushauri wa Bunge. Kwa hiyo, ni vizuri Waziri apunguziwe mamlaka haya ili kusudi sheria ikamilike vizuri kwa ajili ya kutenda haki kulingana na ushauri na uamuzi wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, umekalia Kiti vizuri, Kiti kimekutosha na wewe umekitosha Kiti, lakini je, mbona huruma yako imezidi kiwango? Katika mjadala, Msemaji aliyenitangulia alisema kwamba, tusipofanya

utaratibu wa kubadilisha sheria hizi itakula kwenu, je, itakula kwenu hii iko katika utaratibu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nashukuru, naomba ufafanuzi kama utaendana na ushauri wangu basi nitaunga mkono hoja, lakini kwa muda huu, naomba niishie hapa. *(Makofi)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nakushukuru na nikupongeze kwa jinsi ambavyo unaendesha vikao vyetu hivi tangu jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee wangu Cheyo wakati anachangia alisema kwamba yeye angelikuwa na uwezo angelifuta kifungu, lakini mimi nataka niende mbali zaidi, kwenda kwangu mbali ni kumpa tahadhari Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mtoa hoja ambaye ni *AG* na ambaye tayari ameshasambaza *amendment* kwa baadhi ya vipengele, kaingia katika kipengele Na. 9 kinachohusu Mahakama pamoja na *Assessors*. Kipengele hiki sitaki nikuombe lakini nakuambia kiondoe!

*(Hapa Mwanasheria Mkuu wa Serikali alikuwa anatikisa kichwa)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Usitikise kichwa na unakiondoa kwa maslahi ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachomwambia *AG*, kama anataka kuitia nchi hii katika vita vya wenyewe kwa wenyewe, katika vita vya kidini, basi hii *amendment* aiache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeteua au tunachagua ma-*assessors* kwa ajili ya kumshauri mtoa hukumu, leo tunamwambia mtoa hukumu kwamba hutofungwa na yale mapendekezo ambayo watayatoa hawa ma-*assessors* na zaidi ina-*relate* katika dini ya kiislam lakini vilevile katika masuala ya kimila. Sasa unapoingilia masuala ya dini, ukaingilia na masuala ya kimila unategemea nchi unaipeleka wapi? Hili halikubaliki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mtoa hukumu awe ni Mkristo, ambaye ameleta mashtaka au anayeshtakiwa ni Muislamu, Muislamu anachojua ni kwamba hukumu zake zote na sheria zake zote tayari zipo katika Quran Tukufu, ambaye anaijua Quran Tukufu ni yule *assessor.* Sasa leo atakuja kutoa hukumu ambayo hatakubali ushauri wa yule *assessor,* itakuwaje? Hii itatuweka pabaya. Si ombi, Mheshimiwa *AG* hili liondoe kwa usalama wa nchi na usalama wa Chama chako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba anguko la CCM 2015 ni lazima lakini angalau hili anguko lisiwe kubwa. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rajab nenda kwenye mada.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende katika pointi yangu ya pili kuhusu suala la ardhi. Nina ushauri kama ambavyo Mama yangu Pindi Chana alitoa, kwa kweli kuna kila haja ya haya Mabaraza kuwepo chini ya Wizara ya Sheria na Katiba. Katika nchi yetu tumekuta kuna matatizo

mengi sana ya ardhi. Hivi sasa Mkuu wa Wilaya ana amri, Mkuu wa Mkoa ana amri, Halmashauri zina amri, kila mwenye dhamana yake ana amri mwenyewe katika suala la ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano mmoja hai wa kule Katosho-Kigoma, mwaka 1964, Serikali iliweka eneo kwa ajili ya upanuzi wa bandari huru, lakini ni mwaka juzi tu Serikali hiyohiyo bila ya kuondoa mipaka ile ya zamani ikaamua kuainisha mipaka mipya ambayo haikutolewa hata taarifa kwa wananchi. Kinachoendelea sasa hivi ni mamluki pamoja na mawakala ambao wamewekwa na Wizara inayohusika na suala hilo kuwabana watu, kuwadhulumu watu na kuwanyanyasa watu. Leo imefikia hadi pale Katosho watu hawazikani. Unapotaka kwenda kuzika, vita vinaanguka pale. Kwa kweli hili suala la ardhi, *AG* ilikuwa uende kwa mbali zaidi ili haya Mabaraza yawe na nguvu, ili wananchi wajue sasa wapi tunakimbilia. Vilevile hawa wana mabaraza, hebu na wao watengewe angalau posho nzuri. Suala la Katosho ni zito na tutakuja kulizungumza zaidi katika Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimalizie ajenda yangu ya tatu, ni suala la usafirishaji au uuzaji wa binadamu. Nilikuwa naangalia gazeti la Nipashe la leo, linasema kwamba, biashara kuu, biashara ya kuuza mabinti yashika kasi. Mheshimiwa *AG*, tuna tatizo la kuleta Sheria vipande-vipande. Mimi nataka nikupe tena ushauri mwingine nasaha mdogo, kwa vile, sasa hivi tunaunda Katiba Mpya, hivi huoni kwamba, iko haja na sisi kuzipitia hizi Sheria zetu zote, ili tuje tuendane na hii Katiba mpya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, hii biashara imekuwa kubwa kabisa. Hii biashara sio kwamba inafanywa kwa ajili ya kuchukua vijana hapa na kuwapeleka nje, lakini hata humu ndani ya nchi, biashara hii inafanyika. Wako mawakala ndani ya nchi sasa hivi wanawachukua vijana wetu, wanawapeleka kwa Wahindi, Wachina sasa hivi, wanafanyishwa kazi ngumu kweli kule, hawajui kitu wale vijana maskini. Nakubaliana sana na hili ambalo umeliweka Mheshimiwa *AG,* lakini nafikiri hii Sheria kuna haja ya kwenda mbali zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia na mimi kwenye Sheria hii ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali. Mimi nitaanza kuchangia Mabadiliko ya Sheria ya Mahakimu, Sura ya 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo ninaomba kuchangia hapa ni kwamba, Wizara hii ya Katiba na Sheria, haina Sera rasmi ya kuajiri Watumishi, Mahakimu, Majaji, haina Sera rasmi? Leo kuna watu wameajiriwa kama Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, wana *Masters*, kuna watu wameajiriwa kama Mahakimu wa Mahakama za Wilaya, wana *Diploma* yaani sifa ya mtu kuwa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo na kuwa Jaji ni sawa, hakuna tofauti ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna *confusion* nyingine, mwaka jana hawahawa Mahakimu ambao wamewaajiri Wizara ya Katiba na Sheria, kuna watu ambao wamemaliza

*Law School* haohao, kwa hiyo, kuna mtu ni Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, ameajiriwa mwaka jana, mmoja ana *Masters,* mwingine ana *Degree,* mwingine ana *Law School.* Sasa sijui mnapimaje maslahi yao, mnapimaje utendaji kazi wao? Kwa hiyo, hakuna Sera Maalum ya kuajiri Mahakimu na Majaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya mapendekezo yanayoletwa hapa yanaleta *confusion,* yataleta vurugu kwenye Mahakama. Mapendekezo yanayoletwa kubadilisha maana ya Hakimu, maana yake tutakuwa na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wa aina mbili; Hakimu wa kwanza atakuwa anaitwa *Primary Court Magistrate* na Hakimu wa pili atakuwa anaitwa *Resident Magistrate,* kutakuwa na Mahakamimu wa aina mbili wa Mahakama za Mwanzo kwa mapendekezo haya. Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ambaye atakuwa *Resident Magistrate,* atakuwa na *jurisdiction* ya kusikiliza kesi sawa na Hakimu wa Mahakama ya Wilaya, kwa haya marekebisho ambayo ameyaleta Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ndio itakavyokuwa; watakuwa wanafanya kazi namna gani, hajatueleza itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili kwenye hoja hiyohiyo, Mahakimu hawa wa Mahakama za Mwanzo, bado wapo wenye Diploma, wanaitwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, wenye *Degree* yaani *Resident Magistrate,* ana *Degree* anaitwa *Resident Magistrate,* sio *Primary Court Magistrate,* ambaye sijui hata rufaa yake inakwenda wapi? Kwa sababu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hajatueleza Mahakama zipi zitakuwa zinaweza kusikiliza kesi zipi? Kwa mfano, wananchi hawatakuwa na uwezo wa kujua kwamba, huyu ni Hakimu wa Mahakama

ya Mwanzo, ambaye hakuwa na *Degree,* watakuwa hawajui wala hawawatambui kwa sababu, hawana nembo na wala hawatajua kwamba, huyu ni Hakimu mpya sasa mwenye *Degree* ambao mamlaka yao ni tofauti na majina yao ni tofauti na kazi zao ni tofauti. Sasa nataka wakati anahitimisha hapa, anipe majibu sahihi kwamba, Hakimu mwenye *Degree* anayeitwa *Resident Magistrate,* kazi zake zitakuwa ni zipi na huyu wa kwanza ambaye ana *Certificate* anaitwa *Primary Court Magistrate* atafanya kazi zipi na wananchi watazitambuaje hizi Mahakama zinazoongozwa na watu tofauti, wenye mamlaka tofauti? Hilo ni moja, najua ni pana sana kulielezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili. Hizi *amendment* zinatutengenezea kuwa na hukumu za aina mbili Mahakamani yaani Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, kwa mujibu wa *Schedule of Amendment* ambayo ameileta Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lugha ya Mahakama za Mwanzo itakuwa aidha Kiswahili *or English.* Sheria ya zamani ilikuwa inasema kwamba, lugha ya Mahakama za Mwanzo itakuwa ni Kiswahili. Marekebisho haya yanasema itakuwa ni Kiswahili au *English* kwa hiyo, maana yake ni kwamba, kutakuwa na Hakimu wa Mahakama za Mwanzo ambaye anajisikia kuandika Kiswahili anaandika, anayejisikia kuandika Kingereza anaandika. Kwa hiyo, tutakuwa na hukumu za aina mbili, ndio maana yake; ndio mapendekezo anayotuletea Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamekuwa wanazungumza hapa Bungeni kutaka lugha za Mahakama ziwe Kiswahili mpaka Mahakama Kuu lakini kwa mabadiliko haya tunarudisha, Mahakama za Mwanzo zilikuwa zinatumia Kiswahili, sasa tunawapa nguvu sasa watu

waanze tena kutumia Kingereza kuanzia Mahakama za Mwanzo. Sasa sijui Wabunge tulioko humu ndani, sijui mmetumwa na wananchi wenu mje mbadilishe hata lugha za Mahakama za Mwanzo ziende tena kwenye Kingereza ambacho hawajui. Hukumu za Mahakama za Wilaya zinaandikwa kwa Kiingereza, hawawezi kuzisoma, sasa mmeona hiyo haitoshi, muwapelekee mpaka kwenye Mahakama za Mwanzo; ndio mapendekezo anayotuletea Mwanasheria Mkuu wa Serikali; ndio *Schedule* yako hiyo, unataka mpaka *Primary Court* watu watumie Kingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye Sheria hiyohiyo, napenda kupata ufafanuzi wa Serikali, rufaa zitakuwaje? Rufaa inayotoka kwa *Resident Magistrate* ambaye yuko kwenye *Primary Court* kwenda kwa Hakimu wa Wilaya, *District Magistrate,* nataka unifafanulie hukumu zitakuwaje? Je, mtu aliyepeleka kesi yake kwa Hakimu, *Resident Magistrate* ambaye yuko kwenye *Primary Court,* mwenye *Degree* ambao mmewaanzisha, hukumu yake inakwenda Mahakama Kuu au inakwenda wapi? Nataka majibu sahihi. Je, huyu ambaye amepeleka kesi yake kwa Hakimu huyu mwenye *Certificate,* hukumu yake anaipeleka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipitia hii Sheria kwa umakini sana, nimeona ina mapungufu makubwa na haijaweza kutatua lengo la Serikali la kutaka hao Mahakimu walioajiriwa wapya waende kufanya kazi zao sanasana inaongeza *confusion.* Itaongeza matatizo kwenye utendaji kazi wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, nataka kujua ameleta *amendment* kuhusu Wazee wa Mabaraza, *Assessors.* Sasa nataka kujua, huyu Hakimu mwenye *Degree* ambaye mmemweka *Primary Court,* mnataka awasikilize *Assessors* kwa kesi zipi? Kwa sababu na yeye ni *District Magistrate,* kwa kesi zipi anakuwa *bound?* Nataka majibu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niiache hiyo hoja, nije kwenye hoja nyingine. *Amendment* ya Sheria hii, mimi sipingi mabadiliko haya ya kutaka Majaji wote wa Mahakama Kuu wasikilize kesi za ardhi, hakuna mtu anayekataa kwa sababu zitatupunguzia malalamiko mengi ambayo yamekuwepo. Malalamiko yamekuwa lakini yanasikilizwa Kitengo kimoja cha Mahakama Kuu cha Ardhi, hilo sipingi. Shida kubwa ni kwamba, kesi nyingi za ardhi zimeongezeka na Serikali mmekuwa hamtaki kuleta mabadiliko ili kesi hizi ziweze kwenda kirahisi kuanzia Vijijini mpaka juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza haya bado ni machache, leo amezungumza hapa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwamba, kesi hizi ziendelee huko, mashauri haya yaendelee kwenye Mabaraza ya Ardhi, mimi binafsi sikubaliani naye. Amesema bajeti ni ndogo na sidhani kama ni rahisi ninyi *Judiciary* kwa bajeti yenu ilivyo kidogo na Wizara yake ilivyo na bajeti kidogo, mpaka tutakapomaliza kujenga majengo ya Mahakama hizi, Mabaraza haya kila Wilaya, kwamba, ndio wananchi wapate haki sasa ya kupeleka mashauri yao kwenye Mabaraza ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa kuwapa ushauri, kesi za ardhi zirudisheni kwenye mfumo wa Mahakama. Kama mmekubali kesi za ardhi kuwa kwenye mfumo wa Mahakama katika ngazi ya Mahakama Kuu, kitu gani kinawafanya ninyi mkatae kesi za ardhi zisirudi Mahakamani kuanzia Mahakama ya Mwanzo? Mnaajiri mtu mwenye *Degree* amesoma *Land Law,* ambaye ana uwezo wa kutatua migogoro ya ardhi, mmempeleka *Primary Court,* lakini hamumpi mamlaka ya kutatua migogoro ya ardhi kule kwenye *Primary Court,* mnapeleka kwenye Mabaraza ya Kata ya Ardhi, ya watu ambao hawajui taratibu za maamuzi, hawajui Sheria wala hamjawapa mafunzo yoyote ila kuzipeleka kwa hawa watu ambao mnawaajiri, ambao wamesoma Sheria za Ardhi, hamtaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ushauri mwingine wa bure kwa sababu kujenga majengo nchi nzima ni gharama, ajirini watu 133 kwenye kila Mahakama, ambao watakuwa ni Mahakimu wanaojishughulisha na kesi za ardhi peke yake, hiyo ndio itakuwa suluhisho. Lakini huku chini wanaanza watu wanachakachua hovyohovyo kuanzia kwenye Baraza la Kata, inakuja huku tena kuna *confusion,* kesi ziko kwenye Wizara zaidi ya mbili; TAMISEMI wanaanzanazo, zinatoka TAMISEMI mnaleta Wizara ya Kazi na Maendeleo, inakuja *High Court* mnaleta *Judiciary* – Wizara ya Katiba na Sheria. Hii ni *confusion,* hamuwezi kutatua matatizo ya ardhi kwa namna hii na kama mnasubiri kwamba, mtatatua matatizo ya ardhi siku mtakapomaliza kujenga nyumba za Mabaraza haya kwenye kila Wilaya, mjue wananchi watakuwa wameshahangaika vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, chukueni ushauri wangu huu wa bure. Ajirini watu, tuna watu wengi nchi hii wanaomaliza Shahada za Sheria, ni zaidi ya 2,500 kwa mwaka. Chukueni watu 200 tu, wekeni kwenye Mahakama za Wilaya, kazi yao iwe kushughulikia kesi za ardhi, *very simple,* rahisi sana. Haihitaji kuchanganyikiwa sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria nyingine hizi wamezijadili wengine. Mimi nilikuwa nimejikita kwenye maeneo hayo zaidi, lakini ninaomba majibu kwa mara nyingine na hili sio jambo la kwanza ninaliomba, Bunge hili tumekuwa tunafanya marekebisho ya Sheria kila wakati *as if* Serikali haina *program* ya kubadili Sheria. Ni mwaka jana tu tumefanya mabadiliko ya *Anti-Money Laundaring Act,* mwaka huu mnatuletea mabadiliko mengine, hivi mlikuwa hamyajui haya mambo mwaka jana?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mkosamali.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Miezi miwili mitatu iliyopita, mlikuwa hamyafahamu haya mambo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali, kaa chini. Mheshimiwa Christina Mughwai, ajiandae Mheshimiwa Assumpter.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu katika Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita zaidi katika marekebisho yanayolenga au yanayohusu kiwango cha elimu katika Mahakama za Mwanzo, kama ambavyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali alivyotwambia. Marekebisho haya sasa yanalenga kuwaruhusu Mahakimu wenye kiwango cha elimu ya Shahada ya Chuo Kikuu ili waweze kufanya kazi katika Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wote tunavyojua, mwaka jana, zaidi ya Mahakimu 300 waliajiriwa ili wakafanye kazi katika Mahakama za Mwanzo. Mahakimu waliajiriwa zaidi ya 300 wenye kiwango cha elimu cha Shahada ya Chuo Kikuu, mimi ambaye sio Mtaalamu wa Sheria nilidhani kwamba, wakati Mahakimu hawa wanaajiriwa na kuapishwa, kulikuwa kuna Sheria inayowaruhusu kwenda kufanya kazi, lakini nashangaa leo hii, miezi mingi baadaye ndio Serikali, inakuja ikitwambia kwamba, turekebishe Sheria, ili Mahakimu wenye Shahada ya Kwanza ya Chuo Kikuu waweze kufanya kazi katika Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaihoji Serikali, ni kwa nini waliajiri Mahakimu wengi kiasi hicho, ilhali wakijua Sheria ilikuwa haiwaruhusu kwenda kufanya kazi katika Mahakama za Mwanzo? Je, tangu kuajiriiwa huku na kuapishwa, Mahakimu hao wamekuwa wakifanya kazi gani katika maeneo ya kazi waliyokuwa wamepangiwa? Napenda kujua iwapo Mahakimu hao wapya walioajiriwa

mwaka jana, wamekuwa wakilipwa mshahara? Kama wamekuwa wakilipwa mshahara, je, wamekuwa wakilipwa mshahara kwa kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atakapohitimisha, atwambie ni kiasi gani cha fedha mpaka leo hii tunapojadili kuruhusu Mahakimu hawa wakafanye kazi, kiasi gani cha fedha kimetumika kuwalipa mishahara watumishi ambao walikuwa hawafanyi kazi, ilhali kuna malalamiko mengi ya watumishi ambao wako makazini katika sehemu mbalimbali, wenye mapunjo mbalimbali na stahili zao mbalimbali na hawajaweza kulipwa malipo yao wakati huohuo Serikali ina hela ya kuwalipa Mahakimu ambao wamekuwa hawana kazi ya kufanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini marekebisho haya pia yanayoletwa na Serikali, yanalenga kuwaruhusu Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu Wakazi waweze kufanya kazi katika Mahakama za Mwanzo lakini wote tunajua kwamba, huko katika Mahakama za Mwanzo, iwapo Sheria hii itapitishwa, kuna Mahakimu ambao wana viwango vya elimu vya Cheti na Diploma. Sasa wanaenda kuchanganyika na Mahakimu ambao wana *Degree* au wana Shahada ya Kwanza ya Chuo Kikuu; mimi naona suala hili litaleta mkanganyiko na litaathiri utendaji na maamuzi katika Mahakama za mwanzo.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwaje kwa mwananchi mwenye kesi katika Mahakama ya Mwanzo kumkubali Hakimu mwenye ngazi ya elimu ya cheti au diploma afanye maamuzi ya kesi yake ili hali Sheria sasa inatamka kwamba kiwango hicho cha elimu hakitakiwi

katika Mahakama za Mwanzo. Suala hili litaleta mkanganyiko na litaathiri kwa mawazo yangu maamuzi katika Mahakama za Mwanzo na wale wananchi walio wengi hawataweza kupata haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vyuo kama vile chuo cha Lushoto ambacho vinaendesha kozi mbalimbali za ngazi ya cheti na ngazi ya stashahada na kuna wanafunzi wanaendelea na masomo mbalimbali leo hii Serikali inatuletea Muswada wa mabadiliko ya Sheria ukisema kwamba Mahakimu wote sasa kuanzia ngazi ya chini ya Mahakama ya Mwanzo wanatakiwa wawe na *degree* ya kwanza. Sasa tunawaambia nini wanafunzi hawa ambao wako katika hatua mbalimbali za masomo ya kiwango cha chini ya Shahada ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejipanga vipi kutokana na wingi wa Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Mwanzo zimeenea nchi nzima. Je, Serikali ina uhakika kwa marekebisho haya Mahakama zote za Mwanzo zitaweza kuwa na Mahakimu wenye kiwango cha elimu ya shahada ukizingatia matatizo yaliyopo katika vyuo vikuu vya nchi yetu ambapo wanafunzi wanashindwa kuendelea na masomo kutokana na kushindwa kulipa ada, kujigharamia gharama nyingine za masomo. Je, tutawapata wapi Mahakimu hawa wengi kiasi hiki wenye *level* ya Shahada ya kwanza ili wakatumikie katika Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile ni kweli kwamba, Idara ya Mahakama sasa katika utaratibu wake wa ajira hawahitaji kiwango cha elimu ya chini, Mahakimu wenye cheti na *Diploma*. Ni kweli kwamba kesi zote

ambazo zimekwenda kwenye Mahakama zetu za kwanza zinahitaji Hakimu mwenye uelewa wa Chuo Kikuu? Naomba Serikali itakapokuja ilete ufafanuzi wa hoja hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema Mahakimu waliopo sasa hivi wenye kiwango cha elimu ya cheti na diploma wataendelea na kazi hiyo, mpaka watakapokwisha, sasa sijaelewa kwanza wako wangapi ili tujue watakwisha lini na wale ambao wangependa kujiendeleza Serikali inawawekea utaratibu gani ili kuwafanya waweze kujiendeleza kuendana na kiwango cha elimu kinachopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona tatizo la Mahakama zetu ni miundombinu na vitendea kazi vibovu, ni bajeti finyu inayoletwa na Serikali na siyo kiwango duni cha elimu kwa Mahakimu wetu. Kwa hiyo, ningependa kwanza tuboreshe maeneo ya kazi na vitendea kazi katika Idara za Mahakama, tuboreshe mishahara na marupurupu, tuboreshe makazi ya Mahakimu na Maofisa katika Idara za Mahakama. Kwa sababu leo hii unaposema vijana wanaomaliza chuo kikuu waliosoma kwa shida waende wakafanye kazi katika Mahakama za Mwanzo na wote tunajua zina hali gani, je, Serikali ina uhakika vijana hao watakwenda kukaa katika hizo Mahakama za Mwanzo au mtazalisha Mahakimu ambao baadaye wataenda kuomba kazi katika Idara zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mengi yameshasemwa na Wabunge waliotangulia, naunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani na naomba mapendekezo yaliyoletwa na Kambi hii yaweze kupatiwa majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa kumalizia nitende haki kwa wananchi wa Mkoa wa Singida kwa kusema kama alivyosema Mheshimiwa John M. Cheyo, kuna tatizo kubwa la chakula, wananchi hawana chakula na maeneo mengi ya Mkoa wa Singida hususan Halmashauri ya Wilaya ya Singida chakula cha msaada hakijakwenda mpaka sasa hivi, naomba Serikali ifanyie kazi suala hili kama jambo la dharura. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Assumpter N. Mshama na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu ajiandae.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2012. Kwanza kabisa, naomba nianze kwa kushangaa na unikubali nishangae. Nashangaa kuona kwamba, kila Mpinzani lazima apinge hata kitu ambacho anaambiwa hiki ndicho, anasema sicho. Ukimwambia ni nyekundu atasema ni nyeusi, lakini katika imani yangu wanasema wana masikio lakini hawasikii, wana macho lakini hawaoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangazwa na jambo moja, msemaji mmoja alisema kwamba Miswada hii inachelewa sana, mlikuwa wapi? Ilipokuja sasa kwa kuwahi ikasemwa mnaharakisha mnakimbilia wapi? Hivi tutoe lipi sasa, tuwe tunaileta au tuwe tunaiacha. Kwa hiyo, nataka niwatahadharishe Watanzania yamkini hawaelewi kwamba humu kuna kinga, mtu anaweza kusema lolote, lakini akitoka nje haruhusiwi kusema. Kwa maana nyingine, mtu

anasema tu ili apate *credit* huko nje, lakini anasahau kwamba amepotosha wananchi. Hivyo, naomba wananchi wa Tanzania wawe wanasikiliza halafu wanachambua, baadaye wanajua pumba na mchele ni upi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wameshachoshwa na kusikia habari ambazo siyo zenyewe. Mfano, mtu anathubutu kusema, Miswada hii iliyoletwa hapa haina tija. Hivi kweli hivi tunavyoongea hakuna tija, kubadilisha sheria kwa mfano ya Mahakama hakuna tija? Yaani kwa kweli siwaelewi, lakini nawashukuru wana Misenyi wanawaelewa na ndiyo maana kule wanajua Chama cha Mapinduzi.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa mujibu wa kanuni ya 68(1) na nakwenda moja kwa moja sasa kwenye Kanuni ya 64(1)(b) ambayo inasema kwamba naomba ninukuu kwa ridhaa yako: "Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala". Mzungumzaji Mheshimiwa Mbunge hapa ambaye anaendelea ametoka kabisa kwenye mada na anaanza kujadili mambo hayako kwenye mada. Naomba arudi kwenye mstari ili ajadili hoja na siyo kupiga bla bla hapa.

**MWENYEKITI:** Mimi sijamwona mchangiaji aliyetoka nje ya mada, Mheshimiwa endelea!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ameipata ndiyo maana. Kwanza, napenda

kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi wanayoifanya, katika hili nawapongeza sana katika kuleta Miswada hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Muswada wa Sheria ya Kusimamia Umiliki wa Ardhi katika Vijiji vilivyokwishaanzishwa. Kuna faida kubwa katika kuwa na Mabaraza haya. Napenda tu ieleweke kwamba, hasa katika tatizo la ardhi mara nyingi linakumbana na watu kwa mipaka na mipaka, mtu kuuza kitu ambacho siyo chake, lakini tukiwa na Mabaraza kule chini wataweza kuelewa na wana historia ya mahali pale kujua kwamba nani mwenye kipande hiki na mpaka wa mtu ni wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nasisitiza habari za baraza ziendelee kwa sababu zinaeleweka vizuri. Nataka nikutolee mfano, kwetu kuna watu walikuwa wanagombania mti, mti tu, ambao kwenye Kabila letu unaitwa *kigabiro* yaani mti mkubwa sana. Huo mti ulipotaka kuanguka uliangukia kwenye upande mwingine, lakini watu waligombana kwa sababu kuna kasehemu ka ardhi. Aliyemaliza tatizo hilo ni Mabaraza lakini mtu wa Biharamulo hawezi kujua huu mti ulipokuwa pale Misenyi nani aliupanda. Kwa hiyo, nasisitiza, historia inajulikana na wale watu wanaokaa mahali pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda la kushauri, tunapokuwa na Mabaraza haya wanapomaliza isiende moja kwa moja *High Court*, waende kwenye Mahakama ya Mwanzo ndipo waweze kwenda katika hatua nyingine. Unapotoa mtu kule Misenyi kuleta hoja yake *High Court* wakati mwingine ni gharama kubwa, lakini nadhani tukiajiri

watu waliosomea Sheria ya Ardhi wanaweza kusaidia katika maeneo yale ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Mabaraza yaendelee. Lakini hivi mtu unapomweka pale tangu asubuhi mpaka jioni anatetea labda haki ya mtu na anaondoka pale na miayo, hivi anaweza kufanya haki? Lazima tutenge kiposho kidogo sasa cha kuwapa watu wa Mabaraza ili wasiweze kuhongwa na waweze kusimamia haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine mtu ana *lobby* kwa elfu kumi tu, hivi tukiweza kusema mchana mmoja ni elfu kumi kwa mama au kwa baba yule wa pale katika maeneo husika, si anatoa haki na huku moyo wake ukifurahi. Ninachoomba hatua ya pili isiwe Mahakama Kuu bali iende katika Mahakama ya mwanzo kama usuluhishi umeshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya pili, marekebisho ya mafao ya wastaafu wa utumishi wa umma hasa katika Polisi au majeshi yetu. Kwa kweli naomba tufanye iwe *uniform*. Unakuta Polisi na Magereza na Jeshi wanapewa viwango tofauti. Kwa mfano, kwenye miaka, kijana wa miaka 45 unapomwambia kazi basi, aende wapi, kijana wa miaka 50, mimi hapa nina miaka 52 hivi leo ukiniambia kazi basi, kweli utakuwa umenitendea haki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu tuangalie na iwe *uniform* kama ni miaka 50 mpaka 55, iwe ni kwa wote siyo Polisi wa Magereza au Polisi wa Polisi iwe wote wawe na kiwango kimoja na kama kuna sababu yoyote ya mtu kuendelea kubaki kazini isiangaliwe kwa

sababu eti ni Sajenti au huyu ni Meja au huyu ni nani, umri ndiyo una-*matter* katika kufikiri na kutenda kazi. Kwa hiyo, naomba kama ni kustaafu, wastaafu wote kwa kiwango kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mahakimu na Mahakama, kweli hii ni changamoto, lakini naomba niulize hivi, kote huko tulikotoka tunafanya kazi mlikuwa mna *section* gani ambayo ni watu wa *degree* tu, ni watu wa *masters* tu, ni watu wa *Ph.D.* tu hivi hawa watu wakichangamana kuna tatizo gani au ndiyo ile sera ya kupinga tu hata kama unaona *blue* unasema ni *black?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana huko waliko, wanaweza kufanya kazi bila tatizo lolote na sasa hivi ninachokiomba Serikali sana sana, nafikiri kwamba, watu wasiwe *phased out* kama vile unapiga mstari, hapana twende pole pole kama tunaweka wenye *degree* tuanze hawa hawa pole pole na kama ambao hawana *degree* wasomeshwe na wakopeshwe mishahara yao ili waweze ku-*qualify* kuendelea katika maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema sasa itatungwa sheria kwamba, kama wewe huna *degree* nyumbani mimi nadhani hiyo siyo sawa. Kama huna *degree* na bado unataka kuendelea na kazi wapelekwe wasome na Serikali iwalipie hata kuwakata katika mishahara yao kama mikopo ili waweze ku-*qualify* kuendelea katika kazi zao. Sioni tatizo lolote la kuwa na mtu mwenye *degree* kukaa na mtu mwenye *certificate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine wana *degree* wakikaa na *certificate* wanawazidi maamuzi na uwezo wa kufikiri. Kwa hiyo, wakati mwingine watu wamekaririshwa ama kuwa na *masters,* lakini ukimwangalia na mwenye *degree* moja hakuna tofauti yoyote, maadam wanasimamia sheria. Lakini niiulize swali kwa Serikali, nimekuwa nikiangalia utaratibu huu wa Mahakama, jamani hali wanayofanyia kazi Mahakimu haipendezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kwenye Mahakama yangu ya Mwanzo ya Misenyi pale, jamani ukienda pale hata huyu kuondoka kulewa ni kwa sababu anachanganyikiwa kutokana na hali ilivyo. Unaingia pana vumbi, mvua ikinyesha unanyeshewa na inabidi ubebe dawati utoke mahali ulipo kwa sababu labda mafuriko yameingia ndani ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa nini tunaandaa sera nzuri ya kupeleka watu wenye *degree,* basi tuandae na sehemu za kufanya kazi zifanane na *degree* zao. Lakini hivi kwenda ilivyo, sisemi hata *degree* siyo *degree* tu, mtu na utu wake ana daftari kuandika wanatumia daftari hana faili, hana mahali pa kuweka kumbukumbu za hukumu, hivi hiyo Mahakama ya Mwanzo tunaitendea haki jamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwanasheria Mkuu anapokuja hapa atuambie mikakati aliyonayo kwa ajili ya kurekebisha utaratibu wa kazi wa Mahakama ya Mwanzo, hususan katika utaratibu wa kiofisi. Ofisi zao zinatia aibu, mtu anakuja na kesi ya mabilioni, unamwomba karatasi, hivi atakupa haki kweli, naomba sana, Serikali ina mipango mizuri ya kuweka wasomi kule chini na ambavyo ndivyo ilivyo hata wakati tunaanza nchi hii walikuwepo ma-

*engineer* wawili tu, lakini leo kuna ma-*engineer* kila kona, hivi wote waajiriwe Dar es Salaam, waajiriwe mjini wasipelekwe vijijini, nadhani suala siyo *degree,* suala ni kazi kutendeka kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoomba kama mtu hana usafiri, hata kapikipiki basi aweze kununuliwa, anategemea mwenye kesi ampitie, amlete Mahakamani kama mvua zinanyesha, halafu akifika pale dawati halipo, limebomoka upande, hana mahali hata pa kuficha hata *document* ya hukumu aliyotoa, akiomba tu karatasi ya kuandikia alete mshtakiwa, hivi kweli hiyo ni Mahakama kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali katika hilo na mimi nachangia niiombe sana sana iziangalie Mahakama za Mwanzo kwa kuzipa vitendea kazi na si kuzitelekeza na hata kubeba vijana hawa watakapokwenda kule pia na wao wanaielewa hali ya nchi, lakini tafadhali sana wasiende pale wakakatishwa tama, mwisho wakaishia kunywa pombe kwa sababu ya *frustration*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naunga mkono hoja mia kwa mia na naomba hoja hizi zitekelezwe. Ahsante kwa kunisikiliza.

**MWENYEKITI:** Nashukuru, Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa Mchungaji Peter S. Msigwa, ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia marekebisho haya ya Sheria Mbalimbali yaliyowasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na-*declare interest,* ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi na naomba niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, nitajadili au nitachangia marekebisho ya Sura ya sita yanayohusu marekebisho ya Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho haya yalihusisha wadau, tulijadiliana kwa kina na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na niseme hayana nia ya kulifunga Bunge. Lakini utakubaliana na mimi kulikuwa na mkanganyiko wakati Katiba imempa mamlaka *CAG* kuwasilisha ripoti tarehe 31 Machi, kwa Mheshimiwa Rais na wiki ya kwanza iwasilishwe Bungeni, maana yake ni mwezi wa Nne, ni kipindi ambacho pia Kamati zetu *Oversight Committees* za Bunge zinawasilisha ripoti zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi hiko tunapokuwa tunajadili taarifa za Kamati zetu na Mdhibiti na Mkaguzi amewasilisha ripoti ya mwaka ambao haujajadiliwa na Kamati zetu, kwa kweli pale kulikuwa na mkanganyiko. Tunapojadili tulikuwa tunakwenda kwenye taarifa ambayo imewasilishwa mezani. Kwa hiyo, marekebisho haya yanalenga kutoa fursa kwamba, tunapojadili Kamati tujadili ya Kamati, lakini ile taarifa inayowasilishwa ili baadaye iende kufanyiwa kazi na Kamati zetu, kuijadili kwa wakati ule inakuwa hatuitendei haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ilijitokeza Bunge la mwezi wa Nne, pamoja na nia nzuri iliyokuwepo Bunge la mwezi wa Nne mwaka jana ya kuifanya Serikali iwajibike vizuri na kweli iliwajibika, lakini *burden* yake au madhara yake ni

makubwa siyo kwamba tu tunawasaidia wananchi, tunasema, lakini tuone athari zake kwa *donors* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono marekebisho au nyongeza ya Kifungu cha pili katika kifungu 39 ya kwamba taarifa hiyo lazima ijadiliwe kwenye Kamati. Lakini pia kuna tatizo gani wakati Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawasilisha ripoti yake na Serikali nayo ikawasilisha majibu yake yakajadiliwa, kwa sababu mara zote tumekuwa tukiona majibu ya hoja za Mdhibiti, Serikali inawasilisha na tunawekewa kwenye *pegion*. Kwa nini tunapopewa fursa leo kwamba, tujadili tena majibu haya, tuone hivi ni kwa nini kwa wakati ule Serikali ilishindwa kujibu, lakini leo inajibu, tunaogopa. Lazima tuhoji, sioni matatizo! Tumepewa fursa zaidi kuona Serikali inasema hivi na CAG amesema hivi, lakini sisi majibu yetu ni haya, kwa nini tuiogope hiyo fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mapendekezo hayo kwamba baada ya kuona tu kwenye *pigeon,* haitoshi, yajadiliwe hapa ili umma wa Watanzania wafahamu hayo majibu, kwa nini tunaangalia upande mmoja tu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu siyo peke yake ya kuanika maovu, ni ushauri pia. Katika ripoti yake mara nyingi pia kuna ushauri ambao ama kwa hakika nyingine inatafsiriwa vibaya, kwa hiyo, lazima Serikali ipate fursa ya kujibu, tatizo liko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwatoe wasiwasi Wabunge, hatujafungwa, tunapata fursa ya kusema *CAG* amesema hivi, Serikali imejibu nini, tunaona amesemaje na kama tunaona kabisa kwamba hili si sawasawa tunasema. Tumepata fursa ya kupima kama ambavyo tunatoa hoja binafsi hapa, upande wa Serikali nao unajibu. Sasa leo hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa nini Serikali isitoe majibu ya kuingia ndani ya Bunge ili yajadiliwe kwa mujibu wa sheria na kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono na wala sioni wasiwasi, lakini pia mabadiliko ya kwamba Mdhibiti na yeye kwenye ripoti yake aingize utekelezaji wa majibu ya Serikali, nadhani siyo utaratibu mpya kwa sababu kwenye *management letter* zile ambazo zinaletwa na Mkaguliwa zinaainisha, *CAG* anaainisha kabisa pale, hoja ilisema nini, majibu ya Mkaguliwa na *comments* zake. Kwa hiyo, si jambo la ajabu kwamba tutajadili ndani ya Bunge hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea ni kwamba, ile ripoti anayoleta ndani ya Bunge ni *general report,* ndiyo ambavyo kwa sababu ni *summary* ya matukio yote, ndiyo yaingize majibu ya Serikali, lakini kwenye *individual report,* hata ukienda kwenye Halmashauri zetu, anaingiza majibu, Halmashauri imesema nini au Wizara imesema nini, CAG anasemaje kuhusu lile jambo, kwa hiyo siyo jambo jipya, lakini limehalalishwa kwamba na sisi Bunge tujadili hayo majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba, nadhani mapendekezo haya hayana nia ya kutufunga midomo, tuyapitishe, tutajadili kwenye Kamati zetu, lakini pia hata

kanuni za Bunge zinasema, si vyema kuwahisha mijadala, vile tulivyokuwa tunajadili, Kamati inaleta ripoti ya mwaka uliopita na *CAG* analeta ya mwaka huu, halafu tunajadili zote kwa pamoja, tulikuwa tunawahisha mijadala. Kwa hiyo, nadhani hii imeipata nguvu kanuni zetu za Bunge, tusiwahishe mijadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono, lakini pia kama nilivyosema *CAG* siyo kazi yake kusema kwamba jambo fulani limeharibika, pia kutoa ushauri. Kuna hoja zinakuwa za kutoa ushauri, deni ya Taifa, Serikali haijakatazwa kukopa, lakini deni linapokuwa kubwa, anatoa ushauri, lakini tunavyojadili hapa ni ufisadi, ni ufisadi wakati siyo kweli, *CAG* amesema deni linaongeza, tafuteni mikakati mingine, hapo siyo kwamba amesema ufisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, au katika misamaha ya kodi, misamaha ipo kwa mujibu wa sheria, lakini lazima aseme mimi navyoona misamaha inaongezeka, hebu angalieni hiyo sheria, aidha mpunguze misamaha, lakini si kwamba kuna ufisadi kwenye misamaha. Kwa hiyo, naunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, naunga mkono pia marekebisho ya hizi kesi za ardhi, badala ya kitengo cha ardhi peke yake kujadili kesi za ardhi au masuala ya ardhi, naipongeza Serikali kwa kuona kwamba Mahakama Kuu yoyote inaweza ikajadili. Kwa sababu kuna malalamiko mengi na kesi nyingi ambazo zimepelekwa zinazopitiwa na Mabaraza yetu ya Wilaya, wananchi wanapokataa rufaa kwenda Mahakama Kuu ya Ardhi, kwa kweli haki inachelewa, ni zaidi ya miaka miwili au mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashukuru Serikali kwa kuliona hili na kuleta mapendekezo kwamba, zinaweza pia zikapatiwa au maamuzi yanaweza yakafanyika katika Mahakama zingine. Naamini kwamba lengo la marekebisho haya ni zuri na kumpa fursa Mtanzania apate haki kwa sababu haki nayo inayochelewa, si haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachangia kwenye Mabaraza ya Kata. Sisi tunaokaa Wilayani, tuna matatizo na Mabaraza ya Kata, pamoja na kuwa yanafanya kazi nzuri, lakini Mabaraza haya yamepewa kazi nyeti, lakini hakuna uwezeshaji. Unakuta Mabaraza yale hayana posho, sasa unataka mtu atoe haki kwa masuala ya ardhi na tunajua masuala ya ardhi yana thamani, lakini mwisho wa siku na ndiyo maana Mabaraza mengi yanatuhumiwa kwamba mengi yanakula rushwa, lakini kwa kweli kwa uhalisia wake mazingira wanayofanyia kazi ni magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na marekebisho haya yanayopendekezwa, lakini naiomba Serikali hebu iyatazame haya Mabaraza, tutakuwa tunayalaumu, lakini kwa kweli kama kesi zote hizo ziende kwenye Mabaraza ya Wilaya, Mabaraza yenyewe katika Mikoa yetu si kwamba kila Wilaya ina Baraza. Kwa kweli kama nilivyosema, haki inayocheleweshwa nayo si haki, Watanzania watakosa fursa ya kupata haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza tuangalie hata *composition* ya Mabaraza ya Kata yale, hata uchaguzi wa wajumbe wa Mabaraza yale, pengine Mwenyekiti wa Baraza lile awe ni mwajiriwa. Tumewapeleka hao Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ambao

watakuwa na weledi mkubwa na wasomi, lakini pia niwashukuru Mahakimu waliokuwa kwenye Mahakama za Mwanzo wametusaidia, kwa sababu Mahakimu ambao walikuwa kwenye Mahakama za Mwanzo wamefanya kazi kubwa, wamepunguza mlundikano wa kesi katika ngazi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoomba, pengine nisingeweza kuzipata mzigo Halmashauri, lakini labda pengine Serikali izielekeze Halmashauri kwenye bajeti zao iweze kuyasaidia yale Mabaraza ya Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Mahakama za Mwanzo, kwa kweli zimechoka. Wenzangu wamesema, tunawapeleka wasomi kwa nia njema, kwa nia kwamba pengine watapunguza kwa kasi au watakuwa na kasi zaidi ya kushughulikia malalamiko au kesi mbalimbali. Lakini mazingira yao, Mahakama za Mwanzo zingine ziko mbali na miji. Serikali imeangalia sehemu ambazo watakuwa hao Mahakimu au ndiyo itabidi aishi mjini, kila siku aende akasikilize kesi kwenye maeneo hayo, kwa kweli itakuwa ni gharama kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ufinyu wa bajeti, niipongeze pia Wizara ya Sheria na Katiba, kwa mikakati waliyokuwa nayo ya ujenzi na ukarabati wa hizo Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipongeze wazo walilokuwa nalo kwamba na Halmashauri pia kwa sababu Mahakama zinatusaidia kuamua mashauri mengine ambayo yanahusisha Halmashauri zetu, kwa mfano, mashauri yanayohusu uvunjani wa sheria zinazolenga labda

kuongezea mapato Halmashauri, niziombe Halmashauri tusione vibaya kwenye bajeti zetu angalau kuingiza ukarabati mdogo hata kupaka rangi tu, tusisubiri Serikali Kuu, kwa kweli hali ni dhohofu na kwa sababu Mahakama hizi zinatusaidia na zinaleta utulivu kwenye maeneo mbalimbali kwa sababu wananchi watakapokuwa wanaridhika na hukumu mbalimbali watafanya kazi na wachangia ustawi wa Halmashauri zetu na hatimaye Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, niunge mkono pendekezo la kuongeza umri wa kustaafu wa Wanajeshi wetu wa Magereza kwa vyeo hivi vya Koplo, lakini niombe kama walivyoongea Waheshimiwa Wabunge wengine, tuangalie kwa maeneo yote, ili tunapofanya marekebisho iwe *once for all*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Subira. Mheshimiwa Msigwa, ameomba jina lake litolewe, mambo mazuri hayataki mjadala, Mheshimiwa Mnyika! Hayupo. Sasa nimwite Mheshimiwa Shibuda.

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii na mimi niweze kutoa mawazo na maono machache kuhusu *agenda* kubwa tuliyonayo ya kurebishwa sheria mbalimbali zilizowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, patokeapo mambo kwenda ovyo ovyo, hutokea watu wakasema mbona wazee mnaacha mambo yanakwenda ovyo ovyo. Patokeapo mambo mazuri, lakini mwendo wa jongoo, hutokea watu

wakasema, wazee kaeni pembeni mwendo kasi hamwezi. Sasa naomba kwa dhamira hiyo hiyo ya makundi mawili ya mitazamo tofauti niseme machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nawapongeza dhamira njema ya kutakiwa kuwepo sheria za kutatua matatizo mbalimbali ambayo yamebainishwa na marekebisho yaliyoletwa. Dhamira inaweza kuwa ni njema sana, lakini mfumo wa utekelezaji ukawa na utata. Natambua kasoro mbalimbali zimezungumzwa na kubainishwa na upande wa Kambi ya Upinzani. Napenda kuwaomba ndugu zangu na Bunge lote hili, tukubaliane ya kwamba dini yetu ni Katiba ya Nchi, tukiendekeza mvutano wa kila mwamba ngoma huvutia kwake tunajenga utengano ambao hautosaidia maslahi ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhimiza kwa dhati kabisa, pale palipo na mawazo bora kutoka upande wa kushoto, tutambue kwamba, tunamuenzi baba wa Taifa aliyesema ya kwamba, wengi wamekataa tusiwe na mfumo wa Vyama Vingi lakini na wachache wasikilizwe. Dhamira ya hiyo ilikuwa ni kujenga maono endelevu kwa maslahi ya vizazi vya kesho na ubora wa maamuzi yetu ya leo, ubora wa kauli zetu za leo, ndiyo msingi wa ubora wa nyongeza kwa vizazi vinavyokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua maneno haya yanaweza yakatafsirisha mtazamo wa fikra hasi, lakini naamini kwamba, tuko pamoja kwa sababu subira yavuta heri na aliye na subira yuko na Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nianze na mahimizo ya busara na hekima kwa sababu ya matetemo yanayotokea katika mitazamo ya kutangatanga kwamba, huyu hafai na huyu anafaa. Hebu tujiulize sisi Wabunge humu tunalithaminisha vipi Bunge letu, kusadikika na Watanzania na Watanzania wakaona faida ya mfumo wa Vyama Vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hoja ambayo sasa tujiulize bila kuwa na hamasa ya hasira wala hamaki. Tukubaliane kwamba kukosoana ni kusahihisha na kusahihishana ni kuimarishana. Nasikitika sana tunapokuwa na jazba tu kwamba, mtu akikosea basi aadhibiwe, mwanafunzi anapofeli mtihani aliyotungiwa na Mwalimu tafsiri huwa kwamba kabainisha kasoro za hitilafu za upungufu wa kutofahamu jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hitilafu za kutofahamu jambo zikitokea, nakuomba mshauriane na Mheshimiwa Spika muwe na mfumo wa kutoa maelimisho ya kusaidia makundi kutambua kasoro na yakakosolewa kiungwana. Dhamira njema ya kukosoana kwa vijembe, haijengi inatafsirisha na kujenga hamaki za kuviziana na pale palipo na nongwa pana visasi. Kwa hiyo, niliona haya niyaseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba nijielekeze katika wigo mpana wa Katiba, matakwa ya Katiba ya Ibara ya 63(2) wajibu wa Bunge ni kuishauri Serikali na kuisimamia Serikali. Kwa masikitiko makubwa sana, Bunge leo hili limesikiliza sheria zilizowasilishwa, lakini palikuwa na sheria iliyotarajiwa ya kuongeza muda wa kufanyika mashauri ya kesi za uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pasipokuwepo na muda wa kutosha kutatuliwa tatizo hilo, linazalisha nongwa ya hisia potofu, ya mitazamo potofu, kwamba, pana ugandamizaji wa kukuzwa demokrasia na mfumo wa Vyama Vingi, pana kugandamizwa matakwa ya mashindano ya kutambulishwa kasoro za uchaguzi zifanyiwe marekebisho kupitia Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, vivyo hivyo pia napenda kumwomba Jaji Mkuu, toeni mwongozo sasa wa kuwaelimisha Mahakimu wa Mikoa na ofisi za Wanasheria wa Mikoa, watoe kauli elekezi ya kutoa subira kusubiri sheria hiyo itakuja lini dhidi ya kuachiwa maamuzi huria ambayo yanaharamisha kuthaminika Serikali ya CCM. Uharamisho huo ni pale Hakimu atakapoamua apendavyo yeye wakati itakapokuja sheria inakuwa pia na machukizo na kasoro za usumbufu kwa wale wadai haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hilo Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu alipe heshima yake, ashauriane na Jaji Mkuu, watoe mwongozo, ukimya una hatari zake. Watoe haki ya Katiba Ibara ya 18 ya kupewa habari wananchi kwa mambo yanayowahusu. Fukuto la Mtwara liwe kisomo, palikuwa na kikauli kifuniko na mwendo kifuniko, desturi kifuniko kwa uhalali wa kupewa jamii stahiki habari ambazo Rais aliweza kuja kuzitoa, hali hiyo ikawa watu wanashikwa na butwaa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia kifuniko, ni sawa sawa na mficha maradhi hufichuliwa na kifo. Natahadharisha na kuiomba Serikali itimize wajibu wake na kuwatendea haki watu ambao wamechelea sasa kuanza kusema kwamba, wale waliokuwa wameshtakiwa na kesi za uchaguzi

wanasitiriwa na Serikali na kwa sababu Serikali ni ya CCM, wateule wa Mahakama ni wa CCM, wengi Wabunge ni wa CCM, je, mtatokana vipi na dhahama ya uzushi kwamba haya yote yanatengenezwa kwa sababu ya kustiri uhafifu ama hitilafu ambazo zimo ndani ya mfumo wa uongozi. La hasha, nakuombeni mhakikishe mnaitabanaisha jamii dhidi ya fikira potofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kabisa kwamba, chuki na batili zaweza kuleta msongamano ambao unaweza ukazaa kisomo cha hitilafu mbalimbali. Lakini naomba kusema kwamba, ukweli haufunikwi na javia la aina yoyote ukabadilika kuwa uwongo. Kwa hiyo, naomba palipo na ukweli na kila mpenda Tanzania na kila anayetaka kumuenzi baba wa Taifa tuwe tayari kuyapokea kwa wito wa rai njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasoro ninayoiona ni mfumo wa uwasilishaji wa lugha. Lakini kila madhalia yana sababu zake. Ukiona vijana wa upande mmoja wana mihemko ya kauli hatarishi na zikajibiwa kwa kauli hatarishi, ni sawasawa na kichaa akikuibia nguo zako na wewe unatoka baharini kumkimbiza, hapo hapataeleweka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nawaombeni msiwe malighafi ya hila na tahira ambazo zinatokea. Nakuombeni sana au nawaomba Wabunge wote tujihadhari kuwa madhalia ya machukizo ya kutothaminisha na kusadikika Bunge letu hususan mbele ya watoto wa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukomazwa kwa hasira za makundi ya siasa, ni kwa sababu tu tunasema kwamba, nimemkomoa, nimemkomesha, umemkomesha nani?

Ugonjwa wa fikira wenye tohara za kisiasa na unyago wa kisiasa, huwa una subira patokea hitilafu. Nakuombeni tuendelee kuwa na subira dhidi ya hatarishi ambazo zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia lugha ya mahimizo ambayo ni lugha fanisi ambayo imeumba mang'amuzi na ina viarifu vya vidahizo vya kukoleza busara na hekima. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, torufi ya umoja na mshikamano ni kuheshimiana, waongozwa waheshimiwe na viongozi na viongozi watalipwa heshima. Kwa hiyo, napenda kuhimiza kwamba, tuheshimiane, kuheshimiana kumepungua sana. Lakini mkubwa akimheshimu mdogo, mdogo atapata makuzi na upendo wa kupenda kuheshimu ili na yeye aje kuwa malighafi kwa wajukuu zake. Nawaombeni sana tuepukane na tabia ya mizaha ya michakato na mikakati ya kupuuza wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea tena asiyetibu kidonda, huota kidonda ndugu, hivyo basi tusipuuze fikira za watu wachache. Ninyi mlio wengi wa Chama cha Mapinduzi kuweni shamba darasa. Kama ninyi hamtokuwa shamba darasa, mjitambue siyo mnahasi watu waliomo humu ndani, mnahasi demokrasia kwa upana wake, mnahasi siasa bora, mnahasi kuwa ni madhalia ya uongozi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niliona hili niliseme kwa sababu linazaa mdororo wa kutoheshimiana na linazaa mdororo kwa kutowajibika kwa matakwa ya Katiba ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasoro hii inabainisha kwamba, pana makundi ya fikira tasa kwa maslahi ya umma, jambo ambalo ni hatarishi kwa kuthaminika kwamba, Bunge ni kikaango cha upungufu dhulumati kwa maslahi ya umma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shibuda, twende kwenye mada, ambayo ni Muswada. *(Kicheko)*

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yah ii ni kufanya marekebisho ya jamii kujitambua iwe na maadili mema. Sasa natoa fafanuzi ya faida ya sheria zilizoletwa hapa ili ziende sambamba na kumilikishwa na kurasimishwa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko pamoja na nitaendelea kuwa pamoja nawe lakini palipo na ombwe, nitimize wajibu wa Katiba ibara 63 kukata kiu ya kuhitajika ushauri makini kwa maslahi ya kuiongoza Serikali na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, neema uliyonayo, ikikutoka, ndipo unapojuta, mtu akiibiwa pesa husikitika, Loo! Nimeibiwa pesa nasikitika! Tuna neema na sheria hizi zipo kwa ajili ya kudumisha neema kwa wanavijiji wetu katika mambo mbalimbali. Napenda kusema kwamba, amani timilifu ni pale panapokata kiu ya haki. Kwa hiyo, sheria hizi, twende nazo na nawaomba hasa namwomba Waziri Mkuu, ahimize Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kuwa patanifu na kuheshimiana kwamba, mihimili mitatu inayojenga shirikisho la Dola ni Bunge, Serikali na Mahakama. Lakini ni kiasi gani Wabunge sheria zikipitishwa hapa wanatambulika kwamba na wao wana mawazo

kikolezo, kwa maslahi ya kuhakikisha maadili mema yanapatikana ndani ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia, palipo na haja ya udadisi, basi ni bora pakawa na hekima ya kuvumilika kwa yale yanayohitajika. Hifadhi ya amani na fikira za waongozwa zikiwa na kasoro, ambaye ni mwalimu, basi atumie subira na lugha ya staha kuhakikisha wale wanaohitaji kukosolewa wanaelimika na kupokea kasoro za kukosolewa kwa utamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kusema kwamba, Serikali huleta marekebisho ya sheria, hii ni jitihada ya kutunza uaminifu na utiifu wa kusadikika Serikali. Lakini vile vile Bunge tuna wajibu wa kuhakikisha tunaendelea kudumisha imani ya umma. Sasa naomba tujiulize, kwamba, je, siri ya mafanikio ni kitu gani? Siri ya kufanikiwa ni desturi imara ya kuheshimiana, ya kuthaminiana na kupeana mawazo ambayo yana desturi imara ya tabia za kupendana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kusema kwamba, Mihimili yetu mitatu tusipoangalia, tutakuja kuzaa mifarako kwa sababu ya mwamba ngoma, wakati sote tunajenga nyumba moja kama anavyosema Mheshimiwa Rais wetu. Changamoto ya kuzaa michakato ya kufarakana, ni ufunuo ambao kwa kweli kuna mdudu mmoja anaitwa, dhulumati! Je, kila mmoja ajiulize, ametoka kwenye Bunge hili ana dhamira ya kumsaidia mwenzake awe mwelevu au ametoka anashangilia kwamba fulani leo nimemkosoa kwa dhihaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, chemsha bongo nawaomba ndungu zangu wa Kamati ya Bunge la CCM, hebu mkae mtafakari, mnasaidiaje kukuza utulivu wa fikra za wachache. Mnaondoaje dhana ya wachache kuhisi wanaonewa? Tukiondoa dhana hizo, maadili mema ya kuthaminika na kusadikika Bunge letu, yatakuwa yamekomaa. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo, palipo na dhuluma kiu ya kudai haki huendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shibuda nakushukuru sana.

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Masihara tuyaepushe, tutekeleze wajibu wetu. Amina, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Shibuda, nakushukuru sana. Sasa mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Celina O. Kombani, Waziri!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba nami nianze kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye mada, Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika ukurasa wa tisa, naomba kununukuu hayo aliyoyasema:

"... madhumuni na shabaha ya mapendekezo hayo, marekebisho haya yana kusuduo la kufuta sifa za Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, ili kuwawezesha Mahakimu Wakazi na Mahakimu wa Wilaya, kusikiliza kesi katika Mahakama za Mwanzo".

Mheshimiwa Mwenyekiti, akaendelea: “Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya ni mfano mwingine wa jinsi ambavyo Serikali ya CCM haina tena uwezo wa kutekeleza shughuli za nchi kwa weledi na baada ya tafakari ya kutosha ya masuala ya kitaalam na kisera, kwanza, mapendekezo haya yanadhihirisha kwamba Serikali hii na hata Mahakama ya Tanzania, kama mhimili mmojawapo wa dola haina sera ya rasilimali watu, yaani (*manpower policy*)”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ina sera makini ambayo ni *manpower policy*, sera hiyo inaitwa Sera ya Ajira katika Utumishi wa Umma, ikiwemo Mahakama ambayo inaitwa Sera ya Menejimenti ya na Ajira katika Utumishi wa Umma, kama ilivyorekebishwa mwaka 2008. Kwa hiyo, sera ya Chama cha Mapinduzi ipo na inatekelezwa kwa makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sera hiyo, inataja sifa za msingi, za ajira, inaweka miundo ya utumishi. Chini ya sera hiyo, kila mhimili wa dola ikiwemo Mahakama, Bunge pamoja na utawala inatoa sera ambazo zinalingana kabisa, haziendi kinyume na sera hiyo ya Menejimenti na Ajira ya mwaka 2008. Kwa hiyo, mihimili yote hii ina *manpower policy*. Sivyo kama alivyopotosha ndugu yangu, Waziri Kivuli wa Upande wa Upinzani. Kwa hiyo, hiyo *manpower policy* ipo, na akitaka tunaweza tukampatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ameongelea kuhusu miundo ya Utumishi. Jamani katika miundo ya utumishi, haiko *static,* miundo ya utumishi inabadilika mara kwa mara. Inabadilika kulingana na mabadiliko ya kiuchumi, kisayansi, kiteknolojia na kijamii pia. Tanzania siyo kisiwa, kwa hiyo, mabadiliko ya miundo ya utumishi (*scheme of service)* inabadilika kulingana na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sioni dhambi kwa Mhimili wa Mahakama, kubadilisha Muundo wa Utumishi na kusema kwamba Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo awe na digrii, sioni dhambi. Kwa sababu, sasa hivi wapo wasomi wengi wenye *degree*, kama wapo kwenye soko la ajira, kwa nini tuendelee kuajiri waajiriwa wenye diploma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali ambalo ameliuliza kijana wetu, upande wa Upinzani, kati ya Mkosamali au, kwa kuwa nachanganya majina yao, ni kwamba, je, hao wenye *Diploma* watakwenda wapi? Wenye *Diploma* na wenye *Degree* wote watakwenda pamoja. Tunasema kuanzia sasa, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, atakuwa na *Degree*. Wale waliopo wanaendelea kama kawaida, wale ambao ni *trainable* tutawapeleka shule watajiendeleza, wale ambao siyo *trainable* watabaki kwenye kada zile na kufanya kazi na wataji–*phase out* pole pole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo mara ya kwanza, tumefanya hivi kwa watumishi wa umma mbalimbali, zamani tulikuwa tunaajiri darasa la saba, baada ya muda tukasema kwa kuwa kidato cha nne wapo wengi, mhudumu lazima awe kidato cha nne. Wale ambao ni darasa la saba na wako katika kada hii, wale *trainable* waende mashuleni, waende vyuoni, wafanye mitihani na

wale ambao siyo *trainable* wabaki katika kada zile watajiphase out* polepole. Niwaulize Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi wale darasa la saba, wahudumu na katika kada mbalimbali hamwoni kwamba wameshaji-*phase out* na wameondoka katika *system* pole pole?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na walimu wa UPE, walimu wa UPE walikuwa darasa la saba, ilikuwa ni *crush program*, lakini baada ya muda, tuliwapa muda maalum, kwamba wajiendeleze, wafike kidato cha nne, ili waweze kuwa Walimu wa daraja la 3A. Tumefanya hivyo baada ya muda, ambao ni *trainable* wamekwenda shule, asilimia 90 ya Walimu wamejiendeleza, wamefika kidato cha nne, wengine kidato cha sita, wamekwenda mpaka kwenye *Diploma*, mpaka kwenye *Degree* na *Masters*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hicho siyo kitu kigeni, tunashangaa nini kwa Mahakimu, naona tusishangae! Tunasema kwamba, wale wa Lushoto na wale wenye *Diploma* watakwenda wapi? Tutabadilisha muundo wa utumishi, watakuwa Makarani wa Mahakama na wasaidizi wa Mahakimu wa Mahakama na hao watasaidia sana Mahakimu kwa sababu watajua a,b,c za Mahakama. Kumwajiri *form four* au *form six* ambaye hajui lolote kuhusu Mahakama na kumuajili mwenye *Diploma* ya Lushoto au *Certificate* ya Lushoto, je, yupi atafanya kazi vizuri zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, muda wa Utumishi wa Mahakama nao tutau-*prolong* kama ilivyo kwa Walimu. Mnaona Walimu sasa hivi *Certificate holder* yeye ni Mwalimu *grade* A, mpaka anafikia *principal*. Akipata *Diploma*, anakuwa Afisa Elimu Msaidizi, akipata *Degree*, anakuwa Afisa Elimu. Sasa hivyo hivyo kwa Mahakimu,

tutarekebisha muundo ili uendane na hali ya sasa hivi. Kwa hiyo, jamani, naomba tusikione ni kitu cha ajabu, ni kitu cha kawaida na wenzetu, Afrika Mashariki nzima, wameshaweka muundo wa utumishi wa Hakimu, mtu anayeitwa Hakimu lazima awe na na *first degree*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niende upande unaohusu ajira za mkataba. Ingawa iko nje ya mada, kwa sababu katika, hiyo *miscellaneous amendment,* hawakueleza habari za mikataba, wala ajira za Majaji. Mikataba ya Majaji, Ajira za Majaji, lakini nipende tu kuwaelewesha Wabunge wenzangu. Jana nilijibu swali, kwamba iwapo Waraka wa Rais namba moja (1) wa mwaka 1998, kipengele cha 12(2) kinasema wazi kwamba: "Iwapo Serikali inamhitaji mtaalam fulani au mfanyakazi fulani, inaweza ikampa mkataba".

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo kwa Majaji, naomba msome Katiba, naomba msome Katiba, Ibara ya 110 (3), inasema wazi, iwapo Rais anaona huyo Jaji, amefikia miaka 60 na bado anahitajika, anaweza aka-*extend* muda wake wa kufanya kazi. Kwa hiyo, hilo ni kwa ajili ya kuelewesha umma tu, ingawa haliko kwenye mada wala kwenye hiyo *miscellaneous amendment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechanganya kidogo mada, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ameeleza kwamba, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo anateuliwa. Kuna nafasi za uteuzi na nafasi za ajira jamani. Hivi mamlaka ya uteuzi ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ni ipi? Yule anaajiriwa siyo anateuliwa. Kwa hiyo, kuna *rank* kabisa za Mahakimu wanaoajiriwa, anaajiriwa Mahakama ya Mwanzo, anapata *promotion,* anakwenda Mahakama ya

Wilaya, anakwenda anakuwa Hakimu Mfawidhi, baada ya hapo, kuna Wasajili, Wasajili wengine ambao ni wa kanda mbalimbali, uteuzi wao ni Jaji Mkuu. Uteuzi wa Majaji, pamoja na Msajili wa Mahakama Kuu, Msajili wa Mahakama ya Rufaa na Msajili Mkuu, ni Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusichanganye, *employment* na *appointment*. Ni vitu viwili tofauti, nafikiri, Mwanasheria, Mheshimiwa Tundu A. Lissu, angebidi atofautishe vitu hivi, kwamba Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, hateuliwi, anaajiriwa. Anakwenda kwa *promotion* mpaka akifikia *rank* fulani ndipo anapoteuliwa. Hivyo, kuna nafasi za uteuzi na kuna nafasi za ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kuliongelea, hilo naliomba tu, kwamba Waheshimiwa Wabunge tuwe tunachangia mada husika, tusitoke nje ya mada. Tukitoka nje ya mada tunawapotosha Watanzania na sisi upande wa Serikali, inabidi tujibu hoja ambazo haziko kwenye mada, kwa mfano mikataba ya Majaji, haikuwa kwenye mada; *promotion* za Mahakimu hazikuwa kwenye mada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba na sisi upande wa Serikali muwe mnatulinda na Waheshimiwa Wabunge, ili tuwe tunajadili mada, ndani ya mstari na siyo nje ya mstari. Mheshimiwa John P. Shibuda, ametoa maneno ya hekima kidogo, naona yametusaidia kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru na ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kusema kwamba, naunga mkono mada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimesimama ili kuweka ufafanuzi wa hoja mbili kubwa ambazo zimeelekezwa Wizara ya Fedha na Waheshimiwa Wabunge wawili. Moja, ni ile mada ya madeni ya Taifa, ambayo kwa kiwango kikubwa jana, nilishazungumza, lakini kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge pengine itafaa, wapate dodoso kidogo, juu ya aina gani ya mikopo na kupata matumaini kwamba, tunawekeza katika miradi ambayo inalenga kuboresha uchumi wa nchi hii. Hatuwekezi katika maeneo ya kula, nitawapeni mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewekeza katika bomba la gesi ambapo tumekopa 1.225 billion *dollars*. Katika mkopo huo, ni mkopo nafuu, ambao ni dola milioni 930, huo ni *concessional loan. Commercial loan*, ni dola 245 na hela ya ndani ni dola milioni 60. Kwa hivyo tumekopa tuwekeze kwenye gesi ili nchi hii tuweze kuwa na umeme wa kutosha, tuongeze viwanda, tuongeze uzalishaji, tuongeze ajira, kwa hiyo, tunakopa kwa malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tumekopa ili tuweze kuboresha hali halisi ya maji, tumekopa, *Euro* milioni 40, ili tuwekeze mitandao mizuri ya maji, pale Bukoba na Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, tumekopa milioni 178.25 *million dollars*, ili tuweke mtandao wa maji, Ruvu, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, tumekopa milioni 29.14 *dollars*, kwa ajili ya kujenga madaraja matatu ya Malagarasi ili kuimarisha njia ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, tumekopa, milioni 60 *dollars*, ili tuweze kujenga mkongo ambao utaimarisha mawasiliano katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, tumekopa, *dollar* au *US$*167.6 milioni, kwa ajili ya kuboresha, miundombinu ya *Local Government.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tumekopa, milioni 45 *Euro* na milioni nyingine 51 *Euro* kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maji, pamoja na barabara, katika miji yetu midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumekopa, *Euro* milioni 22 kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji, katika maeneo ya Lindi, Kigoma na Sumbawanga. Hii natoa mifano ya miradi mikubwa ambayo tumewekeza kwa kukopa, ili baadaye *infrastructure* ya Tanzania iweze kuwa ahueni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaungana nami kwamba, tukiwekeza katika miundombinu na kuboresha *infrastructure*, hali ya Tanzania itakuwa imejengeka kwa ajili ya kuimarisha na kuanzisha viwanda na huduma bora kwa ajili ya nchi yetu. Tuwekeze katika miundombinu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ni hoja toka kwa Mheshimiwa John Cheyo, kwamba mpaka sasa, Wizara ya Fedha haijatoa hata senti moja kwa ajili ya *development*

*expenditure* na vile vile *OC*. Ninazo takwimu hapa kwa ruhusa yako nisome ili tuone ukweli uko upande gani. Sisi tunao ukweli kwamba, ni kweli kwa upande mmoja, hatujatoa asilimia mia moja kama ilivyotarajiwa, lakini si kweli kwamba hatujatoa hata senti moja, kwa sababu tuna takwimu zilizopo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, tuna takwimu ambazo zinaonesha kwamba *development expenditure* ambayo imeidhinishwa ni *2.08 Trillions* ambazo tunatakiwa kutoa pesa mpaka mwisho wa mwaka, lakini mpaka wiki iliyopita tarehe 31, mwezi Januari, tumetoa bilioni 853.5. Kwa hivyo, hii siyo *zero disbursement,* hii ni *substantial disbursement* ambayo ni *853.5 billion*. Kwa Miradi mbalimbali, ni kweli kuna maeneo hawakupata asilimia kubwa walivyotarajia, lakini katika miradi mingi mikubwa tumefanya *disbursement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiende kwenye *OC*, hakuna aliyepata chini ya asilimia 45 na wengi wamepata kuanzia asilimia 60 na kuendelea mpaka asilimia *80* ya walichokuwa wanatarajia. Kwa hivyo, *data* zote ninazo hapa, kwa ruhusa yako kwa wanaohitaji tunaweza tukawapa ili wote tufahamu kwamba kitu gani kimetolewa, nani amepata na *data* zote ninazo ili hata mtu anapotaka kujua Wilaya yake imepata kitu gani, aone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Sasa namwita Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kuchangia maeneo kadhaa, kwenye Muswada huu ulioko mbele yetu, Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na nianze kuchangia sehemu ya pili ya Muswada huu inayohusu Marekebisho ya Sheria juu ya Sheria ya Fedha Haramu, kwa maana ya *amendment of the Anti Money Laundering Act, Cap* 423.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masuala kadhaa ambayo ningependa kwa kweli kauli ya Serikali katika majumuisho juu ya marekebisho haya yanayokuja, marekebisho yanayohusu jambo linalohusiana na fedha haramu zinazohusishwa na masuala ya ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kwamba, kwenye Bunge hili, katika Mkutano wa Bunge Kikao cha tarehe 3 Februari, 2012, Bunge lililetewa Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha Haramu, sasa ningependa kauli ya Serikali na maelezo ya Serikali, ni kwa vipi mwaka mmoja tu uliopita, mwezi Februari kama huu, tulifanya marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha Haramu lakini kifungu hiki hakikuletwa wakati ule, kwa sababu tunakuwa tunarudiarudia mara kwa mara, tunapoteza fursa ya kwenda kurekebisha sheria nyingine ambazo zinahitaji marekebisho, kwa sababu tu marekebisho yanapoletwa hatuyaangalii mambo kwa upana wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuletwa kwa marekebisho haya wakati huu, ukilinganisha na mambo mengine ambayo tumekwishayajadili katika Mkutano huu wa Bunge, inaonesha kwamba, kuna mambo ambayo yanaletwa

yenye mwelekeo kidogo wa shinikizo kutoka nje kuliko ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atueleze kwamba uamuzi wa kuleta kifungu hiki, kama ulikuwa uamuzi wa kwetu ama tumepewa masharti katika kuweka kifungu hiki wakati huu. Nitaomba vilevile majibu kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kama marekebisho haya yangekuwa ni ya kwetu peke yake, ni kwa nini katika hatua hii hatukuletewa mapendekezo ya marekebisho ya jambo ambalo lilitokea tarehe 3 Februari, 2012, tulipojadili Muswada wa Sheria hii ya *Anti Money Laundering (Miscellaneous Amendment)* wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka tarehe 3 Februari, 2012, niliwasilisha mapendekezo ya marekebisho yaliyokuwa yanalenga kurekebisha hii Sheria ya Fedha Haramu ili kuongeza ukubwa wa adhabu na wakati ule tulileta marekebisho mimi na Mheshimiwa Felix Mkosamali, ya kuongeza ukubwa wa adhabu kwa watu wanaobainika kujihusisha na fedha haramu, isiwe tu adhabu ya kifungo peke yake, bali kuwe na adhabu inayolingana vile vile na ukubwa wa makosa yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ambayo yaliletwa na Mheshimiwa Felix Mkosamali yalikataliwa, mapendekezo ambayo niliyawasilisha mimi, yalikubaliwa na Bunge. Baada ya Muswada kusomwa kwa hatua zake zote tatu, hatua ya kwanza, hatua ya pili na hatua ya tatu na ukawa umepitiswa kwa hatua zake zote tatu, tulipokuwa tunaelekea mwishoni, maamuzi yamekwishafanyika na Mkutano wa Bunge unakaribia kusitishwa, mwongozo

ukaombwa na Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, kuhusiana na kifungu ambacho kilishapitishwa na Bunge tayari na Mwenyekiti wa Bunge, kinyume kabisa na Kanuni akatoa kauli mwishoni kwamba, marekebisho yale yaliyopitishwa na Bunge, yamefutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naelewa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa mujibu wa taratibu na Kanuni zetu, Bunge likishafanya maamuzi namna pekee ya kuyageuza ni kupitia ama hoja ya mabadiliko au kuletwa kwa marekebisho. Sasa ni kwa nini tulipoletewa huu Muswada sasa hivi unaohusika na *Anti Money Laundering*, Serikali haikutoa maelezo kuhusu namna gani ilifumbua utata uliojitokeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie katika eneo hili, kwa kusisitiza tu, masuala haya ya fedha haramu, sheria sawa ni muhimu na tuwe na sheria za kudhibiti ikiwemo fedha haramu za masuala ya ugaidi, lakini utawala wa sheria, kwa maana ya kuzisimamia sheria zenyewe sasa ndiyo jambo muhimu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, utakapohitimisha hoja hii, tarehe 3 Februari, 2012 tulikuainishia maeneo ambayo tunaona kwamba kuna mianya ya fedha haramu na kashfa mbalimbali za masuala ya fedha haramu. Kwa kuwa sasa mwaka mmoja umepita na Serikali iliahidi kuongeza nguvu zaidi baada ya marekebisho tuliyoyafanya, katika majumuisho ya hoja, pamoja na ufafanuzi, Serikali ieleze imechukua hatua gani kutoka mwaka mmoja uliopita, tulipozibadili Sheria za Fedha Haramu kuiongezea nguvu Serikali katika kukabiliana na tatizo hili la fedha haramu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye eneo lingine, nalo ni lile linalohusu masuala ya Sheria hizi za Mahakama, kwa maana ya *amendment of the Magistrate Court Act, Cap. 11.* Kuna mapenedekezo mengi ambayo yamewasilishwa, sijaridhika na mchango wa maelezo yaliyotolewa na Waziri, kuhusiana na hoja zilizotolewa na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ndiye mtoa hoja, ikifika nafasi ya kujibu hoja hii, ni muhimu hoja zile zikajibiwa kwa umakini na zikajibiwa kwa ufasaha ili tuelewe kwamba, sheria hii tunayoipitisha isije ikaleta mgogoro katika mfumo mzima wa Kimahakama na *hierarchy* nzima ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kuna mapendekezo mapya tumeletewa ya maeneo mbalimbali ya marekebisho ya sheria hii na kuna mapendekezo tumeletewa ya kuibadili sheria, kuondoa lugha zinazotumika. Sheria iliyokuwepo awali, lugha ilikuwa ni Kiswahili, sasa tunataka kuleta marekebisho ya kuweka lugha, kuwa ni Kiswahili au Kiingereza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili katika Mikutano yake iliyopita, lililetewa Mikataba inayohusiana na masuala ya lugha, Mkataba wa Afrika Mashariki na siku ile Wabunge wa pande zote, kila upande na hata upande wa Serikali ulionesha umeguswa sana na lugha ya Kiswahili na ukaweka dhamira ya kwamba, sasa tunavyokwenda mbele, tutakipa kipaumbele Kiswahili kwenye mifumo yetu ya kisheria na mifumo yetu ya Kimahakama. Inashangaza kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuleta mapendekezo ya marekebisho ya kuturudisha nyuma! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana kwamba, ya kwenda kukipa kipaumbele Kiingereza kwa kutaka kitumike kwenye Mahakama zetu na sasa tunakwenda kwenye Mahakama za chini zaidi ambazo zitakuwa na athari kubwa sana kwenye utoaji wa haki, kama wale watu wanaoongoza zile Mahakama wakiamua kutumia mwanya huo wa kisheria kuchagua lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kupeleka tatizo kwenye Mahakama za chini, hizi za Mwanzo ambazo zinaathiri wananchi kule vijijini, kwenye Tarafa, kwenye Kata zetu na maeneo mbalimbali kwenye Majimbo yetu. Sikubaliani kabisa na haya marekebisho ambayo yameletwa ya kuongeza masuala haya ambayo yanaturudisha nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumeletwa pendekezo hapa la kuweka mipaka ya Wazee wa Mahakama ama Washauri wa Mahakama katika masuala ya baadhi tu ya kesi za madai au kesi za daawa na kesi nyingine, lakini, haya mapendekezo yaliyoletwa kwenye marekebisho kifungu cha tisa, yamejikita kwenye upande mmoja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sisi tunaamini na kama Serikali inaamini, kwamba imepanua wigo wa kitaaluma kwenye Mahakama za Mwanzo kama inavyotaka kudaiwa sasa kwamba Mahakama za Mwanzo na zenyewe zitakuwa na wataalam, ni kwa nini wigo huu wa wazee wa Baraza unakwenda kuminywa kwenye eneo moja tu kama ambavyo mapendekezo yameletwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini sasa kama tunaamini Mahakimu wanaokwenda kwenye Mahakama za Mwanzo, kama sasa watakuwa na uwezo, ni kwa nini ushauri huu wa Wazee wa Mahakama usiwe ushauri na maamuzi yakawa ya Hakimu. Tunaamua ku-*deal* na suala moja tu la kesi zinazohusiana na masuala ya kiimani peke yake. Kwa nini wigo huu hatuzami kwa upana wake kwa kuzingatia masharti vilevile ya Katiba ya nchi? Hili ni jambo ambalo ningeomba vilevile lizingatiwe katika majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba maelezo vile vile kutoka kwa Serikali, kama tumeamua kupeleka Mahakimu wenye ngazi ya shahada mpaka Mahakama za Mwanzo, suala ambalo bado tutahitaji maelezo, kwa kuzingatia masuala ambayo yamehojiwa na Kambi ya Upinzani, lakini kama uamuzi uko hivyo, ni kwa nini vile vile, Serikali haikuleta mapendekezo ya marekebisho ya sheria, ili mawakili na waendesha mashtaka nao waliokuwa wamezuiliwa kwenda kwenye Mahakama za Mwanzo, nao wakapewa uhuru wa kwenda kwenye Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunakwenda kupeleka Mahakimu wenye uwezo, lakini bado tumeziba mianya ya watetezi wa haki kwenda kushirikiana na Mahakimu katika kuhakikisha kwamba haki inatendeka kuanzia Mahakama za chini. Kwa hiyo, ni vizuri Mwanasheria Mkuu wa Serikali, binafsi nilitaka kuleta jedwali la marekebisho ya sheria, lakini ilionekana kwamba jambo hili liko mbali sana na mapendekezo yaliyoletwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa Muswada huu ni wa Serikali, nitaomba Serikali iwasilishe marekebisho, ili Mawakili nao na Waendesha Mashtaka, kama haki ilivyopanuliwa kwa Mahakimu na wenyewe waweze kupewa haki hizo waweze kwenda kusimamia masuala ya haki kwenye Mahakama zetu kwenye ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zilizotolewa na Wabunge wenzangu kwenye masuala yanayohusu marekebisho ya Sheria za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali, iwe ni hesabu za Serikali za Mitaa, iwe ni hesabu za Serikali za Mashirika ya Umma, iwe ni hesabu za Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu tuliokuwa nao sasa, pamoja na kuwa kuna marekebisho kadhaa yanayohitajika, lakini ni utaratibu ambao umefungua mianya ya uwajibikaji, ninachokiona hapa, ni Serikali ambayo inashindwa kuwajibika kwa wakaguzi wanapokwenda kwenye ukaguzi, Maafisa Masuuli wanashindwa kujieleza wakati Wakaguzi wanapokwenda, wanakuja kujieleza baada ya ripoti kuwa zimewasilishwa kwenye vyombo vya usimamizi, hii siyo sahihi. Tunaachia uzembe uendelee, tunaachia ufisadi ulindwe na muda mrefu zaidi uchukuliwe wa kushughulikia masuala haya ya ufisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taratibu za kikaguzi, Mkaguzi anapokagua, kabla hata ya kupeleka taarifa kwenye mamlaka nyingine, anarudisha kwa menejimenti, menejimenti iandike ripoti yake, iandike maoni yake, maeneo mengi yanayokaguliwa, menejimenti zikipelekewa ripoti ya ndani ya Mkaguzi, ripoti ya awali ya Mkaguzi,

hazijibu hoja, zinaachia hoja ziendelee, hoja zinajitokeza, zinakuja mpaka zinafika Bungeni, halafu baadaye ndiyo wanakumbuka shuka ama kwa vielelezo halali au kwa vielelezo vya kughushi, wanakuja kusema kuna vielelezo vilisahaulika, wanakuja kuchakachua.(*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri marekebisho haya yanayotaka kufanyika yasiachie mianya ya namna hiyo na tutarudisha nyuma jitihada za mapambano dhidi ya ufisadi kwenye rasilimali za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu hii ya Sheria ya Ardhi, ambayo ni sehemu ya nane ya marekebisho yanayohusiana na Ardhi ya Vijiji na yanayohusiana na ardhi kwa ujumla wake, kuna marekebisho kadhaa hapa yanayohusu masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hukumu moja ya Jaji Fauz Twaib, hukumu ya *Emmanuael Malangisi* akiiwakilisha bwana mmoja anaitwa *Anastotis Agusto*, raia wa Ugiriki, hukumu iliyokuwa dhidi ya Kabidhi Wasii wa Serikali kwenye migogoro iliyohusu Ardhi.

Tumekuwa tukielezwa mara kwa mara kwenye Bunge letu kwamba, sheria yetu ya ardhi inakataza wageni kumiliki ardhi, kwa mujibu wa sheria, lakini sheria ile ina makatazo makali zaidi kwenye hati ya pembeni ya sheria, kwenye maudhui ya msingi ya sheria yenyewe, sheria haijakataza waziwazi wageni kumiliki ardhi, kwa kurithi. Kwenye hukumu hii niliyotaja, Mahakama ilimpa haki raia wa kigeni kumiliki ardhi wakati yeye siyo Mtanzania na sababu ya Mahakama kufika maamuzi haya ni kwa kuwa sheria yetu ina udhaifu

kwenye kile kipengele, haikugusia masuala ya umiliki wa ardhi za mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunabanwa Wabunge kuleta marekebisho katika hatua hii kwa Muswada ambao umeshaletwa na Serikali. Ningependa kauli ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ili azingatie marekebisho hayo, kuepusha wageni kurithi ardhi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilipokuletea *notice*, sikuwa namaanisha kuchangia katika hoja ambayo iko mezani, lakini nilikuwa na suala linalohusu utaratibu ambalo nilipenda kulileta mbele ya Bunge lako Tukufu. Kama unaniruhusu niendelee na suala hilo, naomba basi sasa nitumie Kanuni ya 64.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigwangalla, hoja iliyoko mbele ya Bunge hili, ni Muswada, naomba tuzingatie tunachangia Muswada, umeniomba nikakwambia nitakupa dakika 15 uchangie Muswada ambao uko mezani. Kama una lingine, uko muda wake wa hilo lingine.

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi kulikuwa na Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed ambaye aliomba Mwongozo na Mheshimiwa James Mbatia waliomba Mwongozo na miongozo yao mpaka sasa hivi inafanyiwa kazi. Kwa sababu tunataka majibu ya kitaalam na wataalam sasa hivi wanashughukia, naomba wawe na subira, ikiwa tayari mtajulishwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umebaki nusu saa, lakini wachangiaji wamekwisha na muda huu hautoshi kwa Serikali kutoa majibu kwa hoja nyingi ambazo zimeulizwa hapa ndani. Kwa maana hiyo, naliahirisha Bunge mpaka kesho sasa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.17 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 8 Februari, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*